

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 30 Januari, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt.Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, Katibu.

**KIAPO CHA UAMINIFU**

Wabunge wafuatao waliapa:-

Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro.

Mhe. Justin Joseph Monko.

Mhe. Stephen Lemomo Kisurwa.

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninayo taarifa ya Mheshimiwa Spika. Taarifa ya kwanza ni ya kuhusu kifo cha Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu Bunge letu lilipatwa na msiba mkubwa wa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Marehemu Leonidas Tutubert Gama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini ambaye alifariki tarehe 23 Novemba, 2017 katika Hospitali ya Peramiho. Marehemu Leonidas Tutubert Gama alizikwa tarehe 27 Novemba, 2017 katika Kijiji cha Likuyu Fusi, Manispaa ya Songea, Mkoani Ruvuma.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa kifo hiki kilitokea wakati sisi hatupo hapa Bungeni, naomba sasa sote tusimame kwa muda wa dakika moja ili tuweze kumkumbuka aliyekuwa Mbunge mwenzetu.

*(Hapa Wabunge walisimama kwa dakika moja kumkumbuka aliyekuwa Mbunge wa Songea Mjini Marehemu Mhe. Leonidas Tutubert Gama)*

**NAIBU SPIKA:** Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi, amina.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa nyingine inatolewa chini ya Kanuni ya 33 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2016. Katika Mkutano wa Tisa wa Bunge, Bunge lilipitisha miswada minne ya Sheria ya Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania wa mwaka 2017 (*The Tanzania Telecommunications Corporation Bill, 2017*);

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa mwaka 2017 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 4, Bill 2017*);

(iii) Muswada wa Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania wa mwaka 2017 (*The National Shipping Agencies Bill, 2017*);  
na

(iv) Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya wa mwaka 2017 (*The Drugs Control Enforcement Amendment Bill 2017*).

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa hii, mnataarifiwa kwamba tayari Miswada hiyo minne imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria za nchi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa zinaitwa:-

(i) Sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania Na.12 ya mwaka 2017 (*The Tanzania Telecommunications Corporation Act No. 12 of 2017*);

(ii) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 na Na.13 ya mwaka 2017 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments No. 4, Act No.13, 2017*);

(iii) Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania Na.14 ya mwaka 2017 (*The National Shipping Agencies Act No.14, 2017*);  
na

(iv) Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na.15 ya mwaka 2017 (*The Drugs Control and Enforcement Act No.15 of 2017*).

Waheshimiwa Wabunge, pia kuna taarifa ya Mheshimiwa Spika kuhusu matokeo ya michezo ya Mabunge ya Afrika Mashariki. Kama mnavyofahamu Michezo ya Nane ya Mabunge ya Nchi za Afrika Mashariki yaani *Inter-Parliamentary Games* kwa mwaka 2017 ilifanyika kuanzia

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

tarehe 1 hadi 11 Desemba, 2017 Jijini Dar es Salaam ambapo Bunge la Tanzania lilikuwa mwenyeji wa michezo hiyo ambayo ilihusisha michezo ya riadha, mpira wa miguu, mpira wa pete, mpira wa wavu, kuvuta kamba, kutembea kwa kasi na gofu. Katika michezo hiyo, matokeo ya timu yetu ya Bunge la Tanzania yalikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Riadha Wanawake, Bunge la Tanzania tulikuwa wa kwanza. *(Makofi)*

(ii) Kutembea kwa haraka wanawake mshindi wa kwanza. *(Makofi)*

(iii) Mpira wa miguu mshindi wa pili. *(Makofi)*

(iv) Kuvuta kamba wanaume mshindi wa kwanza. *(Makofi)*

(v) Kuvuta kamba wanawake mshindi wa pili; *(Makofi)*

(vi) Mpira wa wavu wanaume mshindi wa pili; *(Makofi)*

(vii) Mpira wa wavu wanawake mshindi wa pili. *(Makofi)*

(viii) Mpira wa pete mshindi hakutangazwa baada ya baadhi ya matokeo kulalamikiwa. Hata hivyo, timu ya Tanzania iliongoza kwa kushinda michezo yote mitatu iliyocheza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na matokeo hayo, baadhi ya wachezaji wa timu ya Bunge letu walifanikiwa kutunukiwa medali kwa uchezaji na ushiriki bora kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete ambaye alitunukiwa Medali Maalum ya Ushiriki wa Michezo. Ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

(ii)Huwa ni kazi ngumu sana kujisemea mwenyewe, lakini wa pili ni Naibu Spika ambaye alipata Medali ya Dhahabu, mshindi wa kwanza kutembea kwa haraka. *(Makofi/Vigelegele)*

(iii) Mheshimiwa Yosepher Ferdnand Komba ambaye alipata Medali mbili za Dhahabu. Medali hizi alikuwa mshindi wa kwanza katika mbio za mita 800 na pia mita 1,500. *(Makofi/Vigelegele)*

(iv) Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, alipata Medali ya Fedha, mshindi wa pili mbio za mita 100. *(Makofi/Vigelegele)*

(v) Mhe Rose Cyprian Tweve, Medali ya Shaba, mshindi wa tatu mbio za mita 100. *(Makofi/Vigelegele)*

(vi) Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, Medali ya Fedha, mshindi wa pili mbio za mita 200 na mita 400. *(Makofi/Vigelegele)*

(vii) Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, mchezaji bora wa mpira wa wavu wanaume. *(Makofi/Vigelegele)*

(viii) Mheshimiwa Jesca David Kishoa ambaye alikuwa ni mmalizaji mzuri wa mpira wa wavu kwa wanawake. *(Makofi/Vigelegele)*

Aidha, katika mbio za mita 1,600 za kupokezana vijiti, Tanzania ilipata Medali ya Dhahabu kwa kuwa mshindi wa kwanza ambapo waliohusika ni Naibu Spika, Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika anawapongeza sana sana Wabunge wote walioleta medali na kuleta heshima kwa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia anawahimiza Wabunge wengine ambao hawashiriki michezo kikamilifu kuanza mazoezi wakati huu wa Bunge ili waweze kushirikiana na Wabunge wenzao kuhakikisha Bunge letu linazidi kupata heshima na wale ambao wamepata medali basi waendeleo kujifua zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo ilikuwa taarifa ya Mheshimiwa Spika Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**NAIBU SPIKA:** Hati za kuwasilisha mezani, Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 5 wa mwaka 2017 [*The Written Laws Miscellaneous Amendments*] (No. 5) Bill, 2017]

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA-MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 5 wa mwaka 2017 [*The Written Laws Miscellaneous Amendments*] (No. 5) Bill, 2017]

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mtolea

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA - MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 5 wa mwaka 2017 [*The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 5) Bill, 2017*]

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na.1

**Kuwasaidia Vijana Walioathirika na Dawa za Kulevya**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR (K.n.y. MHE. IBRAHIM MOHAMEDALI RAZA)** aliluliza:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua kwa kuwasaidia vijana walioathirika na matumizi ya dawa za kulevya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Mohamedali Raza, Mbunge wa Kiembe Samaki kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua tatizo la matumizi ya madawa ya kulevya na athari yake kubwa kwa nguvu kazi ya Taifa letu ambayo asilimia kubwa ni vijana. Katika kukabiliana na tatizo hili, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imechukua hatua kadhaa kuwasaidia

vijana na makundi mengine walioathirika na matumizi ya dawa za kulevya. Hatua hizo ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Kutoa tiba kwa waathirika ambapo hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2017 jumla ya vituo vitno vya tiba (*methadone*) kwa waathirika wa dawa za kulevya vilikuwa vimeanzishwa nchini katika Hospitali za Muhimbili, Temeke, Mwananyamala, Zanzibar na Mbeya. Kupitia vituo hivyo, jumla ya waraibu 5,830 walipatiwa tiba na wengine wanaendelea kupatiwa matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mwaka huu wa 2018, Serikali inatarajia kufungua vituo vipya vya tiba katika Mikoa ya Mwanza na Dodoma. Kutokana na utafiti uliofanywa mwaka 2014, Serikali imepanga kufungua vituo vya tiba katika Mikoa ya Pwani, Morogoro, Arusha, Kilimanjaro na Tanga kwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

(ii) Kuanzisha kituo kikubwa cha kuwapatia waathirika tiba kwa njia ya kazi (*occupational therapy*) ambapo mafunzo ya stadi za kazi mbalimbali yatatolewa. Kituo hiki kinajengwa katika eneo la Itega, Mkoani Dodoma.

(iii) Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, imetengeneza miongozo mbalimbali kwa ajili ya kusimamia utoaji wa huduma kwa waathirika wa dawa za kulevya kuanzia katika vituo vya afya hadi kwenye huduma za kijamii zinazotolewa na asasi mbalimbali za kiraia.

(iv) Kutoa elimu kwa njia ya redio na luninga ambapo viongozi wa ngazi tofauti wa mamlaka wamekuwa wakitoa elimu katika vipindi mbalimbali. Vilevile elimu imekuwa ikitolewa katika shughuli za Kitaifa kama vile Mwenge, Nane Nane, maadhimisho na matamasha mbalimbali.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Faida Bakar swali la yongeza.



**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini kuna kitu amekiongelea, amesema kutibu. Mimi ninavyoona kinga ni bora kuliko tiba; na kwa kuwa Serikali inawatibu vijana hawa baada ya kuathirika lakini ni bora ingewakinga wasiathirike. Je, Serikali itachukua hatua gani za haraka au madhubuti za kuwakinga vijana wake wasitumie madawa ya kulevya badala ya kuwapeleka kwenye *sober house* wakati wameshaathirika na kuwatibu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa *scanning machine* katika maeneo mbalimbali ni muhimu sana katika maeneo kama *airport*, bandarini na sehemu nyingine zozote. Hata hivyo, kuna maeneo mengine kama kule kwetu Pemba, juzi nimesafiri kuja huku *scanning machine* yake haifanyi kazi na sehemu hizi ndizo wanazopitisha vitu vyao watu hawa wabaya.

Je, Serikali itachukua hatua gani kuwanunulia mashine nyingine pale *airport* ya Pemba ama kuwatengenezea ile mashine ili kuepokana na matatizo haya ya kusafirisha madawa haya ya kulevya? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli, kinga ni bora zaidi. Katika utaratibu wa kushughulikia masuala ya dawa za kulevya, hatua ambazo Serikali imezichukua zipo katika mgawanyo wa sehemu tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza tunaiita ni *supply reduction*, ni punguzaji wa upatikanaji wa dawa za kulevya ikiwa ndiyo sehemu ya kwanza kusaidia kumfanya

kijana huyu au mtu yeyote asipate madawa ya kulevya. Ni dhahiri kabisa kwamba baada ya Mamlaka ya Dawa za Kulevya kuanza kazi yake, kuanzia Januari mpaka Desemba, 2017 ninavyozungumza hivi sasa tayari wamefanyakazi kubwa ya kuzuia upatikanaji wa madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa takribani kilo 196 za *heroin* zilikamatwa lakini takribani tani 47 za bangi zilikamatwa, tani 7 za Mirungi zilikamatwa na mashamba ya bangi hekari 542 yaliteketezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukiyafanya haya sasa, yanasaidia kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya huko mtaani. Kwa hiyo, kazi ya kwanza Serikali inayofanya ni hio ya kusaidia hio kitu inaitwa *supply reduction*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha pili tunachokifanya ni *demand reduction*, tunapunguza pia uhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ya tatu ni *harm reduction*. *Harm reduction* sasa huyu ameshatumia dawa za kulevya hatuwezi kumuacha hivyo hivyo ndiyo maana sasa tunakuja na tiba lakini vilevile kumsaidia mtu huyu aweze kurudi katika hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa ninavyozungumza mamlaka imefanya kazi yake vizuri sana, hata katika uagizaji wa *methadone* hapa nchini tumetoka katika kiwango cha kawaida cha kilo 120 mpaka kilo 300, maana yake nini? Maana yake ni kwamba dawa za kulevya sasa hivi mtaani hazipatikani, kwa hiyo, hawa waathirika wanapata tabu kubwa ndiyo maana wanakwenda kutibiwa katika vituo vyetu ambavyo tumeviweka kwa ajili ya kuwatibu waraibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali inalitambua hilo na ndiyo maana tumekuja na hio mikakati tofauti tofauti kuhakikisha kwamba dawa za kulevya hazipatikani na tunawalinda vijana wetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Ndtiye, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDTIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Napenda kuongezea kwenye swali la pili la Mheshimiwa Faida Bakar kwamba kwa mujibu wa taarifa tulizonazo kutoka *Zanzibar Airport Authority (ZAA)*, *scannerya* Pemba inafanya kazi vizuri kabisa na inafuatiliwa kila siku na kila wakati. *Scanners* zote za viwanja vyetu vya ndege tunazifuatilia mara kwa mara, ahsante sana.

## T A A R I F A

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, *scanner* ya Pemba haifanyi kazi nimesafiri juzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Faida naomba ukae. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu yote yaliyotolewa na Naibu Mawaziri kuhusu suala hili, tunatambua umuhimu mkubwa wa kuhakikisha viwanja vyetu vyote vya ndege *scanner* zinafanya kazi na hizo ndizo zinazoweza kutusaidia kudhibiti tatizo la uingizaji wa dawa za kulevya.

Kwa hiyo, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kama kuna tatizo kwenye *scannerya* Zanzibar basi tutafanya utafiti wa kina ili ndani ya Serikali tuzungumze ili *scanner* hiyo iweze kufanya kazi na tuweze kuendelea kudhibiti tatizo hilo la dawa za kulevya. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo. Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa naibu Spika, mwaka jana tumeshuhudia Serikali yetu ikijaribu kupunguza tatizo la utumiaji wa madawa ya kulevya kwa kuwataja hadharani watumiaji na wauzaji jambo lililosaidia kupunguza lakini siyo kumaliza tatizo hili.

**MBUNGE FULANI:** Subiri, subiri, *Mr & Mrs* wameingia. (*Makofi/Vigelegele*)

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee. Nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia mwaka jana Serikali yetu ikijaribu kupunguza tatizo la utumiaji wa madawa ya kulevya kwa kuwataja hadharani watumiaji na wauzaji lakini jambo hili halikumaliza tatizo bali ilipunguza tu, suala hili bado lipo tena kwa wingi zaidi na wanaoathirika ni vijana wa Kitanzania ambao ni nguvu kazi ya nchi. Je, ni lini sasa Serikali itaona umuhimu wa kujenga *rehab* zitakazotambulika ili kumaliza janga hili? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani umelisikia swali ambalo limepigwiwa makofi mengi sana humu Bungeni siku ya leo.

**WABUNGE FULANI:** Ahaaa. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Halima Bulembo kwa namna ambavyo anawapigania vijana wa Taifa letu la Tanzania, lakini amekuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa naibu Spika, ni kweli tunafahamu kwamba moja kati ya njia ya kuwarudisha waathirika wa

dawa za kulevya katika hali yao ya kawaida ni pamoja na kuwa na *sober houses* nyingi na *rehabilitation centers* ambazo zitawasaidia kuwarudisha kurudi katika hali yake ya kawaida. Ndiyo maana katika majibu yangu ya msingi nimesema, moja kati ya mkakati ambao tunao ni uanzishwaji wa tiba ambao inaitwa *occupational therapy* ambao lengo lake kubwa ni kumsaidia muathirika huyu wa dawa za kulevya kurudi katika hali yake ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utaratibu huo, waathirika wote wa dawa za kulevya ambao watapelekwa katika vituo vyetu mbalimbali watafundishwa stadi mbalimbali za kazi ili baadaye akirudi asirejee katika matumizi ya dawa za kulevya. Katika mpango wetu huo, Serikali tunaanza utoaji wa tiba hiyo katika kituo ambacho kinajengwa hapa Dodoma katika eneo la Itega. Hali kadhalika tunafanya kazi pia na taasisi na wadau mbalimbali katika kuhakikisha kwamba tunawasaidia vijana wetu wa Kitanzania wasipate madhara zaidi ya matumizi ya dawa za kulevya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naona Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu yale niliyokuwa nikitaka kuuliza, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa naomba ujitambulishe jina tafadhali.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Naitwa Nuru Bafadhili.

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali la nyongeza.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vijana wengi wanaopelekwa katika *sober houses* wanalipishwa kiasi fulani

cha fedha ili waweze kujikimu kwa vyakula. Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka kuwasaidia kwa sababu kuna baadhi ya jamii hazina uwezo wa kuwasaidia watoto wale? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli *sober houses* nyingi zinamilikiwa na watu binafsi na waathirika hawa wa dawa za kulevya wamekuwa wakilipishwa. Mpango wa Serikali ni kuandaa utaratibu sasa ambapo na sisi tutatengeneza *sober houses* za kwetu ili kufanya huduma hii ipatikanike kwa urahisi na kila mmoja ambaye hana uwezo wa kumpeleka katika *sober house* za *private* aweze kupata tiba hii na imsaidie kurudi katika hali ya kawaida.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la pili, Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, Mbunge wa Uzini, sasa aulize swali lake.

Na. 2

### **Kutambua Rasmi Ajira ya Waendesha Bodaboda/Bajaji**

**MHE. SALUM MWINYI REHANI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawatambua rasmi dereva bodaboda au bajaji kuwaandikia mikataba, kuwekewa akiba na kulipiwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na waajiri wao kwani vijana hao wameshajajiri kwa zaidi ya asilimia 15 - 25 kwenye kila Wilaya au Halmashauri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, Mbunge wa Uzini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikwishakuwatambua rasmi madareva wa pikipiki (bodaboda) au bajaji tangu mwezi Aprili, 2009 ambapo pikipiki na bajaji zilikubaliwa kufanya biashara ya kusafirisha abiria kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili madareva wa pikipiki (bodaboda) au bajaji waweze kutambuliwa kwa urahisi kwa lengo la kupatiwa hduma mbalimbali zikiwemo za Hifadhi ya Jamii kutoka Serikalini na wadau wengine, Serikali imefanya juhudi kubwa ya kuwahamasisha waunde vyama vyao katika ngazi mbalimbali ambapo kwa kupitia vikundi hivyo, elimu juu ya masuala ya sheria za kazi na hifadhi ya jamii hutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kusimamia matakwa ya sheria yanayomtaka mwajiri kutoka mikataba kwa mwajiriwa wake hasa ikizingatiwa kwamba, mkataba unabeba haki za kimsingi na wajibu wa kila upande.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kutoa maagizo kwa waajiri wote nchini wanaotoa ajira kwa vijana waendesha pikipiki au bajaji kuzingatia sheria ikiwa ni pamoja na kuwa na mikataba ya kuhakikisha kuwa wanapata huduma nyingine muhimu zinazowawezesha kufanya shughuli zao kwa ufanisi na kwa kuzingatia usalama wa uhai wao na vyombo vyao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salum Rehani, swali la nyongeza.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba niulize swali moja la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado wamiliki wa vyombo hivi hawajawapa mikataba waendesha bajaji na bodaboda, matokeo yake wanakubaliana kwa maneno kwamba baada ya mwaka mmoja chombo hiki kitakuwa chako kwa kiasi fulani cha fedha lakini ikifika miezi saba au nane anamnyang'anya kile chombo na kumpa mtu mwingine.

Je, Serikali iko tayari kusimamia zoezi la kukabidhiwa mikataba waendesha pikipiki na wakamatwe waendesha pikipiki waulizwe mkataba allokupa mwajiri wako uko wapi ili kuwashinikiza wamiliki hawa kutekeleza hii sheria?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili alilolulizia Mheshimiwa Mbunge la mikataba hapa lazima tuweke vizuri na ieleweke. Mikataba aliyokuwa anazungumzia Mheshimiwa Mbunge ni mkataba wa umiliki wa pikipiki hasa baada ya kuwa kuna makubaliano kati ya mwenye chombo na yule dereva ambaye amepewa chombo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali, mkataba ambao tuna uwezo wa kuusimamia wa kwanza kabisa ni mkataba wa ajira ambao upo kwa mujibu wa sheria, kifungu cha 14 cha Sheria Na. 6 ya mwaka 2004 ambacho kimeelezea vyema namna ambavyo kila mwajiriwa anapaswa kupewa mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo kalizungumzia Mheshimiwa Mbunge, ni makubaliano ambayo yamekuwa yakifanyika kati ya waendesha vyombo na wamiliki wa vyombo ambapo utaratibu katika maeneo mengi ni kwamba yule mmiliki anampatia muda muendesha chombo akisharejesha fedha yake basi baadaye chombo kile kinabaki kuwa cha yule dereva.



Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo, nitoe tu wito wa kwamba makubaliano hayo yanaingiwa na pande mbili; mmiliki na mwendesha chombo, ikitokea namna yoyote ambayo haki ya mwendesha chombo huyu inadhulumiwa basi vyombo vya sheria vipo na tuwaombe watu hawa ambao wananyanyasika katika eneo hilo waende kulalamika na hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi ya hao ambao wanakiuka utaratibu na makubaliano ambayo wameshaingia hapo awali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Zungu, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru. Pamoja na mikataba ya bodaboda na bajaji, mikataba ni fursa za hawa vijana kufanya kazi katika miji. Sera ya MKURABITA ni mkakati wa kurasimisha biashara za wanyonge ziwe rasmi. Bodaboda na bajaji hizi baada ya mikataba hii wanapata tabu sana kufanya biashara katika miji na hasa kwenye barabara kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kutambua na kuwajali wafanyabiashara wadogo wadogo, lakini Mamlaka za Halmashauri bado zinazuia vijana hawa wasifanye biashara kwa uhakika na kuwatia hasara sana. Yako malalamiko, madalali wanaokamata bajaji na bodaboda wanaruhusu bodaboda zao tu ziingie mjini.

Je, Serikali sasa kwa kutambua sera MKURABITA wanaonaje sasa hili jambo liruhusiwe na hawa vijana wapate uhalali wa kufanya biashara katika miji yetu? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo yanatofautiana, ni *case by case* Mikoa kwa Mikoa na Wilaya kwa Wilaya, lakini Mheshimiwa Zungu ame-raise

jambo la msingi sana. Naomba Ofisi yangu ilichukue jambo hili kwa ajili ya kuliwekea utaratibu mzuri tuangalie jambo gani lifanyike katika eneo gani ili mradi tufikie muafaka kwa ajili ya vijana wetu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vyombo hivi vya usafiri bodaboda na bajaji vimekuwa vikisababisha ajali nyingi na wananchi wengi wanapoteza maisha, lakini kwa hali ilivyo sasa wamiliki wanakatia bima ndogo ambayo haim-coveryule anayeendesha na yule abiria wake. Je, Serikali haioni umuhimu wa kukaa na wamiliki wa bodaboda wakatie bima kubwa (*comprehensive*) ili kuwalinda wananchi wetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA):** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake ilikuwa ni kwamba Serikali haioni umuhimu wa kukaa ili kutengeneza mfumo mzuri ambao utasaidia na hawa ambao ni abiria lakini vilevile na hawa ambao wanaendesha vyombo hivi kuwa katika hali ya usalama. Limeletwa wazo na sisi kama Serikali tunalichukua kuona utaratibu mzuri ambao utasaidia katika kuondoa adha hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kuongezea si tu katika bima tutakwenda mbali zaidi kuwataka pia na hawa waajiri ambao wanawaajiri hawa vijana wajiunge na Mfuko wa Fidira kwa Wafanyakazi kwa maana ya *WCF* ili inapotokea tatizo lolote la muendesha bodaboda huyu basi na yeye awe katika sehemu nzuri ya kuweza kupata utaratibu ambao umewekwa na *WCF* kwa maana ya kuweza kumshughulikia

katika matatizo ambayo yanatokana na magonjwa au ulemavu kutokana na shughuli ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Gekul kwamba suala hili tunalichukua lakini tutakwenda mbali zaidi kusisitiza kwamba na hawa wanakuwa katika utaratibu huo mzuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu kwamba biashara ya bodaboda imekuwa ni sehemu kubwa sana ya ajira kwa vijana, lakini naomba tu kufahamu ukichukulia Jimbo la Nyamagana peke yake zipo bodaboda takribani 6,700 lakini vijana hao wenye uwezo wa kujijiriri ni asilimia 30% peke yake, ni nini mkakati wa Serikali kutumia walau fedha za Mfuko wa Vijana na Fedha za Uwezeshaji kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu waweze kukopeshwa na fedha hizi watumie kama sehemu ya ajira yao ili kuepusha migogoro na waajiri wao na mikataba isiyokuwa rafiki kwao?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mabula kwa kazi kubwa anayofanya kupambania vijana wa Nyamagana hasa vijana wamachinga na bodaboda amekuwa akifanya kazi hii vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali ni nini katika hili? Ni kweli tunatambua kwamba asilimia kubwa ya vijana wangependa kumiliki pikipiki hizi ziwe mali yao lakini kikubwa ambacho kinawakwamisha ni upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu, lakini vilevile na fedha kuweza kununulia vifaa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali hatua ya kwanza ambayo tumekuwa tukiifanya ni kuhamishisha vikundi vya vijana kwanza wakae pamoja, wajisajili *then* baada ya pale sisi chini Ofisi ya Waziri Mkuu tunalo Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambalo linaratibu zaidi ya mifuko 19 ambayo inatoa mikopo na inatoa na ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, rai yangu ni kuwaomba Waheshimiwa Wabunge ambao naamini kila Mbunge hapa kwake ana bodaboda ambao wana mahitaji haya kwanza kuwahamasisha kukaa katika vikundi, wajisajili na baadae tutawasaidia kuwaunganisha na mifuko mbalimbali na taasisi za kifedha ili waweze kupata mikopo ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko programu nyingi ambazo zinafanyika sasa hivi ambapo yule mwendesha bodaboda ana-*deposit* kiasi kidogo tu katika taasisi ya fedha na anakabidhiwa chombo chake na anakuwa anafanya kazi kurudisha taratibu taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote, najua ni kilio cha Wabunge wengi hakikisheni kwamba mnahamasisha uundaji wa vyama vya bodaboda na baadaye Ofisi ya Waziri Mkuu, sisi tutafanya kazi ya kuwasaidia kuratibu kwa maana mifuko gani inaweza kusaidia kuwezesha makundi haya.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo. Sasa tunaelekea Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa *Engineer* Edwin Amandus Ngonyani, Mbunge wa Namtumbo, sasa aulize swali lake.

Na. 3

## Hitaji la Hospitali ya Wilaya na Vituo vya Afya Namtumbo

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI** aliuliza:-

Wilaya ya Namtumbo haina huduma stahiki za Hospitali ya Wilaya wala Vituo vya Afya licha ya kuwepo kwa Sera ya kila Wilaya iwe na Hospitali ya Wilaya na kila Kata iwe na Kituo cha Afya.

(a)Je, sera hiyo kwa Wilaya ya Namtumbo itatekelezwa lini?

(b) Makadirio yaliyofanywa na *TBA* kwa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo ni shilingi bilioni19. Je, Serikali ipo tayari kutenga na kutoa kiasi hicho katika bajeti ya mwaka 2018/2019?

(c)Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa vitendea kazi na wataalam katika Vituo vya Afya vitano vilivyopo Namtumbo ili viweze kutoa huduma bora za afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Amandus Ngonyani, Mbunge wa Namtumbo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo ulianza rasmi mwaka 2010 na unatekelezwa kwa awamu tofauti ambapo mpaka sasa unaendelea. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 600 kimeshatumika kwa ajili ya kujenga majengo ya utawala,

jengo la wagonjwa wa nje yaani *OPD*, chumba cha kujifungulia yaani *labour room*, kichomea taka (*incinerator*), msingi na jamvi kwa chumba cha akina mama wajawazito (*maternity ward*) pamoja na mfumo wa maji safi na taka (*water and sewage system*). Kwa mwaka 2017/2018, Halmashauri imepokea shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuendeleza na kumaliza jengo la wodi ya akina mama wajawazito.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo imetenga kiasi cha shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo la upasuaji ili kuimarisha huduma za upasuaji katika hospitali hiyo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Namtumbo ina jumla ya vituo vya afya saba ambapo vitano vinamilikiwa na Serikali na viwili vinamilikiwa na mashirika ya dini. Vituo vya Afya vya Serikali ni Namtumbo, Msindo, Mputa, Mkongo na Lusewa. Vituo vya Afya vya mashirika ya dini ni Namabengo na Hanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya upasuaji wa dharura kwa akinamama wajawazito inafanyika katika Kituo cha Afya Hanga. Katika Kituo cha Afya Lusewa, jengo la upasuaji lipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji na vifaa vya upasuaji vipo katika mchakato wa kununuliwa lakini kuna tatizo la maji ambalo pia linashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Namtumbo kimepokea jumla ya shilingi milioni 400 tarehe 21 Desemba, 2017 kwa ajili ya ujenzi, ukarabati wa majengo ya upasuaji, wodi ya wazazi, maabara na chumba cha kuhifadhia maiti ambayo kazi yake inaendelea katika hatua za ukamilishaji na inategemea kukamilika tarehe 30 Aprili, 2018. Aidha, Serikali imeagiza vifaa vya chumba cha upasuaji kwa ajili ya kutoa huduma ya upasuaji kwa akina mama wajawazito (*CeMOC*) kwa Vituo vya Afya vya Msindo na Mputa ili kuondoa tatizo la vifo vitokanavyo na uzazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Edwin Ngonyani, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijauliza swali la nyongeza, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru sana wewe kwa ushiriki wako mkubwa kutafuta fedha za kujenga Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo kupitia *Selous Marathon* na hivi karibuni tutakuwa na chakula cha jioni kule Dar es Salaam, nakushukuru sana. Wananchi wa Namtumbo wataenzi sana kazi hiyo unayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, hivi Serikali hususani Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na TAMISEMI haioni umuhimu wa kuongeza bajeti ya kuendeleza ujenzi wa jengo la upasuaji kutoka milioni 100 zilizotajwa kwa mwaka ujao wa fedha hadi walau bilioni moja ili kweli ujenzi ufanyike?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa kuwa aliyekuwa Naibu Waziri wa Afya Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla alishafika Lusewa, Makao Makuu ya Mji Mdogo wa Sasawala na kujionea umbali ulivyo kutoka pale Lusewa hadi maeneo ambayo yanaweza yakapatikana huduma za upasuaji na hivyo akajionea kabisa hatari ambayo akina mama wajawazito wanaipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi Waziri wa TAMISEMI atatusaidiaje kuteleleza ahadi ambayo Naibu Waziri huyo aliitoa ya kuhakikisha Kituo hiki cha Afya cha Lusewa kinakamilika na kuanza kutoa huduma ndani ya mwezi mmoja wakati akijua kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo haina fedha kabisa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, nadhani umesikia, hapo mahali inapojengwa hospitali hiyo

mimi mwenyewe nimefika pale, hizi habari zilizoandikwa hapa kidogo..., Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI majibu tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Ngonyani kwa kazi kubwa anayofanya ya kuwalilia wananchi wake. Bahati nzuri mimi nimeweza kufika kule Namtumbo na Naibu Waziri wakati huo sasa hivi Waziri wa Maliasili, ni kweli changamoto ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwa ujumla wake na ndiyo maana kutokana na changamoto ya eneo hili ukiachia kile Kituo cha Afya cha Namtumbo tulichopeleka takribani shilingi milioni 400 mwezi Desemba na kazi tume-*target* mpaka tarehe 30 Aprili, zote ziwe zimekamili lakini tumeanza juhudi tena kubwa zingine kuhakikisha tunaongeza vituo vya upasuaji katika Kituo cha Afya cha Msindo na Mkongo ambapo tunaenda kuweka *theater* maalum kwa ajili ya upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tumesikia kilio chake, tutafanya kila liwezekanalo na timu yangu hapa chini ya Naibu Mawaziri wangu kuhakikisha kwamba mambo haya yanaenda kwa kasi na ndiyo maana kutokana na jiografia ya Wilaya ile jinsi ilivyo leo hii tuna zoezi tena la vituo vya afya viwili. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, inavyoonekana hili swali la afya linawagusa wengi. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI hebu angalia kidogo Wabunge waliosimama, wote hawa wana maswali ya nyongeza. Mheshimiwa Ally Ungando, Mwenyekiti wa Wandengereko, swali la nyongeza. (*Kicheko*)



**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza awali ya yote sina budi kushukuru kwamba hali ya ulinzi Kibiti inazidi kuimarika. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kumshukuru Rais wetu, kipenzi chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Kibiti sasa kinazidiwa, je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha ili kuwa Hospitali ya Wilaya ya Kibiti? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu, Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba hospitali inazidiwa na tafsiri yake nini ambacho kinatakiwa kufanyika? Ni kwamba tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba tunajenga vituo vya afya vingi ili Hospitali ya Wilaya hiyo iwe na sehemu ya kupumulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu Mheshimiwa Mbunge awahimize wananchi wake waonyeshe nia ya kuanza ujenzi na Serikali itapeleka mkono pale ambapo tayari wananchi washaanza ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi napenda niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini na Halmashauri ya Mji ya Bunda Mjini wanataka Hospitali ya Manyamanyama iwe Hospitali ya Wilaya na tayari

vikao vya Halmashauri vilishakaa. Tatizo hawana jengo la *mortuary* na tayari kupitia wadau wameshaanza ujenzi. Je, Serikali haioni kwamba inapaswa kuisaidia Halmashauri ya Mji wa Bunda na hasa ukizingatia Halmashauri ile ni changa kumaliza jengo lile ili sasa ile dhamira ya Hospitali ya Manyamanyama kuwa hospitali ya Wilaya ifanikiwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata manufaa na faida ya kwenda kutembelea Halmashauri ya Bunda nikiwa na ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa bahati mbaya Mheshimiwa Mbunge hakuwepo, angekuwepo tungeenda Manyamanyama tukapata fursa ya kujua nini hasa ambacho kinatakiwa kifanywe ili tuweze kushirikiana. Naomba kwa wakati mwingine tuungane tuone namna nzuri ya kuweza kusaidia ili wananchi waweze kupata huduma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omary Mgumba, swali la nyongeza.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkoa wa Morogoro wenye Wilaya saba na Halmashauri tisa ina Hospitali za Wilaya mbili tu ambazo ni Ulanga na Kilosa. Kwa kuwa katika bajeti ya mwaka huu, Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika Wilaya ya Morogoro hususani katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini katika Kata ya Mvuha.

Je, ni lini Serikali italeta hizi shilingi milioni 500 ili tuanze ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika Halmashauri ya Mvuhu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri, napenda kujibu swali hili la Mheshimiwa Omary Mgumba, ni kweli na mimi nilipata fursa ya kufika Mvuhu nikiwa na Mbunge mwenyewe jioografia na hali ya pale tunatakiwa tufanye kila liwezekanalo kuhakikisha tunaimarisha huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine wote ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba tunaboresha sekta ya afya ndiyo maana leo hii tunaboresha vituo vya afya 212 kwa awamu ya kwanza kihistoria.

Mheshimiwa Mgumba naomba nikuambie, nilifika pale na tumebaini changamoto na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi itafanya kila liwezekanalo kuwasaidia wananchi wa Morogoro Vijijini na wananchi wengine katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu moja kubwa ni kwamba tunafanya ujenzi wa vituo vya afya 212 *then* vituo vya afya vingine 70 vipya vitakuja, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kusimamia matumizi mazuri ya fedha, lengo kubwa ni kwamba ikifika tarehe 30 Aprili, tuwe tume-*launch* vituo vya afya visivyopungua 212 katika historia ya nchi yetu hii.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda sasa aulize swali lake.

Na. 4

## Uhaba wa Watumishi Sekta ya Afya Wilaya ya Geita

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA** aliuliza:-

Tatizo la uhaba wa watumishi katika sekta ya afya kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Geita ni kubwa sana.

Je, Serikali ina mkakati gani wa dharura wa kuliiondoa tatizo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu wali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Geita ina mahitaji ya watumishi wa sekta ya afya 465 ambapo waliopo ni 235 na upungufu ni 240. Upungufu huu umetokana na sababu mbalimbali ikiwemo uhamisho, vifo, kustaafu pamoja na zoezi la Kiserikali la kuondoa watumishi hewa na wale waliokuwa na vyeti *fake*. Hata hivyo, baada ya kukamilisha mazoezi hayo, Serikali imeanza kutoa vibali vya kuajiri kada mbalimbali ikiwemo kada ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mgao wa watumishi wa nchi nzima mwaka 2017, Halmashauri ya Wilaya ya Geita ilipata jumla ya watumishi 22 kati yao ni madaktari wawili. Watumishi hao wote wameripoti kwenye vitu na wanaendelea na kazi. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri ya Wilaya ya Geita imetenga katika bajeti na kuomba kibali cha kuajiri watumishi 121 katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha Halmashauri kutenga bajeti kwa ajili ya kuajiri wataalam zaidi ili kutatua changamoto ya uchache wa watumishi katika wilaya hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, swali la nyongeza.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kutokana na jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri inaonesha kabisa kuna upungufu mkubwa wa watumishi 240. Katika mwaka 2017 wameajiri watu 22 vilevile mwaka ujao wanapanga kuajiri watu 121, hii inaonesha ni mkakati wa kawaida tu na kwa sababu hiyo hawajaweza kukidhi kile ambacho mimi nilikuwa nahitaji kujua. Mimi ninachotaka kujua, ni lini sasa Serikali itakuwa na mkakati wa dharura wa kuhakikisha kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Geita inapata watumishi wa kutosha ili waweze kuwapatia wananchi huduma inayostahiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita hasa katika Jimbo la Busanda kuna baadhi ya vituo vya afya ambavyo kwa kweli vina upungufu mkubwa sana hasa katika Kituo cha Afya Katoro ambapo kuna idadi kubwa ya watu vilevile kituo hicho kinahudumia pia na Kata zingine jirani kama Rwamgasa, Busanda pamoja na Kasemye. Kitu hiki kina upungufu mkubwa sana wa wataalam kiasi kwamba inasababisha hata wakati mwingine watu kupoteza maisha yao. Ni lini sasa Serikali itahakikisha inapeleka watumishi kwa dharura katika kituo hiki cha afya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza anauliza mkakati wa dharura, ni

ukweli usiopingika kama tulivyokiri kwenye jibu letu kwamba upo upungufu mkubwa sana na namna pekee ni kuweza kuajiri na suala la kuajiri ni pamoja na bajeti inaporuhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi tukubaliane kwamba kwa kuanzia na hao ambao tumewataja 121 si haba na kwa sababu katika majibu yangu kwenye swali la msingi nimemueleza sababu zilizosababisha upungufu huu mkubwa, siyo rahisi kwamba kwa mara moja tutaweza kuziba pengo hili kwa sababu suala lenyewe lina *budget implication*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Katoro pale idadi ya watu ni kubwa na iko haja ya kuhakikisha kwamba pamoja na hospitali iliyopo vijengwe na vituo vingine vya afya ili kuweza kuongeza maeneo ya afya kuweza kutibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kwa kupitia Halmashauri yake wana uwezo wa kuweza kufanya *allocation* ndani kutazama maeneo yapi ambayo *staff* wako wengi ili ndani kwa ndani kwanza kupunguza wakati wanasubiri ajira kutoka Serikali kuu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba vituo vya afya na zahanati tunavihitaji sana na Serikali inajitahidi sana katika kusaidiana na wananchi kuvijenga vituo hivi na zahanati hizo. Je, si itakuwa ni kazi bure kama tutakuwa na vituo vya afya na zahanati ambazo hazina watumishi ambao watawapa huduma Watanzania? Naomba Serikali ione hilo kwa sababu huduma ya afya ni ya msingi sana watu wetu wasiendelee kuteseka. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa, lakini nataka kutoa majibu ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunahakiki vyeti, watumishi wengi sana imebidi waachishwe kazi na moja kati ya idara ambayo imeathirika sana ni afya. Tumeambiwa katika baadhi ya maeneo hata zahanati zimelazimika kufungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ilikwishatoa kibali cha ajira watu 50,000. Wizara yangu katika wale 50,000 kipaumbele namba moja ni afya na nataka nisema kama kuna Halmashauri yoyote ambayo huduma zimesimama kwa sababu watu wameondolewa na hawajapata watu mbadala waandike moja kwa moja kwangu watapatikana mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala alilouliza Mheshimiwa Mary Nagu, nataka niwaambie Watanzania waondoe mashaka. Tuendeleo sisi wanasiasa, viongozi kuhimiza ujenzi wa vituo vya afya na zahanati pale ambapo inakaribia kukamilika au wakati inajengwa Wizara yangu ikipata taarifa itafanya maandalizi wapatikane watumishi kabla ujenzi haujakamilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya, swali la nyongeza.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Halmshauri ya Kaliua ina upungufu wa watumishi kwa asilimia 76, waliopo ni asilimia 24 tu. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kuna mkakati gani wa dharura kuhakikisha kwamba angalau kwa Kaliua kabla hata ya kuandika barua maana nasema hapa wanapatiwa watumishi wa afya ili akina mama waache kuteseka kwa kukosa huduma? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa nadhani hilo jibu lake ni fupi kama alivyozungumza Mheshimiwa pale. Barua inabidi iandikwe ili watumishi wapelekwe. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):**Mheshimiwa Naibu Spika, umenisaidia kwa sababu majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri wa Nchi na Mheshimiwa Sakaya yuko hapa, sidhani kama itakuchukua muda mrefu kuandika barua kuainisha huo upungufu ili hili jambo liweze kufanyiwa kazi kwa mara moja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nchambi, swali la nyongeza.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, *wabheja* sana.

Kwa kuwa Jimbo la Kishapu lenye watu shapu na Mbunge shapu, ni moja ya Majimbo ama Jimbo lililotekeleza kwa kiwango cha juu sana mpango wa huduma za afya. Tunayo hospitali ya kisasa kabisa katika Wilaya yetu ya Kishapu, tuna vituo vinne vya afya vya kisasa kabisa ambavyo vimekamilika na vinatoa huduma bora katika Jimbo la Kishapu, lakini katika vijiji 118, takribani asilimia 50 mpango wa zahanati katika Jimbo la Kishapu unaendelea vizuri na miongoni mwa vituo hivyo vya zahanati vinatoa huduma bora.



Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu je, ndugu yangu, wajina Mheshimiwa Suleiman Jafo na dada yangu Mheshimiwa Ummy, kutokana na malumbano ama tatizo kubwa la mpango wa afya ambalo ni dhahiri limeelezeka na wewe umekiri kuwa watu wengi wanahitaji kuuliza maswali katika jambo hili la afya na kwa kuwa Kishapu tumekwishajitahidi tumepiga hatua...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nchambi, naomba uulize swali kwa sababu swali lako ni la nyongeza.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Kwa kuwa Kishapu tumepiga hatua kubwa, je, Wizara ya Afya na Ofisi ya TAMISEMI kwa maana ya Wizara hawaoni sasa watoe kipaumbele kwa Jimbo la Kishapu ili kuiweka kuwa ni ajenda maalum na kipaumbele cha kumaliza tatizo hili ili Kishapu iwe mfano katika Wilaya zote nchini kwa kumaliza kabisa tatizo hili kwa kutuongeza michango?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Nchambi kwa kazi kubwa ya ujenzi wa vituo vya afya na zahanati na shughuli kubwa wanayofanya ya uhamasishaji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mbunge kwamba tutamuunga mkono na ajenda ya kwanza ni kwamba Ofisi yangu itafanya utaratibu wa ziara maalum kama ya kiheshima kwenda kule Kishapu ku-*recognize* juhudi kubwa inayofanywa kule. Baadaye tutaangalia *way forward* tunafanyaje kwa pamoja kwa lengo kubwa la kuwasaidia wananchi wa Kishapu kwa juhudi hiyo waliyoifanya.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea. Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 5

**Walimu Kuhama Vituo vya Kazi kwa Hiari**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaondoa vikwazo kandamizi kwa walimu wanaotaka kuhama vituo vyao vya kazi kwa hiari yao kutokana na sababu mbalimbali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna vikwazo kandamizi kwa walimu wanaotaka kuhama vituo vyao vya kazi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kufuata wenza wao au ugonjwa. Hata hivyo, katika kuhamisha mwalimu, Serikali inazingatia ikama ili kutoathiri taaluma kwa kuhakikisha wanafunzi wanaendelea kufundishwa masomo yote kwa mujibu wa mitaala ya elimu iliyoidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitaji hilo ndiyo husababisha katika baadhi ya maeneo walimu kusubiri apatikane mwalimu mbadala kwanza kabla ya kutolewa kibali cha uhamisho ili wanafunzi wasikose haki yao ya kusoma masomo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba uhamisho wa mtumishi wa umma ni haki yake endapo atazingatia utaratibu uliowekwa. Ndiyo maana kuanzia Julai, 2017 hadi sasa Serikali imetoa vibali vya uhamisho kwa walimu 2,755 nchi nzima. Aidha, taratibu za kutoa vibali vya uhamisho kwa walimu wengine walioomba uhamisho zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwaelekeza walimu nchi nzima na watumishi wengine wote kuzingatia utaratibu na waache kutumia viongozi mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kuwaomba uhamisho. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hili angalizo la hapa mwisho hapa, Mheshimiwa Rehema Migilla swali la nyongeza. *(Kicheko)*

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mzuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna tatizo limejitokeza, kuna Waraka unasema walimu wa *arts* ambao wamezidi katika shule za sekondari wanahamishiwa shule za msingi. Huu uhamisho unakuwaje ilhali Rais wetu alisema walimu wasihamishwe mpaka pale fungu lao litakapopatikana.

Je, hao walimu wameshaandaliwa mafao yao ya uhamisho ili waende kwenye vituo vyao vipya huku tayari Wizara imeshasema mpaka itakapofikia tarehe 15 Februari walimu hawa wawe wamefika vituoni kwao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, napenda kujua, huu uhamisho wa kuwatoa walimu wa *arts* kutoka sekondari kuwapeleka *primary* unaweza kuathiri ufundishaji wa wanafunzi wa huko *primary*. Je, Serikali imeandaa *induction course* kwa ajili ya walimu hawa ili waweze ku-*coup* na ufundishaji wa walimu wa *primary*? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kwa wale wanaohusika ambao wamepata Waraka Rasmi wakiusoma vizuri watagundua kwamba maelekezo yaliyomo katika Waraka ule ni kwamba uhamisho unafanyika kutoka kwenye shule ya sekondari kwenda kwenye shule ya msingi ambayo iko karibu na eneo hilo, siyo kumtoa kwenye Wilaya moja kumpeleka Wilaya nyingine. Uhamisho ule ni wa ndani ya kata kwa hiyo hauna gharama za uhamisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ule uhamisho kutoka shule za sekondari kwenda *primary* umezingatia kwanza kipaumbele kwa wale walimu ambao walijiendeleza, zamani walikuwa walimu wa shule ya msingi wakajiendeleza wakapata diploma na *degree* hatimaye wakahamishiwa katika shule za sekondari.

Kwa hiyo, kuwarejesha kwenye shule za msingi ambazo wana uzoefu nazo hakuhitaji *induction course* ya aina yoyote. Kwa hiyo, hicho ndiyo kipaumbele ambacho kimewekwa na kimezingatia walimu wa diploma na walimu wa *degree* ya kwanza. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na swali la Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Ukonga, sasa aulize swali lake.

Na. 6

### **Serikali Kujenga Madaraja ya Mongolandege na Mto Nyebulu – Jimbo la Ukonga**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Katika Mtaa wa Mongolandege, Kata ya Ukonga, kuna daraja la Mongolandege ambalo huunganisha Jimbo

la Ukonga na Jimbo la Segerea. Aidha, daraja la Mto Nyebulu huunganisha Kata ya Buyuni na Kata ya Chanika Magengeni.

Je, ni lini Serikali itajenga madaraja hayo muhimu ili kurahisisha huduma za kijamii katika maeneo yaliyotajwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**AIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja la Mongolandege linatakiwa kujengwa katika Bonde la Mto Mzinga ambalo awali palijengwa makalavati kwa nguvu za wananchi. Kalavati hizo zilishindwa kufanya kazi kwa ufanisi baada ya mkondo wa mto kupanuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mwaka 2012, Manispaa ya Ilala ilijenga *box culvert* ili kuwezesha eneo hilo kupitika. Hata hivyo, mvua zilizonyesha kwa wingi katika kipindi hicho zilileta madhara makubwa ambapo bonde hilo lilitanuka na kalavati hiyo kusombwa na maji na kusababisha kukosekana mawasiliano katika eneo hilo. Daraja la Nyebulu linatakiwa kujengwa katika Mto Vikorongo na litakuwa na wastani wa upana wa mita 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala itatenga fedha katika mpango wa matengenezo ya barabara na madaraja kwa mwaka wa fedha 2018/2019 za kufanyia usanifu wa kina kwa ajili ya madaraja yote mawili. Aidha, baada ya usanifu huo kukamilika, gharama halisi za ujenzi wa madaraja hayo zitafahamika na kutengwa kwenye bajeti.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza nifanye marekebisho kidogo kwenye majibu, hili Daraja la Mongolandege lipo kwenye Mto Msimbazi sio Mto Mzinga, lakini vilevile kwa majibu haya, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa sababu Serikali inakiri kwamba mvua ilinyesha ikaleta madhara makubwa na Daraja la Mongolandege na Mto Nyebulu unatenga maeneo mawili tofauti kwenye huduma za jamii yaani upande mmoja ndiyo kuna shule ya sekondari, msingi, afya na huduma zote za kijamii na upande mwingine wananchi wanakaa pale. Katika hali hiyo mvua ikinyesha huwa ni kisiwa, wanafunzi hawaendi shule mpaka mvua iishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua ni kwa nini Serikali isijitahidi mwaka huu wa fedha ifanye usanifu na fedha itengwe kwa ajili ya kazi hii? Maana kwenye majibu yake anasema wataangalia na baadaye bajeti itengwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa sababu eneo hili ni muhimu na wananchi wanapata shida, tunaweza kupata huduma ya dharura ya daraja la muda katika maeneo yote mawili ili huduma ziendelee hasa wakati wa mvua tunapoelekea mwezi Aprili?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, uwezekano wa kuweza kutenga fedha kipindi hiki ambacho bajeti tayari imeshapitishwa na Bunge lako Tukufu jambo hili litakuwa na ukakasi mkubwa sana. Tutakubaliana na Mheshimiwa Waitara kwamba ili daraja hili liweze kujengwa kwa kina lazima usanifu ufanyike ili isije ikatokea kama yale yaliyotokea mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Mbunge avute subira na leo nilikuwa nafanya mawasiliano na *TARURA*, kwa kuanzia kwa ajili ya usanifu itatengwa jumla ya shilingi milioni 100 na ujenzi kwa ajili ya kuanza, tutatenga jumla ya shilingi milioni 300. Kwa hiyo, asipate shida, naomba nimhakikishie kwamba jambo hili liko kwenye mikono salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya suala la daraja la dharura. Ni wazo jema, ni vizuri tukajua wapi tunaweza tukalipata daraja la muda, lakini baada ya kwenda *site* kutazama uhalisia wa jambo lenyewe likoje. Kwa sababu huwezi ukasema daraja la muda linafananaje bila kwenda *site* kujua uhalisia ukoje. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mbunge wa Kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa ulize swali lake. (*Makofi*)

Na. 7

### **Matumizi ya Sarafu za Zamani**

**MHE. SALMA R. KIKWETE** aliuliza:-

Kwa kuwa watoto wengi hasa waliozaliwa kuanzia miaka ya 1990 na kuendelea hawazijui sarafu za senti tano, kumi, 20, 50 na shilingi moja.

(a) Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kurudisha sarafu hizo kwenye mzunguko wa matumizi kwa mfano kilogramu moja ya mchele kuuzwa shilingi 1,892.50 au shilingi 1,895.75 badala ya shilingi 1,900?

(b) Kwa kuwa mada ya shilingi na senti inafundishwa katika shule zetu hasa za msingi, je, ni lini jambo hili litatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu ya Tanzania imepewa kisheria jukumu la kuzalisha fedha za noti na sarafu kulingana na mahitaji na mazingira ya kiuchumi yaliyopo. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1966, Benki Kuu imezalisha matoleo ya noti na sarafu yenye thamani mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya soko. Mambo muhimu yanayozingatiwa wakati wa kuondoa na kuingiza katika soko noti na sarafu ya thamani ndogo na kubwa ni mfumuko wa bei wa bidhaa za huduma, kulinda thamani ya shilingi na wepesi wa sarafu kubebeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuondoa na kuingiza katika soko sarafu zenye thamani ya juu ni moja ya mikakati na juhudi ya Benki Kuu katika kulinda na kuipa shilingi hadhi ya wepesi wa ubebaji. Sarafu za shilingi zenye thamani ndogo zikiwemo senti tano, kumi, 20, na 50 pamoja na shilingi moja, tano, kumi na 20 kwa uhalisia ubebaji wake ni mgumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa hatuna sera ya kupanga bei ya bidhaa na huduma kwa sasa, ni vigumu kurejesha sarafu hizi katika mzunguko wa fedha kwa njia anayopendekeza Mheshimiwa Mbunge.

Tatu, sarafu ndogo ya fedha itarejea kwa urahisi katika mzunguko ikiwa teknolojia ya kufanya miamala ya fedha kwa



njia ya mitandao itasambaa kote nchini na jamii itakuwa tayari kufanya miamala hiyo kwa njia ya mitandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mada ya shilingi na senti inafundishwa mashuleni ili kuwapa wanafunzi maarifa ya kihesabu kama vile kuhesabu, kujumlisha, kutoa, kugawanya, kuzidisha, kulinganisha na kutafuta uwiano wa thamani mbalimbali ya fedha. Sambamba na maarifa ya mada ya senti na shilingi yanatolewa mashuleni, kigezo kikubwa cha kurejesha sarafu ndogo katika mzunguko wa fedha ni kuimarika kwa thamani ya shilingi au utayari wa wananchi kubeba mzigo mkubwa wa sarafu kwa ajili ya kununua bidhaa na huduma ndogo ndogo. Hata hivyo, sarafu zote zilizowahi kutolewa na Benki Kuu tangu mwaka 1966 bado ni halali kwa matumizi halali ya fedha hapa nchini za zinatumika kwenye miamala isiyu ya fedha taslimu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeamua kuuliza swali hili kwa sababu ya msingi, kwanza, naomba nieleze, mimi ni Mwalimu kitaaluma na mada hii ya shilingi na senti inafundishwa katika shule zetu za msingi.

Kwa kuwa inafundishwa katika shule zetu za msingi, zana ni sehemu muhimu sana katika ufundishaji kwa mwalimu na ujifunzaji kwa mwanafunzi. Hii hupelekea kufanya somo lieleweke kwa ufasaha na kwa urahisi zaidi badala ya kutumia maneno mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuondoa hizi senti, ninaamini kwamba mtoto huyu wa Kitanzania ambaye hajui hizi senti ni kumwekea wakati mgumu sana na siyo kwa mwanafunzi tu bali hata kwa mwalimu.

Je, Serikali haioni kwamba mtoto huyu ananyimwa haki yake ya msingi ya kuzijua hizi senti? Hilo ni swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, umesema kuondoa na kuweka sarafu zenye thamani kubwa kunaimarisha mfumuko wa bei, lakini naomba mtambue kwamba hakuna bilioni moja isiyoanzia na senti tano. Shilingi bilioni moja ni lazima ianzie na senti tano. Hata bajeti zinapokuja tunaambiwa kwamba bajeti hii ni ya Shilingi bilioni moja na senti kadhaa. Sasa tunapoondoa tunaweka uhalisia gani wa senti yetu hiyo ambayo ni senti tano? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu kwa maswali hayo mawili.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua fika kwamba mtoto huyu wa Kitanzania anatakiwa kufundishwa na ndiyo maana mada hizi zipo katika shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la msingi namba (b) nimesema kwamba, fedha hii bado ni halali kwa matumizi halali ndani ya nchi yetu na Serikali kupitia Benki Kuu haijaziiondoa fedha hizi sokoni, bado fedha hizi zipo na zinapohitajika zinapatikana kwa matumizi husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu, sasa aulize swali lake.

Na. 8

### **Tozo ya Kodi za Majengo**

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Bunge lilipitisha tozo ya kodi ya majengo ya shilingi 10,000 kwa nyumba ya kawaida na shilingi 50,000 kwa nyumba za ghorofa, lakini Manispaa na Halmashauri

mbalimbali nchini zimekuwa zikitoza kodi hiyo zadi ya kiasi hicho.

Je, Serikali inasema nini kuhusu hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Kavuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2017, kifungu cha 64 kimebainisha kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania itakusanya kodi ya majengo kwenye maeneo ya Majiji, Mji na Miji Midogo yote nchini, badala ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa majengo mengi hayajafanyiwa uthamini, Serikali kupitia Bunge lako Tukufu ilifanya uamuzi wa kuweka kiwango maalum cha shilingi 10,000 kwa majengo ya kawaida na shilingi 50,000 kwa majengo ya ghorofa kwa kila ghorofa. Viwango hivi ni vya mpito wakati Serikali inakamilisha zoezi la uthamini kwa majengo yote yanayostahili kulipiwa kodi ya majengo.

Aidha, majengo yote yaliyofanyiwa uthamini yanalipiwa viwango stahiki kulingana na uthamini. Kwa hiyo, mwenye nyumba yeyote akiona amepolekewa bili ya zaidi ya shilingi 10,000 kwa nyumba ya kawaida na zaidi ya shilingi 50,000 kwa nyumba ya ghorofa afahamu kwamba nyumba yake imefanyiwa uthamini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niulize maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa majibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyatoa kwa sababu mengi ni ya ukweli. Ni kweli nyumba nyingi hazijafanyiwa uthamini lakini zinatozwa hizo kodi na kodi zinazotozwa ni kwamba siyo zile tulizopitisha za shilingi 10,000 wala shilingi 50,000 ni zaidi ya shilingi 300,000 kwa nyumba ambazo hazijafanyiwa uthamini. Kwa hiyo, nashukuru kwa jibu lake ambalo amelisema ni la ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye swali langu, kwa kuwa nyumba nyingi za watu binafsi hazina *BoQ* kwa sababu wanajenga kwa kujidunduliza, leo mwananchi akipata shilingi 50,000 anasema ananunua *cement*, kesho kutwa akipata shilingi 100,000 atanunua bati, haweki kwenye kumbukumbu kwamba mwisho wa siku ametumia shilingi ngapi; na hiyo nyumba Serikali haifanyii uthamini, lakini kesho inampelekea bili ambayo wao uthamini wao aidha ni wa macho ama ni wa nini, bila kuangalia kumbukumbu za yule mtu binafsi.

Je, Serikali inasema nini na inatoa mwongozo gani thabiti kwa kutoa majawabu ili wananchi hawa ambao ni kama mimi binafsi, ambaye siweki kumbukumbu, nimejenga nyumba na leo nakuja kufanyiwa uthamini ambao ni zaidi ya pesa ambayo nakuwa nimeweka? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize swali la pili, tangu utaratibu huu umeanza, je, Halmashauri zimefaidika kwa kiasi gani? Kwa sababu sehemu ya Halmashauri sasa hawakusanyi mapato, mapato yanakusanywa na *TRA* na pia majengo mengi, maboma yako kwenye Halmashauri huko ambayo ni zahanati na mashule. Kwa mfano, kwenye Jimbo langu la Kavuu kuna maboma ya shule 69 hayana mabati mpaka kesho, Halmashauri zimefaidikaje na hizi pesa zinazokusanywa? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwenza kuhusu uthamini wa nyumba, uthamini wa nyumba unafanywa na wathamini wenye weledi mkubwa na hivyo thamani inayoelezwa ya kila nyumba imefanyiwa na wathamini hawa wenye weledi kwenye kazi yao na wenye uzoovu wa kutosha. Hivyo kila jengo linapewa thamani yake kulingana na bei ya soko la jengo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu Halmashauri zimefaidikaje? Napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba madhumuni ya kodi hii ya majengo kuhamishiwa kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikuwa ni kuleta ufanisi katika ukusanyaji, lakini pia katika matumizi ya kodi hii ya majengo. Lengo la Serikali ni jema na kwenye ufanisi tunafanya vizuri. Kuanzia Julai mpaka Desemba tumeshakusanya zaidi ya shilingi bilioni 16.7 na kulingana na sheria yetu ya fedha ilivyoletwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu, ni kwamba pesa hizi zitarejeshwa kulingana na bajeti za Halmashauri husika zilizopitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu kwa nia njema inafanya hayo yote.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu, sasa aulize swali lake.

Na. 9

### **Vigezo Vinavyotumika Katika Kutafuta Nguzo za Umeme**

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA** aliuliza:-

Kasi ya usambazaji umeme vijijini ni kubwa, lakini katika baadhi ya maeneo, miundombinu inayotumika hasa nguzo hairidhishi.

Je, Serikali inaweza kutuambia ni viwango gani (*standards*) vinavyotumika katika utafutaji wa nguzo hizo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa miradi ya usambazaji umeme vijijini, Serikali imekuwa ikihimiza na kuzingatia ubora wa vifaa vinavyotumika hasa nguzo. Nguzo zinazotumika kwenye miradi hiyo hununuliwa kutoka viwanda mbalimbali vya hapa nchini na awali baadhi zilikuwa zinatoka nje ya nchi.

Wakati wa ununuzi Shirika la Umeme nchini *TANESCO* hutoa viwango vya ubora wa nguzo kwa viwanda vinavyohitajika na vinavyozingatia viwango vya kimataifa. Kwa kuzingatia viwango hivyo, nguzo kwa ajili ya usambazaji na usafirishaji wa umeme zinatakiwa kuwa na urefu kati ya mita tisa hadi 18 na kipenyo kati ya milimita 130 hadi 308.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazalishaji hutumia dawa bora kuzalisha nguzo hizo na *TANESCO* hufanya ukaguzi kabla ya kuanza kutumika ili kujiridhisha katika ubora wake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Othman Hija, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu katika swali langu la msingi ni viwango vya miundombinu hii hasa nguzo. Wamesema kwamba *TANESCO* wana zoezi la kukagua nguzo kabla ya matumizi. Swali langu liko hapa: wanachukua hatua gani wanapogundua kwamba nguzo hizi ziko chini ya viwango? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Juma Othman Hija, kwa swali lake la nyongeza. Kama ambavyo jibu langu la msingi limesema, Shirika la *TANESCO* hufanya ukaguzi kwanza wa vifaa hivi kabla havijatumika kwenye miradi hii. Kwa hiyo, endapo inagundulika nguzo hizi hazina ubora, nguzo hukataliwa na wanaotekeleza miradi miradi hiyo huelekezwa kutimiza vigezo na hasa vile viwanda ambavyo vinatengeneza hizi nguzo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, swali la nyongeza.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Chilonwa, Vijiji vya Bwawani, Kata ya Kamanchali na Vijiji vya Mlebe, Kata ya Msamalo nguzo zilikuwa zimeshapelekwa kwa ajili ya kuweka umeme na mashimo yakachimbwa, lakini baadae nguzo hizi zikaja kuhamishwa.

Je, Serikali ina mpango gani sasa kuona umuhimu wa kuvipa vipaumbele vijiji hivi ambavyo vilikuwa vimeshapelekwa nguzo na kuondolewa ili katika awamu ya tatu visije vikawa vijiji vya mwisho tena? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Makanyaga, Mbunge wa Jimbo la Chilonwa kwa swali lake zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri kwamba ni kweli vipo baadhi ya vijiji ambavyo vilipelekwa miundombinu ya hizi nguzo, lakini baadae zikahamishwa kwa kuwa havikuwepo kwenye mpango wa utekelezaji wa kupeleka umeme vijijini *REA* Awamu ya Pili. Nimdhibitishie kwamba kwenye hii *REA* Awamu ya Tatu ambayo inaendelea kwa *round* hii ya kwanza,

vile vijiji vyote ambavyo kwa bahati mbaya, kwamba vilipelekewa nguzo halafu zikaondolewa, miradi hiyo itatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba vijiji vyote nchi nzima vitapata miundombinu ya umeme kwa kipindi hiki ambacho kinaendelea. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, sasa aulize swali lake.

Na. 10

### **Kukamilisha Mradi wa Umeme - Momba**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi ya umeme katika vijiji ambavyo havijafikiwa katika Halmashauri ya Momba?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kufikisha umeme katika vijiji vyote visivyo na umeme nchini ikiwemo vijiji vya Wilaya ya Momba ifikapo Juni, 2021. Katika Wilaya ya Momba jumla ya vijiji 27 vitapatiwa umeme kupitia mzunguko wa kwanza wa awamu ya tatu ya miradi ya kusambaza umeme vijijini. Vijiji hivyo ni pamoja na Ikana, Nakawale, Ipanga, Mpui, Mfuto, Machindo, Muungano, Samang'ombe, Tundumakati, Unyamwanga, Nello, Tukuyu, Mlimani, Majengo Mapya, Ihanda na Migombani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za mradi zinazotekelezwa na Kampuni ya *STEG International* ambazo zinahusisha ujenzi wa kilometa 60 za umeme msongo wa kilovoti 33 na kilometa 108 za njia za umeme msongo kilovoti



0.4, kufunga transfoma 54 na kuunganisha wateja 1,773. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa shilingi 6,607,000,000 na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vitakavyobakia katika mzunguko wa kwanza wa *REA III* vitapatwiwa umeme katika mzunguko wa pili wa *REA-III* iunaotarajiwa kuanza mwezi Aprili, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa David Ernest Silinde, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya kuridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali madogo mawili. Swali la kwanza, miradi ya umeme ya *REA III* imezinduliwa karibu nchi nzima katika kila Mkoa, lakini utekelezaji wake mpaka sasa hivi haupo, isipokuwa ipo katika mipango kama hivi ambavyo inaonesha. Nini ambacho kinasababisha au kimesababisha kucheleweshwa kwa miradi ya *REA III* kuanza kukamilika tofauti na iliyopo katika maandishi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili ni kwamba pamoja na majibu yake, Miradi ya *REA* tuliwekea zuwio la fedha, yaani tuli-*ring fence* fedha zake ambazo zilitakiwa zisiguswe, lakini mpaka sasa hivi miradi hii haitekelezeki kwa sababu hizi fedha hazieleweki mahali ziliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu nataka niulize je, hizi fedha ambazo tumezi-*ring fence* kwa ajili ya utekelezaji wa hii miradi, kwa nini hazitumiki kutekeleza mradi ikizingatiwa kuna fedha ambazo tunakata katika mafuta shilingi 50 kwenye kila lita ya mafuta? Kwa nini zinashindwa kutumika kwa ajili ya kumalizia hii miradi? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli miradi hii ya umeme vijijini ilizinduliwa mwezi wa Sita mwaka 2017. Naomba nimhabarishe Mheshimiwa Mbunge kwamba wakandarasi wote ambao waliteuliwa takribani 27 tulikutana nao tarehe 13 Januari, 2018 hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi una kazi mbalimbali. Kwanza, walikuwa wana-*survey* na mnakumbuka Waheshimiwa Wabunge wengi mlileta mapendekezo, maombi ya vijiji mbalimbali, kwa hiyo, lazima *survey* ifanyike.

Pili, baada ya *survey* lazima kuwe na michoro, lakini nimthibitishie kwa Mkoa wake wa Songwe na Wilaya yake ya Momba, mkandarasi wake ameshaagiza vifaa na kesho tarehe 31 Januari na tarehe 01 *TANESCO* wanaenda Mkoa wa Arusha kuangalia zile transfoma. Kwa hiyo, ni wazi kwamba miradi hii inatekelezeka, lakini zipo hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongezee kwa kusema pia, vipo vijiji ambavyo vimeshawashwa umeme *REA* hii ya *III*. Kwa hiyo, inategemea Mkandarasi na huo muda. Kwa mfano, Geita kuna vijiji vimewaka; Mwanza Halmashauri ya Bumbuli pia umeme umewaka *REA* hii ya *III*. Kwa hiyo, miradi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili alikuwa anasema kwamba, vipi kuhusu pesa zake za miradi hii ya umeme vijijini? Ni kweli nalishukuru Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Bunge hili iliwekwa tozo maalum kwenye mafuta na mfuko huo kweli umelindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niishukuru Wizara ya Fedha kwamba pesa zimekusanywa, zimewasilishwa na mpaka sasa tumeshapata shilingi bilioni 170.

Kwa hiyo, pesa kwenye miradi hii siyo tatizo. Tatizo ambalo lipo, changamoto tuliyokuwa tunaiona ni hawa wakandarasi kujipanga kwa mujibu wa wakati na ratiba wanavyozipanga. Ndiyo maana baada ya kuona hilo tatizo, tumekutana nao hapa Dodoma na tumewapa maelekezo kwamba mwisho tarehe 28 Februari, wakandarasi wote waanze kazi. Siyo kazi ya *survey*, kazi ya kuweka nguzo na miundombinu mingine ili miradi itekelezeke.

Mheshimiwa naibu Spika, nilithibitishie Bunge lako, miradi hii muda wake, hii awamu ya kwanza hii ni kipindi hiki mpaka Aprili, 2019.

Kwa hiyo, niwatoe hofu. Kwa kuwa pia tumeweka usimamizi mzuri, kila mkoa tumemtaka *engineer* mmoja asimamie, kila Wilaya kuwe na *engineer* mmoja kwa ajili ya miradi ya *REA* tu. Kwa hiyo, ninaamini, hata kasoro ambazo zilijitokeza kwa miradi ya *REA* awamu nyingine, kwa Awamu hii ya III itaenda vizuri na itakamilika kwa wakati. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hongoli, swali la nyongeza.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ina vijiji 12 tu ambavyo vimepata umeme wa *REA*, lakini vijiji 22 bado havijaingizwa kwenye mpango huu wa *REA III*. Naomba kujua ni lini sasa Serikali itaingiza hivi vijiji 22 vyote ili waweze kupata umeme wa *REA*? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Hongoli kwamba vijiji vyake 22 vilivyosalia vyote vitaingizwa kwa Awamu ya Tatu *round* ya pili ambavyo vinahusika vijiji 4,314. Kama ambavyo nimejielekeza tangu mwanzo, lengo la Serikali hii ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha vijiji vilivyosalia 7,873 vyote vinafikiwa na miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu hii tumeanza na vijiji 3,559 vinasalia vijiji 4.314. Kwa hiyo, ndani yake kuna vijiji 22,000 vya Jimbo lake la Njombe. Kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania wote, Serikali ya Awamu ya Tano inaenda kufanya mapinduzi ya nishati vijiji vyote. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaelekea kwenye Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 11

### **Mmiliki wa Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Katika Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro, ipo karakana ya kutengeneza ndege (*hangar*) ambayo ilijengwa na Serikali ya Uholanzi, lakini sasa hivi haitumiki.

(a) Je, ni lini Serikali itafufua karakana hiyo ili ndege zetu za Bombardier na nyingine ziweze kufanyiwa matengenezo hapo?

(b) Je, ni nani mmiliki wa uwanja huo wa ndege?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye Sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, karakana ya kutengeneza ndege ya *KIMAF* iliyopo Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro kwa sasa inaendeshwa na kusimamiwa na Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Karakana hiyo ilijengwa mwaka 1980 na kukabidhiwa rasmi kwa Serikali mwaka 1985 na ina uwezo wa kuhudumia ndege kubwa aina ya *B747'S* au ndege tano aina ya *B737'S* kwa wakati mmoja. *ATCL* inaendelea kuifanyia matengenezo karakana hiyo ili iweze kurudi kwenye ubora wake na kutoa huduma za matengenezo ya ndege.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (*KIA*) ni kati ya viwanja 59 vinavyomilikiwa na Serikali chini ya usimamizi wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kiwanja hiki kinaendeshwa na Kampuni ya Uendeshaji wa Viwanja vya Ndege ya Kilimanjaro (*Kilimanjaro Airports Development Company – KADCO*) ambayo inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Aidha, taratibu za kuunganisha *KADCO* na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA*) ili kuwa na taasisi moja inayosimamiwa na viwanja vya ndege nchini zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu 2018.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taska Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa ajili ya usalama wa nchi kwa kawaida viwanja vya ndege vinatakiwa viendeshwe na *Agency* za Serikali ambazo ni *TCAA* na *TAA* pamoja na Taasisi ya *Meteorological*. Taasisi hii ya *KADCO* ni kampuni, sasa swali langu kwa Mheshimiwa Waziri, Kampuni ya *KADCO* itaunganishwaje na *TAA* kama alivyoeleza kwenye majibu yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni lini ndege za *Bombardier* zitashuka Wilayani Mpanda, Mkoani Katavi maana tunazihitaji? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, katika jibu langu la msingi nimeeleza tu kwamba, *KADCO* ni Shirika la Umma ambalo linamilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. Kwa hiyo, siyo kitu cha ajabu kuunganisha *KADCO* na *TAA* kwa sababu zote zinamilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, zote ni taasisi za Serikali na zikiunganishwa tutapata uongozi wa aina moja na bodi ya aina moja ambayo itarahisisha sana menejimenti ya viwanja vya ndege kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, tuko kwenye harakati za kupanua uwanja wa ndege wa eneo hilo. Kwa hiyo, tutakapopanua uwanja wa ndege wa eneo hilo Mheshimiwa Mbunge, ndege za Bombardier zitaanza kushuka. Tuna lengo la kuhakikisha kwamba viwanja vyetu vyote vya ndege vinaongezwa ubora wake na ukubwa ili ndege zote ambazo zina ukubwa wa kutosha ziweze kutua kwa ajili ya kuhudumia Watanzania. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kati ya mambo yanayosababisha Uwanja wa Ndege wa Mpanda usifanye kazi ni kutokuwepo kwa huduma ya zimamoto. Ni lini Serikali itatusaidia kuhakikisha huduma ya zimamoto inakuwepo kwenye Uwanja huo wa Mpanda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwanza nampongeza sana wewe na Wabunge wenzako wote wa Mpanda kwa jinsi mnavyoshughulikia masuala ya huduma za usafiri wa anga kwa ajili ya mkoa wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, sasa hivi gari linalotoa huduma ya zimamoto kwenye uwanja ule limepata hitilafu na Serikali kupitia TAA tunaendelea kushughulikia kuhakikisha kwamba, uwanja ule unapata hiyo huduma ya zimamoto na hivi karibuni tumeendelea kuwasiliana na watu wa kule Mpanda ili walete makadirio yatakayoweza hiyo huduma irudi katika hali yake ya kawaida.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Venance Methuselah Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naona umetuka swali moja.

**NAIBU SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Venance. Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay Mbunge wa Mbulu Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 12

### **Kuweka Lami Barabara ya Karatu – Shinyanga**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Wilaya ya Mbulu haina barabara ya lami kutokana na kuzungukwa na Bonde la Ufa kuanzia Karatu, Mto wa Mbu, Babati – Hanang hivyo, kufanya magari makubwa kutoka Uganda, Kenya na Dar es Salaam kuzunguka umbali mkubwa ili kufika Mbulu Mjini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ahadi yake ya kuweka lami katika barabara ya Karatu – Mbulu – Hydrom

– Mkalama – Lalago Shinyanga ili kurahisisha usafiri katika njia hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Huyu ni Mbunge wa Mikoa mingi kuliko Wabunge wote humu ndani. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Karatu – Mbulu – Hydrom – Mkalama – Lalago – Kolandoto, yenye urefu wa kilometa 389 ni kiungo muhimu kwa Mikoa ya Arusha, Manyara, Mara, Shinyanga na Singida kwa kupitia Kusini mwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa barabara hii ina umuhimu mkubwa wa kiuchumi na kijamii na ni kiungo muhimu kati ya Mikoa ya Arusha, Manyara, Mara, Shinyanga na Singida. Maandalizi ya ujenzi kiwango cha lami ya barabara hii yameanza kwa hatua za awali, ambapo Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) imeingia mkataba na Mhandisi Mshauri aitwaye *HP Gauff Ingenieure GmbH & Co. KG – JBG* ya Ujerumani ili kufanya kazi ya upembuzi yakinifu ambayo inaendelea hadi sasa. Kazi hii inagharamiwa na Serikali ya Ujerumani kupitia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, baada ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika, Serikali itatafuta fedha na kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.



**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na hatua kubwa inayochukuliwa na Serikali yetu.

Je, kutokana na gharama kubwa inayotumika ya matengenezo ya kawaida katika barabara hii inayounganisha mkoa minne kwa kiwango cha changarawe na kwa kuwa katika majibu ya msingi Mheshimiwa Waziri hakueleza mkataba huu unaisha lini, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuharakisha kazi hii ya usanifu ili barabara hii ipate kutengenezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Mheshimiwa Rais aliahidi ahadi nyingi wakati wa kampeni kama sehemu ya utatuzi wa changamoto za wananchi. Katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu aliahidi kilometa tano kwa barabara ambazo zinamilikiwa na Serikali za Mitaa wakati ule. Kwa kuwa sasa barabara zile zimehamia kwa *TARURA*, je, ni nani atakayetekeleza ile ahadi ya kilometa tano katika barabara zile kwa kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa sasa haziko tena kwenye utaratibu wa kuzihudumia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia sana hii barabara muhimu ambayo inaunga mkoa mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba kwanza barabara hii pia inafuatiliwa na Waheshimiwa wa mkoa hii. Mheshimiwa Flatei Massay naye anaifuatilia sana barabara hii tumezungumza, lakini wako Wabunge wa Mkoa wa Singida, wako Wabunge wa Simiyu wanafuatilia hii barabara muhimu sana. Na sisi upande wa Serikali, ili kuharakisha ujenzi wa barabara hii, tumeanza ujenzi katika Mto Sibiti, sehemu ambayo ilikuwa ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba kwa sasa kwanza wananchi wanapita. Wakipita katika barabara hii kwa mtu ambaye anaenda Karatu tuna-save zaidi ya kilometa 400, kwa mtu anayekuja Singida tuna-save zaidi ya kilometa 200; tuna-save muda, lakini pia tuna-save gharama mbalimbali.

Mheshimiwa NAibu Spika, ili kuharakisha ujenzi wa barabara hii, Serikali imechukua hatua kuhakikisha kwamba ujenzi wa daraja utakapokamilika mwishoni mwa mwaka huu, tutakuja kwenda haraka katika ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ahadi za kilometa tano, ninajua kwamba nchi nzima ziko ahadi ambazo sisi kama Serikali tunaendelea kuzitekeleza, ikiwepo ahadi ambayo imetolewa huko Mbulu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira, tumejipanga tunaendelea kuratibu kuona kwa kiasi sasa tunapoenda nusu ya kipindi cha miaka mitano tumetekeleza ahadi ngapi ili tuweze kukamilisha ahadi hizi ambazo Mheshimiwa Rais aliahidi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Venance Methusalah Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, sasa aulize swali lake.

Mheshimiwa Flatei, umegonga sana na Naibu Waziri amekutana hapa kwamba unafuatilia. Hata Mheshimiwa Qulwi Qambalo nimemwona pale. Kwa hiyo, ninyi wote mnafuatilia kwa pamoja. Mheshimiwa Naibu Waziri, ametambua michango yenu.

Mheshimiwa Mwamoto, swali.

Na. 13

**Fedha Zinazopata Wilaya Zinazopakana na  
Hifadhi ya Taifa**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO** aliuliza:-

Je, ni kiasi gani cha fedha kinatolewa kwa Wilaya ambazo zinapakana au zilizo na Hifadhi za Taifa ikiwamo Wilaya ya Kilolo katika Hifadhi ya Udzungwa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii, kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*), inatekeleza Mpango wa Ujirani Mwema (*Support for Community Initiated Projects*) ulioanzishwa mapema miaka ya 1990. Lengo la mpango huu ni kuishirikisha jamii katika kupunguza changamoto za uhifadhi na kuwanufaisha wananchi waishio jirani na hifadhi. Utekelezaji wa Mpango wa Ujirani Mwema unahusisha vijiji katika Wilaya zinazopakana na Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa, vijiji vinaibua miradi ya maendeleo na kuchangia asilimia 30 ya gharama za miradi na shirika kuchangia asilimia 70 ya gharama hizo. Kupitia mpango huu kila mwaka *TANAPA* inatenga kati ya 5% hadi 7% ya bajeti yake kwa shughuli za miradi hiyo. Vilevile mpango huu unahusisha utoaji wa elimu ya uhifadhi na kuwashirikisha wananchi katika uhifadhi wa maliasili na mazingira kama vile upandaji wa miti na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2000/2001 hadi mwaka 2017/2018 Hifadhi ya Taifa ya Udzungwa imefanikiwa kutekeleza miradi ya ujirani mwema

katika Wilaya ya Kilolo yenye thamani ya jumla ya shilingi 435,962,656. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa Wilaya ya Kilolo inahusu uwekaji wa umeme, ujenzi wa barabara, ununuzi wa samani na ununuzi wa vifaa vya maabara vya Sekondari ya Lukosi katika Kijiji cha Mtandika ambapo jumla ya shilingi 49,460,937 zimetumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa nyumba wa awamu za walimu katika Kijiji cha Ikura umegharimu shilingi 60,000,000; ukarabati barabara ya Ilula – Udekwa, ujenzi na ununuzi wa samani Kituo cha Polisi, nyumba ya walimu, shule ya msingi katika Kijiji cha Udekwa umegharimu shilingi 227,501,719 na mpango wa matumizi bora ya ardhi na nyumba ya walimu shule ya msingi Msosa katika Kijiji cha Msosa shilingi 81,000,000 na ununuzi wa madawati kwa ajili ya Wilaya ya Kilolo umegharimu shilingi 18,000,000. Jumla ya fedha zote zilizotolewa na Shirika ni shilingi 435,962,656.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venance Mwamoto, swali la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ambayo yanatofautiana na swali langu, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimkumbushe kidogo Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Milima ya Uluguru wanakaa Waluguru, Milima ya Usambaa wanakaa Wasambaa wanaotoka Tanga na Milima ya Udzungwa wanakaa Wadzungwa na Udzungwa iko Wilaya ya Kilolo kwa asilimia 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu nililopewa hapa, inaonekana kwamba Kilolo wanapewa kama hisani, siyo haki yao. Kwa hiyo, ninachooomba kwa kuwa tayari yalikuwepo makubaliano ya kuhamisha Makao Makuu ya Udzungwa kwenye Kilolo Udekwa, lifanyike ili wananchi wale wanufaike kwamba ile Udzungwa ni ya Wadzungwa siyo ya Waluguru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa mara nyingi yamekuwa yakitokea maafa, kwa mfano vijiji vya Msosa, Ikula, Ruaha Mbuyuni, Mahenge na Mtandika wananchi wanauawa na tembo bila kulipwa fidia; na fidia ambayo wanalipwa ni fedha ndogo sana, ni pamoja na uharibufu wa mazao yao.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutunga au kuja kuleta hapa tubadlishe sheria ili wananchi hawa wawe na thamani zaidi ya wanyama ambao ndiyo wanawaua? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akifanya katika Jimbo lake. Amekuwa akifuatilia sana na amekuwa akiwatetea sana wananchi wa Jimbo la Kilolo. Kwa kweli hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba hili suala la kuhamisha Makao Makuu, tutalishughulikia. Yapo mambo mengi ya kuzingatia tunapotaka kuhamisha makao makuu na jitihada sasa hivi zinafanywa katika kuangalia miundombinu kama itawezekana kwenda kufikika katika hayo maeneo ambayo yalikuwa yamekubalika pale awali. Baada ya hilo kukamilika, basi tutalifanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu fidia ya wananchi ambao wanakuwa wameadhirika na wanyamapori hususan tembo na wanyama wengine, hili suala lipo kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa taratibu zetu. Ni kweli kabisa taratibu ambazo zipo zinabainisha ni aina gani ya kifuta machozi ambacho kinatolewa kwa wananchi wanaokuwa wameathirika na haya matatizo. Sasa namuomba Mheshimiwa Mbunge kwamba katika hao wananchi ambao amewasema, hiki kiasi japo ni kidogo,

hakilingani na thamani ya binadamu anayekuwa amepotea, lakini bado tutaendelea kutoa kwa wakati, nitaomba tuwasiliane nipate hayo majina ili niweze kuyafanyia kazi mara moja. Hilo nitalishughulikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimhakikishie kwamba tuko kwenye harakati ya kuweza kupitia upya sera yetu pamoja na sheria ili tuakikishe kwamba tunahuisha na kuweka viwango vile ambavyo vitakuwa vinatosheleza na vinasaidia katika kupunguza haya matatizo. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Mjini, sasa aulize swali lake.

Na.14

**Madai ya Msingi Watu Wanaoongoza Watalii,  
Wapagazi na Wapishi**

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL** aliuliza:-

Je, Serikali imejipanga vipi kumaliza madai ya msingi na ya muda mrefu kwa waongoza watalii, wapagazi na wapishi kutambuliwa kwa kima cha chini cha mishahara, mikataba ya kazi inayoendana na kazi zao, malipo ya posho kwa huduma wanazotoa kwa siku, sera shirikishi katika kutatua matatizo yao na utalii wa nchi kwa ujumla na malipo ya huduma za jamii kama vile afya na majanga?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII MAJIBU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, madai ya wapagazi, wapishi na waongoza watalii yameshughulikiwa na Wizara kwa kushirikiana na Vyama vya *Tanzania Association of Tour*

*Operators (TATO); Kilimanjaro Association of Tour Operation (KIATO); Tanzania Tour Guides Association (TTGA); Kilimanjaro Guides Association (KGA); Tanzania Porters Organization (TPO); Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi Ajira, Vijana na Ulemavu) na Vyama vya Wapagazi na Wapishi.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano uliofanyika Arusha tarehe 12 Desemba, 2015 Wizara na wadau walikubaliana kuhusu viwango vya chini vya ujira kwa wapagazi wapishi na waongoza watalii. Viwango vinavyopendekewa kwa siku ni shilingi sawa na dola za Marekani 10 kwa wapagazi 15; kwa wapishi na 20 kwa waongoza watalii kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika makubaliano hayo, Serikali ilisisitiza juu ya umuhimu wa kuingia mikataba ya kazi baina ya waajiri na waajiriwa. Serikali ilitoa miongozo ya mikataba ili izingatiwe kwa mujibu wa matakwa ya kila kundi na ilianza kutumika katika Sekta ya Utalii. Waajiri na wajiriwa wanatakiwa kisheria kutekeleza wajibu wao wa kusaini mikataba na kuzingatia viwango vilivyokubaliwa. Endapo makubaliano yao hayatazingatiwa, ni wajibu wa waajiriwa kutoa taarifa kwenye mamlaka husika za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kima cha chini cha mishahara na malipo ya posho kwa huduma za jamii kama vile afya na majanga, Serikali inaendelea kuhimiza kuwa waajiri wazingatie kima cha chini cha mishahara kilichotolewa na Serikali na michango inayopaswa kutolewa kwenye mifuko mbalimbali kama vile Shirika la Taifa la Hifadhi wa Jamii (NSSF), Bima ya Afya na Mfuko wa Fidha kwa Wafanyakazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, swali la nyongeza.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali kuhusu tatizo hilo, lakini bado tatizo hili ni kubwa na linaendelea. Mijadala juu ya wapagazi, waongoza watalii na wapishi imekuwa ya muda mrefu baina

ya Serikali na waajiriwa hawa, lakini utekelezaji wa makubaliano umekuwa hafifu sana.

Swali la kwanza, je, Serikali haioni kwamba kuna haja kwa sasa kwenda kuonana na waajiriwa kuongea nao ana kwa ana, kujua ni kwa kiwango gani miongozo hii ambayo wameipeleka imetekelezwa na imekuwa na tija kwa hao watu ambao ndio waathirika wa tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kumekuwa na utaratibu kwamba wanaoshughulikia matatizo ya watalii imekuwa ni kampuni ya nje na sio watu wa ndani. Ni kwa nini Serikali haioni haja ya kushirikisha kampuni za ndani kuhakikisha kwamba inasimamia suala la *porters* na waongoza watalii na inaliacha katika kampuni za nje? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunakubaliana kabisa kwamba kuna haja ya kuonana na waajiriwa ili kuweza kubaini kama kweli yale makubaliano tuliyoyafikia pale Arusha yametekelezeka. Na mimi naomba kumwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kikao hiki cha Bunge tutapanga safari ya kwenda kuonana na wale ili tuweze kuangalia utekelezaji wa hayo mambo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuhusu matatizo ya hawa wapagazi kwamba yanatatuliwa na kampuni ya nje, hili ni suala ambalo nimelisia sasa hivi, lakini nadhani tatalichukulia hatua na tutahakikisha kwamba matatizo ya Watanzania yanashughulikiwa na Watanzania wenyewe kupitia mifumo iliyowekwa na makampuni yetu yako tayari kabisa kushughulikia hili tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge, hili tatalishughulikia na kulifanyia kazi.



**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutamalizia na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, sasa aulize swali lake.

Na. 15

### **Hitaji la Matangazo ya Redio TBC - Lushoto**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, ni lini Wilaya ya Lushoto itaanza tena kupokea matangazo ya Redio ya Taifa (TBC)?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kijiografia Wilaya ya Lushoto katika Mkoa wa Tanga ni kati ya Wilaya ambazo zinazozungukwa na milima, mazingira ambayo huzuia mawimbi ya TBC FM pamoja na TBC Taifa, ambayo hurushwa kutokea mitambo ya FM iliyoko katika eneo la Mnyuzi Wilayani Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua changamoto hii, TBC imeamua sasa mtambo wa kurushia matangazo hayo ujengwe katika Wilaya ya Lushoto ili matangazo ya redio yaweze kufika kwa uhakika katika wilaya hii. Ili kufanikisha kazi hii, TBC imetenga shilingi milioni 50 toka bajeti yake ya ndani kwa ajili ya mnara utakaotumika kuweka mtambo wenye nguvu ya *watt* 500 na viunganishi vyake kwa ajili ya kupokea matangazo hayo. Mtambo huu utafungwa katika eneo la Kwemashai ambako kuna miundombinu ya kuwezesha zoezi hili kukamika kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali ambayo yanatia matumaini, nina maswali madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, wakati redio ya TBC wanatumia mawimbi ya *short wave* na *medium wave* mawasiliano yalikuwa mazuri. Je, hawaoni kwamba kuhamia kwenda *digital* inaweza ikawa ni changamoto hata kwa maeneo mengine yaliyoko pembezoni katika Taifa letu? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 18(b) tunayo haki ya kupokea na kupata taarifa, sasa anawaambia nini wakazi wa Mlalo ambao wako pembezoni mwa nchi jirani ya Kenya ambao hawapati habari za Taifa lao na je, hawaoni kwamba hii inahatarisha usalama wa Taifa? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii ya kuweza kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rashid Shangazi kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia kwa umakini kabisa matatizo ya wananchi wa Jimbo la Mlalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba baada ya kupokea majibu mazuri kabisa ya Serikali nilitegemea kwamba Mheshimiwa Shangazi atakuwa hana maswali ya nyongeza. Kwa sababu ameuliza maswali mawili, naomba nimjibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kweli kwamba kuhama kutoka kwenye mfumo wa *analogy* kwenda kwenye *digital* imepelekea kuweza kupunguza usikivu wa redio hii ya TBC. Changamoto kubwa ambayo ilikuwepo ni kwamba

mitambo mingi ambayo ilikuwa inatumika ilikuwa ni mitambo ambayo imechoka, mibovu ukizingatia kwamba mitambo hiyo ilikuwa ni ya muda mrefu sana.

Kwa hiyo, hata linapokuja suala zima la kutafuta vipuri kwa ajili ya kufanya marekeboshu ya mitambo hiyo, ilikuwa ni ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Rashid Shangazi kwamba tatizo hilo kwa sasa hivi TBC imelichukua kwa kina na inalifanyia kazi na mpaka sasa hivi katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Mwanza pamoja na Kigoma tumeanza utaratibu wa kuboresha mitambo hiyo ili kuhakikisha kwamba matangazo haya ya TBC Taifa pamoja na TBC FM yanawafikia wananchi kama ambavyo inatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali lake la pili, ametaka kujua umuhimu wa chombo hiki cha Taifa, TBC kwa maeneo ambayo ni ya mipakani. Mheshimiwa Shangazi, Serikali hii ya Awamu ya Tano inatambua kabisa kwamba wananchi wote ambao wanakaa maeneo ya mipakani wana haki ya kupata taarifa kama ambavyo wananchi wengine wanakaa katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hilo, kuna mkakati wa TBC ambao umeshaanza kufanyika katika maeneo ya mpakani, nikianza na eneo la Rombo, lakini ukienda na eneo la Namanga, Tarime pamoja na Kakonko, tayari ufungaji wa mitambo mipya ya TBC umeanza kufanyiwa kazi. Tunaamini kwamba mitambo hii itakapokamilika, kwa kiasi kikubwa sana itasaidia kumaliza tatizo hili za usikivu kwa chombo hiki cha TBC.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Shangazi aliuliza kwa upande wa Lushoto. Kama ambavyo

nimejibu kwenye jibu langu la msingi, ni kwamba tayari shilingi milioni 50 imeshatengwa kwa ajili ya kumaliza tatizo la usikivu katika Wilaya hiyo ya Lushoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kabisa Mheshimiwa Shangazi kwamba eneo hili la Kwamashai ambalo limechaguliwa kuhakikisha kwamba mtambo huu unawekwa, ni eneo ambalo limefanyiwa utafiti wa kina na imeonekana kabisa kwamba mtambo huo ukijengwa hapo, basi maeneo yale ya Lukozi, Mnazi pamoja na Lunguzi ambako imepakana kwa ukaribu kabisa na kijiji ambacho kiko kwenye nchi ya Kenya watapata matangazo ya TBC kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabuge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Nitaleta matangazo tuliyonayo siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo, kwa hivyo shughuli za Serikali Bungeni kwa sasa anayezisimamia ni Mheshimiwa Dkt. George Harrison Mwakyembe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la pili ni la wageni tuliona asubuhi hii. Wageni kundi la kwanza ni wale walioko jukwaa la Mheshimiwa Spika. Wa kwanza ni Mheshimiwa Lekule Laizer naye ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunae pia Mheshimiwa Odo Mwisho ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Ruvuma, tunaye pia Ndugu Parseko Ole Kone ambaye alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida. Karibuni sana wageni wetu. Hawa wamekuja

kushuhudia kiapo cha Waheshimiwa Wabunge watatu waliapishwa leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo wageni wengine ambao wapo asubuhi hii pamoja na sisi, kundi la kwanza ni wageni 50 wa Mheshimiwa Joseph Justin Monko ambao ni wanafamilia, viongozi na wadau wa maendeleo kutoka Singida Kaskazini. Wamekuja kushuhudia kuapishwa kwa Mbunge wao, wakiongozwa na mke wake, Ndugu Regina Monko. Karibuni sana wageni kutoka Singida Kasikazini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wako pia wageni 44 wa Mheshimiwa Dkt. Stephano Lemomo Kiruswa ambao ni wanafamilia viongozi na wadau wa maendeleo kutoka Jimbo la Longido, nao wamekuja kushuhudia kuapishwa kwa Mbunge wao wakiongozwa na mke wa Mheshimiwa Mbunge ambaye ni Ndugu Agnes Kiruswa. karibuni sana wageni kutoka Longido. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 35 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, ambao ni wanafamilia, viongozi na wadau wa maendeleo kutoka Jimbo la Songea Mjini, nao wamekuja kushuhudia kuapishwa kwa Mbunge wao. Karibu ni sana wageni kutoka Songea Mjini. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wawili wa Ofisi ya Bunge kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya wanawake (*UN WOMEN*) ni washauri elekezi katika masuala ya jinsia, ambao ni Mheshimiwa Sarmite Bulte kutoka Canada na Ndugu Fortunata Temu kutoka Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 80 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambao ni wanachuo wa mwaka wa kwanza Kitivo cha Elimu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 29 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wana Maombi kutoka Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana.

Tunaona pia wageni sita wa Wabunge wa Mkoa Iringa ambao ni viongozi wa kutoka Chama cha Walimu cha Mkoa huo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni waliotembela Bunge kwa ajili ya mafunzo, na hawa ni wageni 67 ambao ni Jumuiya ya Wanachuo waliokoka kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, *CASFETA (The Christ Ambassadors Students Fellowship Tanzania)*. Karibuni sana, kumbe hawa wametangazwa mara mbili. Wageni wetu tunawakaribisha sana Bungeni kujifunza namna tunavyofanya kazi na pia kuangalia namna mambo yanavyokwenda. (*Makofi*)

Tangazo lingine Waheshimiwa Wabunge linatoka kwa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaye ni Mwenyekiti wa Ibada ya *Chapel* Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo siku ya tarehe 30 Julai, 2018 saa saba mchana baada ya kusitisha shughuli za Bunge kutakuwa na ibada, kwa hiyo, Wabunge wote mnakaribishwa kwenye *Chapel* ya Bunge kwenye ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge baada ya matangazo haya, Mheshimiwa Chenge ataingia kuendelea na ratiba inayofuata.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo Naibu Spika unaondoka? (*Kicheko*)

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo mwishoni huku kabisa.

**MWENYEKITI:** Nimeshamwita Katibu!

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Aah! ulikuwa hujakaa sasa. Nakuomba Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mwongozo!

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana, mwongozo wangu ni lbara ya 68(7) nafikiri inaeleweka kwa yale yaliyotokea hapa asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wangu ni wenye faida. Hapa asubuhi tulipewa taarifa ya michezo ilivyofanyika pale Dar es Salaam. Tumepata dhahabu, shaba na mambo mengi, lakini katika shughuli hiyo tumepiga makofi sana imenisikitisha sana. Tunapokuwa tunashindana Kibunge ina maana tunawakilisha nchi. Mtu ameshinda amepata dhahabu kukimbia mita 800, 1500, kutembea haraka, mwisho ni makofi. Nataka kuomba unipe mwongozo wako katika Bunge ni dhambi mtu akileta medali asipewe chochote kuanzia hata milioni mbili? Kuna kosa gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nyongeza yangu juzi pale Zanzibar, Zanzibar Herros wameshinda wameingia fainali mashindano ya Afrika Mashariki. Rais Shein amewaita pale Ikulu na kila mchezaji akapewa kiwanja. Naomba Bunge hili tuwape mkono wa ahsante walioshiriki mashindano haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulembo nikushukuru kwa hilo, sina hakika kama kweli ulikuwa unataka mwongozo wa Kiti, kwa vile tukio hili ni tukio letu kama Bunge na umetoa wazo zuri tu, acha tulichukue na uongozi wetu wa Bunge utaona ni jinsi gani tunavyoweza kutumia ushauri wako kuboresha shughuli zetu za michezo na hasa kwa hawa wanaofanya vizuri katika michezo hii. Kwa hiyo, niishie hapo,

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2017 yaani [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill, 2017]**

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni 86 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria Mbalimbali Na. 5 wa Mwaka 2017 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill, 2017] kama ulivyorekebisha kwa mujibu wa jedwali la marekebisho sasa usomwe mara ya pili na Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye lipitisha Muswada huu kuwa sehemu ya Sheria za Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, napenda kumshukuru kwanza Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na afya njema na kuniwezesha kuendelea kutekeleza majukumu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndani na nje ya Bunge hili. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili, siku ya leo kuwasilisha maelezo ya Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa huu ni Mkutano wa Kwanza tangu mwaka huu ulipoanza nakutakia wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge, Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kheri ya mwaka mpya 2018. Mwenyezi Mungu aendeleo kuwabariki na kuwaongoza ipasavyo katika utekelezaji wa majukumu yenu.



Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dotto Mashaka Biteko, Mbunge wa Jimbo la Bukombe kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Madini. Mwenyezi Mungu aendelee kumjalilia hekima na busara katika utekelezaji wa majukumu yake ya Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbo, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini, Mheshimiwa Justin Monko, Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini na Mheshimiwa Dkt. Stephen Kisurwa Mbunge wa Jimbo Longido, kwa kuchaguliwa na wananchi wa Majimbo yao na kisha kuapishwa kuwa Wabunge wa Bunge hili. Nawatakiya mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yao ya Kibunge kwa maslahi na manufaa ya wananchi waliochagua pamoja na taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza pia Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Licha ya changamoto mbalimbali tunatambua kuwa tuna wajibu wa kutekeleza ipasavyo majukumu yetu kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru wananchi wote kwa kuendelea kutupatia ushirikiano kuanzia ushauri, maombi, sala, dua, taarifa muhimu na kadhalika na hivyo kutusaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisha ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2017 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill, 2017]* ambao uko mbele ya Bunge lako Tukufu, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohamed

Omary Mchengelwa, Mbunge wa Rufiji na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Najima Mtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum kwa ushirikiano na ushauri walioitupatia wakati wa kupitia muswada huu katika ngazi ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii ilifanya kazi nzuri ya kuuchambua Muswada huu kusikiliza na kuchambua maoni yaliyowasilishwa na Wadau walioitwa mbele ya Kamati hiyo na kisha kuishauri Serikali namna ya kuuboresha Muswada huu. Ushauri na maoni ya Kamati hiyo vimezingatiwa ipasavyo na Serikali kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa kuwa Kamati za Kudumu za Bunge zinafikia ukomo wake kwa mujibu wa Kanuni ya 116(7) ya Kanuni za Kudumu, Toleo la Januari 2016, napenda kutumia fursa hii kuipongeza na kuishukuru sana Kamati hiyo ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri na kubwa waliyoifanya wakati wa uhai wake ikiwemo kuchambua na kushauri ipasavyo Miswada ya Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kamati hii Bunge lako Tukufu limeweza kutunga sheria mbalimbali. Tunampongeza Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengelwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Najima Murtaza Giga, kwa uongozi bora pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa Kazi nzuri na ushirikiano mkubwa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru Kamati hiyo na Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa ushirikiano mzuri walioipatia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake. Tunazipongeza Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa kazi nzuri. Tunawatakia kila la kheri na Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki katika maisha na utumishi wenu wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2017 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill,*

2017] unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria nne. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuboresha na kuimarisha utekelezaji wa Sheria hizo kwa kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa kuzitumia na kuongeza masharti mengine ili kuleta uwiano kati ya sheria zinazorekebisha na sheria zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na kubadilisha vifungu vya sheria kwa kufuta baadhi vifungu vya sheria hizo na kuviandika upya. Kufuta baadhi ya maneno kwenye vifungu vya sheria, kuingiza maneno mapya na kuongeza vifungu vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria zinazopendekezwa kurekebisha kupitia Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

(a) Sheria ya Ufilisi, Sura ya 25 (*The Bankruptcy Act, Cap 25*);

(b) Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 (*The Budget Act, Cap 439*);

(c) Sheria ya Ardhi, Sura 113; (*The Land Act, Cap 113*); na

(d) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 (*The Public Service Act, Cap 298*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu kuu Tano, ambapo Sehemu ya Kwanza inaaisha masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na tamko kuhusu marekebisho ya sheria mbalimbali zinazopendekezwa kurekebisha kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza marekebisho katika sheria ya Ufilisi, Sura ya 25 (*The Bankrupt Act, Cap 25*), ibara ya nne (4) ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha pili (2) cha

Sheria hiyo ya Ufilisi kwa kuongeza tafsiri ya maneno *official receiver*. Maneno hayo yametumika katika sheria hiyo ya Ufilisi lakini yalikuwa hayajapewa tafsiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa Kabidhi Wasii Mkuu ndiye anayetokeleza majukumu ya *official receiver* na kwa kuwa Kabidhi Wasii Mkuu anateuliwa chini ya Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Kabidhi Wasii, Sura ya 27 (*The Administrators General Powers and Functions Act, Cap 27*), Muswada unapendekeza tafsiri ya maneno hayo iwe kama ifuatavyo:-

*“Official Receiver means Administrator General Appointed Pursuant to the Provision of the Administrator General Powers and Functions Act)”*

Lengo la marekebisho hayo ni kuweka tafsiri ya maneno hayo ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria ya Ufilisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 74(2) cha Sheria ya Ufilisi kinaelekeza pamoja na mambo mengine kuwa *Official Receiver* na *Deputy Official Receiver* atateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya Sheria. Kwa kuwa Muswada umependekeza kuwa *Official Receiver*, Kabidhi Wasii Mkuu ambaye anateuliwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kabidhi Wasii, Jedwali la marekebisho linapendekeza ya kifungu hicho kirekebishwe kwa kuondoa masharti kuhusu uteuzi wa *Official Receiver* chini ya kifungu hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kufanya tafasiri ya neno *Official Receiver* ambayo inapendekezwa katika Muswada huu isipingane na masharti ya kifungu hicho cha 74(2) cha Sheria ya Ufilisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 (*The Budget Act, Cap 439*). Kifungu cha 21(2) cha Sheria hii ya Bajeti kinaainisha masharti kwamba mpango mwongozo wa bajeti ya Serikali uwasilishwe katika Mkutano

wa Bunge la Februari kila mwaka, au wiki ya kwanza baada ya Bunge kuitishwa iwapo hakuna Mkutano wa Bunge mwezi huo.

Kwa upande mwingine Kanuni ya 94(1)(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, inaelekeza kuwa Bunge katika Mkutano wake wa Mwezi Oktoba/Novemba kwa kila mwaka litakaa kama Kamati ya Mpango kwa siku zisizopungua tano ili kukidhi matakwa ya ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Tanzania ya Mwaka 1977 kwa kujadili na kuishauri Serikali kuhusu mapendekezo ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata na pia kupokea kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu mwongozo wa kuandaa mpango wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo Ibara ya sita (6) ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inapendekeza kwamba kifungu hicho cha 2(1) cha Sheria ya Bajeti kirekebishwe kwa kuweka masharti kwamba mpango na mwongozo wa Bajeti ya Serikali utawasilishwa katika Mkutano Bunge wa mwezi Oktoba au Novemba kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapendekezwa pia kuwa iwapo mwezi Oktoba au Novemba itakuwa mwezi wa uchaguzi mkuu basi Mpango na Mwongozo wa Bajeti uwasilishwe katika Mkutano wa Pili wa Bunge baada ya uchaguzi Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la marekebisho haya ni kuoanisha masharti ya Sheria ya Bajeti ya yale ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kuhusu muda wa kuwasilisha mpango wa mwongozo wa bajeti katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na hivyo kuondoa mgongano uliopo sasa hivi baina ya Sheria ya Bajeti na Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu jambo hilo na hivyo kuwezesha Sheria ya Bajeti kutekelezwa kwa ufanisi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Ardhi, Sura 113 (*The Land Act, Cap 113*). Sehemu ya 10 ya Sheria hiyo ya Ardhi inaainisha masharti kuhusu kutumia ardhi kupata mkopo yaani *mortgage*. Hata hivyo, Sheria hiyo ya Ardhi haijaainisha masharti kuhusu matumizi ya mkopo unaopatikana kwa kuweka rehani hati ya kumiliki ardhi.

Kutokana na kukosekana kwa masharti hayo, baadhi ya wamiliki wa ardhi wakiwemo Wawekezaji wamekuwa hawatumii mikopo hiyo kuendeleza ardhi husika huku wamiliki wengine wakitumia mikopo waliyoipata kwa kuweka dhamana ardhi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwekeza nje badala ya kufanya uwekezaji huo hapa nchini na hivyo kusababisha ardhi waliyopewa kutoendelezwa na kutelekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu huo na kwa kuzingatia kuwa Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inamtaka kila mtu katika Jamhuri ya Muungano kulinda maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mali ya mamlaka ya nchi na mali yote inayomikiwa kwa pamoja na wananchi; na kutunza vizuri mali na mamlaka ya nchi na ya pamoja na kuendesha uchumi wa Taifa kwa umakini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya Taifa hili,

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sheria za *“The Natural Wealth and Resource Permanent and Sovereignty Act 2017* na *The Natural Wealth and Resources Contract (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms Act 2017”* zinatambua ardhi kuwa ni moja ya maliasili na rasilimali za nchi ambazo kila mtu ana wajibu wa kulinda na kuitunza kwa mujibu wa Ibara ya 27 ya Katiba, Ibara ya tisa (9) ya Muswada huu kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inapendekeza kuongeza vifungu vipya vifuatavyo kuhusu masharti ya mkopo unaotokana na kuweka dhamana ya ardhi pamoja na masharti kuhusu matumizi ya mkopo huo.

(a) Kifungu kipyua cha 120(A) Kama kilivyorekebisha kupitia jedwali la marekebisha, kinaelekeza kuwa mtu anaweza kutumia ardhi kama dhamana ya kupata mkopo kutoka benki au taasisi ya fedha ndani au nje ya nchi kwa ajili ya kuendeleza ardhi husika au kwa ajili ya uwekezaji mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kifungu hicho kinaelekeza kuwa iwapo ardhi husika itakuwa imeendelezwa mkopo huo utapaswa kutumika kwa ajili ya kuendeleza zaidi ardhi hiyo uwekezaji au kwa ajili ya matumizi mengine. Kwa upande mwingine kama ardhi inayowekwa rehani itakuwa haijaendelezwa au imeendelezwa kidogo mkopo huo utapaswa kutumika kwa ajili kuendeleza ardhi yote au sehemu ya ardhi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mmiliki wa ardhi yaani mkopeshwaji amepewa wajibu wa kuwasilisha kwa Kamishna wa Ardhi taarifa kuhusu namna mkopo husika ulivyoelekezwa katika kuendeleza ardhi iliyowekwa rehani. Taarifa hiyo itawasilishwa ndani ya miezi sita tangu mkopo husika kutolewa.

(b) Kifungu kipyua cha 120(B) kama kilivyorekebisha kupitia jedwali la marekebisha kinaelekeza kuwa mkopo uliotolewa na Benki au taasisi ya fedha ya ndani au nje kutokana na ardhi kuwekwa rehani utatumika kwa ajili ya uwekezaji hapa nchini. Aidha, inapendekezwa kwamba benki au taasisi ya fedha ya ndani au ya nje ya nchi inayotoa mkopo unahusisha dhamana ya ardhi itapaswa kuwasilishwa kwa Kamishna wa Ardhi tamko kwamba mkopo husika unawekezwa katika Jamhuri ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisha haya mbali ya kutekeleza masharti ya ibara 27 ya Katiba na Sheria za *“The Natural Wealth and Resource Permanent and Sovereignty Act, 2017 na The Natural Wealth and Resources Contract (Review and Renegotiation of Unconscionable Terms Act, 2017,* kwa kusimamia matumizi ya rasilimali ya ardhi

inayotolewa kama dhamana kupata mkopo yatasaidia pia kuendeleza ardhi inayowekwa rehani na kukuza uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho Muswada unapendekeza kifungu kipya ya 120C cha Sheria ya Ardhi ambacho kinachoweka masharti kwamba masharti ya vifungu vipya vya 120A(2)(3) na 120B(1) hayatakuwa kwa wamiliki wa ardhi wenye hati ya kimila yaani wanaomiki ardhi kwa njia ya kimila. Lengo ni kuweka bayana wigo wa utekelezaji wa masharti yanayopendekezwa ili masharti haya yositumike kwa wananchi wa kipato cha chini hasa kwa maeneo ya vijijini ambao wanamiliki ardhi katika utaratibu wa kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho, Kifungu kipya cha 120 C kilichokuwa katika Muswada sasa kimeandikwa Kifungu kipya cha 120 D, Kifungu hicho kinaweka masharti kwamba ukiukwaji wa masharti wa Vifungu vipya vya 120A, 120 vya Sheria ya Ardhi utakuwa ni ukiukwaji wa masharti ya haki ya kumiliki na kutumia ardhi chini ya Kifungu cha 45(2) cha Sheria ya Ardhi. Kwa sababu hiyo, Ibara ya nane (8) ya Muswada inapendekezwa marekebisho kwa kile Kifungu cha 45(2) cha Sheria ya Ardhi kwa kuongeza haya mpya ya (g) ambayo inaelekeza kuwa ukiukwaji wa Vifungu vya 120A na 120B vya Sheria ya Ardhi itakuwa ni moja ya sababu za kubatilisha haki ya kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa ni masharti ya Vifungu vya Sheria, Vifungu vya 120A na 120B yanatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada pia kupitia kupitia Jedwali la Marekebisho unapendekeza Kifungu kipya cha 120E cha Sheria ya Ardhi, Kifungu hicho kwenye Muswada kilikuwa ni Kifungu cha 120D na kinaweka masharti kwamba utaratibu wa utekelezaji wa Vifungu vya 120A na 120B vinavyopendekezwa kupitia Muswada huu utainishwa



katika Kanuni ambazo zitatungwa na Mheshimiwa Waziri. Lengo la mapendekezo haya ni kurahisisha utekelezaji bora wa masharti ya Vifungu hivyo vipya vya 120A, 120B vya Sheria ya Ardhi kupitia masharti yatakayoainishwa katika Kanuni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho, marekebisho ya mwisho katika Sheria ya Ardhi ni kukihamisha Kifungu cha 120A kinachotajwa sasa katika Sheria hizi, kuwa Kifungu cha 120F. Lengo la marekebisho hayo ni kuweka mtiririko mzuri wa usomaji wa Sheria hiyo kutokana na masharti ya vifungu vipya vilivyopendekezwa katika Sheria hiyo kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tano, ya Muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 yaani *The Public Service Act, Cap. 298*. Ibara ya 12 ya Muswada huu kama ilivyorekebishwa kupitia Jedwali la Marekebisho inapendekeza kuongeza Kifungu kipya cha 25A ambacho kinaainisha masharti kuhusu umri wa kustaafu. Sheria ilivyo sasa haina masharti hayo isipokuwa umri wa kustaafu umetajwa katika Sheria zinazoanzisha Mifuko ya Hifadhi za Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sheria hii ndiyo inayosimamia Utumishi wa Umma, kuna umuhimu wa kuainisha umri wa kustaafu kwa Watumishi wa Umma ndani ya Sheria ya Utumishi wa Umma. Hivyo, Kifungu kipya cha 25A kinachopendekezwa kupitia Muswada huu, kinaainisha kwamba umri wa kustaafu kwa hiari kwa Watumishi wa Umma utakuwa kuanzia miaka 55 na kwamba umri wa kustaafu kwa lazima utakuwa miaka 60.

Hata hivyo, uzoefu umeonesha kwamba Maprofesa na Waadhiri Waandamizi wa Vyuho vikuu vya Umma pamoja na Madaktari Bingwa wa binadamu wa Hospitali za Umma wamekuwa wakihitajika kuendelea kutoa huduma, utaalam na uzoefu wao licha ya kufikisha umri huo wa kustaafu na hivyo kulazimika kuajiriwa na Serikali kwa Mkataba. Hata

hivyo, hatua hiyo imekuwa ikiongeza gharama kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo Muswada unapendekeza kwamba umri wa kustaafu Maprofesa na Waadhiri Waandamizi wa Vyuo Vikuu vya Umma, pamoja na Madaktari Bingwa wa binadamu wa Hospitali za Umma uwe miaka 60, kwa wale wanaostaafu kwa hiari na miaka 65 kwa wale wanaostaafu kwa lazima. Marekebisho haya yatawezesha Serikali kuendelea kupata huduma, Wataalam na uzoefu wa watumishi hao na pia kupunguza gharama ambayo Serikali imekuwa ikiingia kwa kuwaajiri kwa Mikataba mara wanapostaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu kipya cha 25B ambacho kilikuwa kinapendekeza masharti kuhusu mamlaka ya kubadilisha umri wa kustaafu yaani *The Power to Alter Age of Retirement* kimefutwa kama kinavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya na kwa mara nyingine tena nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwasilisha maelezo haya, kuhusu Muswada wa Sheria ya marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 5 wa Mwaka 2017 yaani (*The Written Laws Miscellaneous Amendments*) (No.5) Bill of 2017 na naomba Bunge lako Tukufu liujadili na kupitisha katika hatua ya kusomwa kwa Mara ya Pili na Mara ya Tatu ili hatimaye uwe sehemu ya Sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Ahsanteni, nakushukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa wasilisho lako.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**SPECIAL BILL SUPPLEMENT**

**No. 7**

**19<sup>st</sup> October, 2017**

*to the Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.7 Vol. 98 dated 19<sup>st</sup> October, 2017*  
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

---

THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.5)  
ACT, 2017

ARRANGEMENT OF SECTIONS

*Section Title*

PART I  
PRELIMINARY PROVISIONS

1. Short title.
2. Amendment of Certain Written Laws.

PART II  
AMENDMENT OF THE BANKRUPTCY ACT,  
(CAP.25)

3. Construction.
4. Amendment of section 2.

PART III  
AMENDMENT OF THE BUDGET ACT,  
(CAP.439)

5. Construction.
6. Amendment of section 21.

PART IV  
AMENDMENTS OF THE LAND ACT,  
(CAP. 113)

7. Construction.
8. Amendment of Section 45.
9. Addition of new section 120A.
10. Amendment of section 120A.

PART V  
AMENDEMENT OF THE PUBLIC SERVICE ACT,  
(CAP.298)

11. Construction.
12. Amendment of Part V.

**NOTICE**

---

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the general public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam,  
17<sup>th</sup> October, 2017

**JOHN W. H. KIJAZI**  
*Secretary to the Cabinet*

**A BILL**  
*for*

**An Act to amend certain written laws.**

**ENACTED** by Parliament of the United Republic of Tanzania.

PART I  
PRELIMINARY PROVISIONS

Short title                    **1.** This Act may be cited as the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Act, 2017.

Amendment of certain written laws                    **2.** The Written Laws specified in various Parts of this Act are amended in the manner specified in their respective Parts.

PART II  
AMENDMENT OF THE BANKRUPTCY ACT,  
(CAP.25)

Construction Cap. 25                    **3.** This Part shall be read as one with the Bankruptcy Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 2                    **4.** The principal Act is amended in section 2, by inserting in its appropriate alphabetical order the following new definition:  
"Official Receiver" means the Administrator- General appointed pursuant to the provisions of the

Cap.27 Administrator- General (Powers and Functions) Act;"

PART III  
AMENDMENT OF THE BUDGET ACT,  
(CAP.439)

Construction  
Cap.439 **5.** This Part shall be read as one with the Budget Act,  
hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment  
of section 21 **6.** The principal Act is amended in section 21, by deleting the  
word "February" wherever it appears in subsection (2) and  
substituting for it the words "October or November".

PART IV  
AMENDMENT OF THE LAND ACT,  
(CAP. 113)

Constructio  
n  
Cap. 113 **7.** This Part shall be read as one with Land Act, hereinafter  
referred to as the "principal Act".

Amendmen  
t of section  
45 **8.** The principal Act is amended in section 45(2), by-  
(a) deleting the "fulstop" appearing at the end of  
paragraph (f) and substituting for it a "semicolon";  
(b) inserting immediately after paragraph (f) the  
following new paragraphs:  
"(g) where there is contravention of section 120A or  
120B."

Addition of  
section  
120A **9.** The Principal Act is amended by adding immediately after  
section 120 the following new sections:

"Mortgage  
of Land

**120A.**-(1) Subject to the provisions of  
this Act, a person may mortgage any land for  
the purpose of obtaining money from the  
local bank or financial institution for  
developing his land or for any other  
investment.

(2) Where a land mortgaged under  
subsection (1) is undeveloped or  
underdeveloped, the money obtained from  
the local bank or financial institution shall be  
utilized to develop part or whole of such  
mortgaged land.

(3) A Mortgagor shall within six months  
submit to the Commissioner information as to

the manner in which the money obtained from the mortgage is invested to develop the mortgaged land.

Money to be invested in Tanzania

120B.-(1) Money obtained from a mortgage from a local bank or financial institution referred to under section 120A shall be invested in Tanzania.

(2) Where the Mortgagor is a bank or a financial institution, the Mortgagor shall submit to the Commissioner a declaration that the money obtained from the mortgage is invested in Tanzania.

Non compliance under mortgage of land

**120C.** Failure to comply with the requirements under sections 120A and 120B shall constitute a breach of conditions of right of occupancy provided for under section 45(2).

Procedure relating to mortgage of land

**120D.** The procedure for administration and enforcement of section 120A and 120B shall be prescribed in the Regulations.

Amendment of section 120A

**10.** The Principal Act is amended by redesignating the contents of section 120A as contents of section 120D.

PART V  
AMENDEMENT OF THE PUBLIC SERVICE ACT,  
(CAP.298)

Construction of Part V

**11.** This Part shall be read as one with the Public Service Act, hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of Part V

**12.** The principal Act is amended in Part V by inserting immediately after the heading the following:

"Age of retirement of public servant

**25A.-(1)** A public servant may retire from the Service-

(a) in case of voluntary retirement after attaining the age of fifty five years; and

(b) in case of compulsory retirement after attaining the age of sixty years.

(2) Notwithstanding subsection (1), a professor or a senior lecturer of a public university or a medical specialist of a public hospital may retire from the Service -

(a) in the case of voluntarily retirement, after attaining the age of sixty years; and

(b) the term in the case of compulsory retirement, after attaining the age of sixty five years .

(3) For the purposes of this section, the term:

(a) "professor" includes an associate professor; and

(b) "medical specialist" includes any specialist above the medical specialist.

Power to  
alter age of  
retirement

**25B.** The Minister may, in consultation with the President and by order published in the *Gazette*, alter the age of retirement of a public servant in such a manner as he may deem necessary, and every such alteration shall take effect as if it were provided for in this Act."

---

### **OBJECTS AND REASONS**

---

This Bill proposes to amend four laws namely, the Bankruptcy Act, Cap. 25, the Budget Act, Cap.439, the Land Act, Cap 113 and the Public Service Act, Cap.298.

The proposed amendments to the respective laws are intended to cure the shortfalls occasioned during the implementation of the respective laws.

This Bill is divided into Four Parts. Part I deals with Preliminary Provisions which includes the title of the Bill and the manner in which the laws proposed to be amended, are amended in their respective Parts.



Part II proposes to amend section 2 of the Bankruptcy Act, Cap. 25 by inserting in its alphabetical order the definition of the term Official Receiver to mean the Administrator General. This is due to the fact that all the functions of the Official Receiver are performed by the Administrator General.

Part III proposes amendment to the Budget Act, Cap.439 whereby section 21(2) is amended by changing the time frame within which the Plan and Budget Gridlines shall be laid before the National Assembly, which shall be October or November of each year. The objective of the amendment is to harmonise the time frame as that preferred under the Standing Orders of National Assembly, 2016 edition.

Part IV of the Bill proposes to amend the Land Act Cap, 113, whereas section 45 is amended by adding provisions regarding default against mortgage of land to considered as a ground for revocation of the right of occupancy.

Sections 120A, 120B and 120C are being added with the aim to allow any loan obtained through mortgaging a piece of land in Tanzania to be used for the development of the same parcel of land which has been used as a security. This condition is only for undeveloped and underdeveloped land. This amendment is intended to bind the occupier of the right of occupancy to be responsible and give feedback on how he has procured the loan obtained through mortgage. Further, this amendment also aims at making sure that moneys obtained from mortgaging piece of land in Tanzania is strictly used to develop the same mortgaged piece of land.

Through these amendments both local and foreign banks or financial institutions are required to disclose information to the Commissioner for Lands to ensure that the money borrowed through mortgage is actually invested on or develop a particular mortgaged land within Tanzania. As a sanction, through these amendments any loan obtained through mortgage and used for investment outside Tanzania shall be invalid. Further, this amendment allows legislations to be executed properly and to legitimize mortgages of rights of occupancy that have been effected before introducing of these amendments.

Part V of the Bill proposes amendment to the Public Service Act, Cap. 298, whereas a new section 25A is introduced with a view to provide for age of retirement for public servants. The amendment further propound on a new Scheme of retirement age for Public Universities professors, senior lecturer and medical specialist in the public hospitals. This new scheme intends to extend the voluntary retirement from the service of the above named categories to be sixty years while the compulsory age is extended to sixty five years. The amendment aims at implementing a recent decision of the government that changed retirement age of professors, senior lecturers and medical specialist in public

university and public hospitals. The extension of retirements to these categories will address the shortage of professor and senior lecturers in public universities and medical specialist in public hospitals. The extension will reduce the costs incurred by the government for re-engaging retired professors, senior lecturers and medical specialist under contract. The extension of retirement age will further afford more time for professors and senior lecturer in public hospitals to serve the nation and mentor young academician and medical officers.

MADHUMUNI NA SABABU

Muswada huu unapendekeza kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali Tano na ambazo ni Sheria ya Ufilisi, Sura ya 25 Sheria ya Bajeti Sura 439, Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, NA Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 238.

Mapendekezo ya marekebisho haya yalitokana na mapungufu mbalimbali ya utekelezaji wa sheria hizo.

Muswada huu umegawanywa katika Sehemu Nne Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha, jina la Muswada na namna ambavyo Sheria zinazopendekezwa kurekebishwa zitakavyorekebishwa ndani ya Muswada huu.

Sehemu ya Kwanza inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 2 cha Sheria ya Ufilisi, Sura ya 25 kwa kupangilia mtiririko wa maneno ya kialphabeti katika kifungu cha 2 na kutoa tafsiri ya neno Mpokezi MKuu kuwa na maana ya neno Kabidhi Wasii Mkuu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa shughuli zote za "Mpokezi Mkuu" zinafanywa na "Kabidhi Wasii Mkuu" ambaye anapendekezwa ateuliwe na Rais ili aweze kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na hili.

Sehemu ya Pili inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 21(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 kwa kuandika upya muda wa kuwasilisha Bungeni muongozo wa kuandaa mpango wa bajeti lengo la marekebisho hayo ni kuondoa mkinzano na kuoanisha na muda uliorejewa katika kanuni za Bunge, Kanuni ya 94(1) na (2) ya Kanuni hizo, toleo la 2016.

Sehemu ya Tatu inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura 113 ambapo kifungu cha 45 kimerkebishwa kwa kuongeza masharti ya adhabu inayotokana na ukiukwaji wa masharti kwa mtu anayeweka dhamana ya milki ya ardhi.

Vifungu vya 120A, 120B na 120C navyo vimeongezwa ili kuwezesha fedha zinazopatikana kutokana na mkopo uliyotolewa kwa dhamana ya milki ya ardhi ya Tanzania zitumike kuendeleza sehemu au ardhi yote iliyowekwa rehani. Sharti hili litahusu milki ambazo hazijaendelezwa. Aidha, marekebisho haya pia yanakusudia kuweka wajibu kwa mkopaji na mkopeshaji kuwasilisha taarifa kwa Kamishna wa Ardhi kuhusu fedha zilizopatikana kutokana na dhamana ya milki ya ardhi zilivyowekezwa kwa ajili ya kuendeleza ardhi husika. Aidha, marekebisho haya yanalenga pia kuweka wajibu kwa fedha zinazokopeshwa kutokana na dhamana ya milki ya ardhi ya Tanzania ziweze kuwekezwa Tanzania.

Aidha, Benki na Taasisi za fedha za ndani na nje ya nchi nazo zinatakiwa kuwasilisha kwa Kamishna wa Ardhi tamko kwamba fedha inayotolewa kutokana na dhamana ya milki ya ardhi ya Tanzania zinawekezwa Tanzania. Kwa maudhui ya marekebisho haya, uwekaji rehani milki ya ardhi katika Benki au Taasisi ya Fedha za ndani au nje ya nchi ambazo fedha zinayopatikana haitawekezwa Tanzania zitakuwa ni batili. Jambo jingine katika marekebisho haya ni kuwezesha kutungwa kwa kanuni za utekelezaji wa masharti ya fungu hili na kuhlalisha rehani za milki za ardhi zilizofanyika kabla ya marekebisho haya.

Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya Marekebisho kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 ambapo kifungu kipya cha 25A kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuweka kwenye Sheria masharti ya umri wa kustaafu kwa watumishi wa Umma, Masharti haya hayapo ndani ya Sheria kwa sasa. Aidha, mapendekezo ya kuongeza kifungu kipya yanalenga kuweka utaratibu mpya wa umri wa kustaafu kwa maprofesa na wahadhiri waandamizi wa vyuo vikuu vya umma na madaktari bingwa wa magonjwa ya binadamu wa hospitali za umma. Mfumo huu mpya unalenga kuongeza umri wa kustaafu Utumishi wa umma kwa ridhaa kwa maprofesa na wahadhiri waandamizi wa vyuo vikuu vya umma na madaktari bingwa wa magonjwa ya binadamu wa hospitali za umma ili umri huo uweze kuwa ni miaka sitini kwa wale ambao wanastaafu kwa hiari na kwa wale ambao wanastaafu kwa lazima iwe ni miaka sitini na tano. Marekebisho haya yanalenga kutekeleza maamuzi ya Serikali yanayolenga kuongeza umri wa kustaafu kwa maprofesa, wahadhiri waandamizi wa madaktari bingwa wa binadamu kutoka vyuo vikuu vya umma na hospitali za umma. Kuongeza umri kwa kada hizi kutapunguza gharama kwa Serikali ya kuingia mikataba na wataalamu hawa mara tu wanapostaafu, na pia kutaongeza muda kwa wataalamu, wengine kuweza kulitumikia Taifa kwa muda mrefu zaidi na pia kusaidia kufundisha na kukuza wataalam wachanga walioko nchini.

Dodoma,  
16 Oktoba, 2017

**GEORGE M. MASAJU**  
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON.  
GEORGE M. MASAJU, THE ATTORNEY GENERAL, AT THE SECOND  
READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS  
(MISCELLANEOUS AMENDMENTS) (NO.5) ACT, 2017"**

*(Made under S.O. 86(10)(b))*

A Bill entitled "the Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Act, 2017" is generally amended as follows:

- A:** By adding immediately after Clause 4 the following new Clause:  
"Amendment of section 74" **5.** The principal Act is amended in section 74 by deleting the words "The official receiver and the" appearing at the beginning of subsection (2) and substituting for them the article "The".
- B:** By deleting Clause 6 and substituting for it the following:  
"Amendment of section 21" **6.** The principal Act is amended in section 21, by-
- (a) deleting the words "by February" wherever they appear in subsection (2) and substituting for them the words "in October or November";
  - (b) adding immediately after subsection (2) the following:  
" (3) Notwithstanding subsection (2), where the general election is scheduled to be held in the month of October or November, the Minister may lay the Plan and Budget Guidelines during the second meeting of the National Assembly after the general election."
  - (c) renumbering sections 3, 4 and 5 as sections 4, 5 and 6 respectively.
- C:** In Clause 7 by adding immediately after the word "with" appearing in the first line the article "the".
- D:** In Clause 9-
- (a) by deleting the marginal note and substituting for it the following-  
"Addition of new sections";
  - (b) in the proposed section 120A, by-
    - (i) deleting the words "local bank or financial institution" appearing in subsection (1) and substituting for them the words "local or foreign bank, or local or foreign financial institution";
    - (ii) deleting the proposed subsection (2) and substituting for it the following:  
" (2) The money obtained from the local or foreign bank, or local or foreign financial institution shall, -
      - (a) where the mortgaged land is developed, be utilized for further development of the land, for investments or for other purposes; and
      - (b) where the mortgaged land is undeveloped or underdeveloped, be utilized to develop part or

whole of such mortgaged land."

(c) in the proposed section 120B, by -

- (i) deleting the words "local bank or financial institution" appearing in subsection (1) and substituting for them the words "local or foreign bank, or local or foreign financial institution";
- (ii) deleting the proposed subsection (2) and substituting for it the following:

"(2) Where the mortgagee is a local or foreign bank, or local or foreign financial institution, the mortgagee shall submit to the Commissioner a declaration that the money obtained from the mortgage is invested in Tanzania."

(iii) by adding immediately after subsection (3) the following:

"(4) For the purposes of this section-

"local bank" means any bank licensed by the Bank of Tanzania to undertake the banking business in Tanzania;

"local financial institution" means any entity licensed in Tanzania to engage in the banking business, but limited as to size, locations served, or permitted activities as prescribed by the Bank of Tanzania or required by the terms and conditions of its license";

"underdeveloped" in respect of land, means a land which is not developed in accordance with the conditions of relevant rights of occupancy";

"undeveloped" in respect of land, means a land without improvement in, on, under or over such land or without any change of substantial nature in the use of such land."

(d) by adding immediately after the proposed section 120B the following:

""Scope of application

**120C.** The provisions of sections 120A (2), (3) and 120B(1) shall not apply to land held under the certificate of customary right of occupancy".

(e) by renumbering the proposed section 120C and 120D as sections 120D and 120E respectively.

**E:** In Clause 10, by re-designating section 120A as section 120F .

**F:** In PART V by deleting the word "AMENDEMENT" appearing in the Title and substituting for it the word "AMENDMENT".

**G:** In Clause 12 -

(a) in the proposed section 25A-

- (i) by deleting the word "after" appearing in the proposed subsection (1)(a) and (b) and substituting for it the word "upon";
- (ii) by deleting the word "after" appearing in the proposed subsection (2)(a) and (b) and substituting for it the word "upon";
- (iii) in the proposed subsection (3), by-
  - (aa) deleting the word "specialist" appearing at the end of paragraph (b) and substituting for it the word "doctor";
  - (bb) adding immediately after paragraph (b) the following new paragraph:

Cap. 346                   “(c) “public university” has the meaning ascribed to it under  
the Universities Act.””  
(b) by deleting the proposed section 25B.

Dodoma,  
....., 2018

**GMM**  
AG

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na hatua inayofuata ni kupokea maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada huu. Nani anawasilisha, Karibu Mwenyekiti. Mheshimiwa Mchengerwa karibu, una nusu saa lakini sio lazima umalize muda wote.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii kuwatakia heri ya Mwaka Mpya pamoja na kuwatakia afya njema Viongozi wetu wote wa Kitaifa, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano, pamoja na watumishi wote wa Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema ambaye amenijalia mimi afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu na kuwasilisha taarifa hii ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho Mbalimbali Na. 5 ya Mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mara yangu ya mwisho kufanya hivi katika kipindi cha takribani miaka miwili toka kuundwa kwa Kamati hii ya Katiba na Sheria ambayo Kikanuni imepewa jukumu kubwa sana la kujadili, kuchambua Muswada wa Sheria zote za Marekebisho ya Sheria Mbalimbali kabla hazijasomwa Bungeni kwa mara ya pili, ya tatu na kupitishwa kuwa sheria rasmi za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hii nakushukuru sana wewe, nimshukuru Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshiwa Naibu Spika na Wenyeviti wengine wote kwa kipekee kabisa Wajumbe wangu wa Kamati ya Katiba na Sheria ambao wamefanya kazi hii kubwa kwa kujitoa sana na kwa weledi wa hali ya juu katika kuhakikisha kwamba Sheria zote za Marekebisho ya Sheria Mbalimbali zinazopitishwa na Bunge hili zinakuwa ni nzuri na ubora wa kimaudhui unaotakiwa na zinazokidhi matakwa Kikatiba,

Kisheria, Kikanuni na Misingi mbalimbali ya Sheria za Kimataifa yaani *International Law Principles. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho Sheria Mbalimbali Na. 5 wa Mwaka 2017 yaani (*The Written Laws Miscellaneous Amendments*)( No. 5) of 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016. Kamati ya Katiba na Sheria iliupokea Muswada huu tarehe 17 Novemba, 2017 baada ya kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Tisa wa Bunge hili ili iufanye kazi na mnamo tarehe 17 Januari, 2018 Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe kwa niaba ya mtoa hoja ambaye Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Profesa Paramagamba John Aidan Mwaluko Kabudi pamoja na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa William Lukuvi walifika mbele ya Kamati yangu iliyoketi hapa Dodoma na kutoa maelezo kuhusu malengo na madhumuni ya Muswada huu wenye lengo la kufanya marekebisho mbalimbali katika Sheria husika na kwa madhumuni ya kuondoa upungufu ama kasoro zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zilizokusudiwa kufanyiwa marekebisho katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Sheria ya Ufilisi, Sura ya 25,
- (ii) Sheria ya Bajeti, Sura 439,
- (iii) Sheria ya Ardhi, Sura 413, na
- (iv) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 238.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 84(2) ya Kanuni ndogo za Kudumu za Bunge hili Toleo la Januari, 2016 na kuzingatia matakwa ya Ibara ya 4 ya Ibara ya 8 pamoja na Ibara ya 21 ya Katiba ya Jamhuri



ya Muungano iliyowapa wananchi nafasi ya kushiriki katika masuala mbalimbali yanayowahusu. Kamati iliwaalika Wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu. Napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru kwa dhati kabisa Wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao katika Muswada huu. Naomba kutambua mchango wa Wadau wafuatao:

- (i) Chama cha Mawakili Tanganyika,
- (ii) Chama cha Wataalam wa Chuo Kikuu (UDOM) yaani *UDOMASA*,
- (iii) Taasisi ya Sekta binafsi Tanzania,
- (iv) Jukwaa la Sera,
- (v) Chama cha Wataalam wa Sekta ya Benki Tanzania,
- (vi) Chama cha Madaktari Tanzani, na
- (vii) Chama cha Madaktari wa Meno Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo na madhumuni ya Muswada; maelezo ya jumla ya Muswada huu yapo katika taarifa ya mtoa hoja. Waziri wa Katiba na Sheria lakini pia yamesomwa hapa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mbele ya Bunge lako hili Tukufu. Malengo na madhumuni ya Muswada yaliyomo kwenye Muswada kuanzia Ukurasa wa saba mpaka wa 11na kwa faida ya muda naomba nisirudie tena maelezo haya ya sehemu hii yote iingie katika taarifa rasmi ya Bunge yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa jumla wa Muswada, pamoja na kwamba Muswada huu unaonekana ni mfupi sana na usio na mambo mengi ukiutazama kwa haraka haraka lazima nikiri kwamba huu ni mmoja wa Miswada ambayo Kamati yangu imetumia muda mwingi na umakini wa kutosha katika kuujadili na kuuchambua. Hii ni kwa sababu ya uzito wa mapendekezo ya marekebisho ambayo Serikali imekusudia kufanya katika Sheria ya Ardhi, Sura 113 na Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 238.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua Vifungu 12 vyote vya Muswada kwa kutazama usahihi wa Kimaudhui, Kisarufi na Kimuundo wa kila Kifungu kwa kulinganisha na

malengo na madhumuni ya Muswada pamoja na Sheria mama zinazofanyiwa marekebisho. Kamati pia katika uchambuzi huu ilijiridhisha katika marekebisho yanayopendekezwa na Serikali yanaendana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Sheria nyingine za nchi na matakwa Sheria na Mikataba ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maudhui ya Sheria kwa ujumla wake Kamati ilitazama mchakato mzima wa marekebisho wa Sheria hizi na hasa kama walengwa au watu wanaoguswa na marekebisho ya Sheria walishirikishwa katika kiwango cha kutosha na katika hatua za awali za marekebisho za Sheria hizi kabla ya Muswada husika haujasomwa Bungeni kwa mara ya kwanza tarehe 17 Novemba, 2017.

Mheshimwa Mwenyekiti, baadhi ya Vifungu katika Muswada huu havikuwa na mjadala wowote katika Kamati kwa sababu ni vifungu vya utangulizi na vya Muundo na visivyo na athari zozote katika Maudhuhi ya Msingi wa Muswada. Kwa mfano Kifungu cha 1, 2, 3, 4, 5, 7 na cha 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vifungu vilivyohitaji mjadala mpana kati ya Serikali na Kamati yangu ni Vifungu vya 8, 9 na 10 vinavyohusiana na marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 na Kifungu cha 12 kinachohusiana na marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 238.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali katika marekebisho yanayokusudiwa katika Sheria ya Ufilisi, Sura ya 25 na marekebisho yanayokusudiwa katika Sheria ya Bajeti, Sura 439.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha sita (6) cha Muswada ambacho kinarekebisha Kifungu cha 21(2) cha Sheria ya Bajeti. Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali kuwasilisha Bungeni Mwongozo wa Mpango wa Bajeti mwezi Oktoba na Novemba na badala ya mwezi Februari kama ilivyo sasa katika Sheria ya Bajeti ili kuendana

na muda uliotajwa katika Kanuni ya 94(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 ambayo inasema kwamba Mwongozo wa Mpango wa Bajeti utawasilishwa Bungeni katika Bunge la Oktoba na Novemba.

Mheshimwa Mwenyekiti, hata hivyo uzoefu umeonesha kwamba katika Mwaka uchaguzi wa Urais na Bunge, hasa Bunge jipya linapoanza kipaumbele cha kwanza cha shughuli za Bunge sio kujadili Miongozo na Mapendekezo ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaofuata na badala yake mapendekezo hayo yamekuwa yakiwasilishwa na kujadiliwa Bungeni katika Mkutano wa Bunge unaofuata. Kwa mantiki hii Kamati ilishauri Serikali iongeze Kifungu kitakachosomeka kama ifuatavyo:-

*"Notwithstanding the Provision of Subsection 2, The Provision of Section 21 shall not apply during the election year."*

Kifungu hiki kitatoa nafasi kwa Bunge kuendelea na shughuli zenye kipaumbele cha kwanza wakati wa kuanza kwa Bunge jipya lolote mara tu baada ya uchaguzi ambapo masharti ya Kanuni ya 23 ya Kudumu za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 yatatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliitaka Serikali ijielekeze tena katika Muundo, Maudhui, Malengo na Madhumuni ya Kifungu cha 8, 9 pamoja na 10 na 12 vya Muswada ili kujiridhisha hasa na nia ya dhamira ya Serikali yaani *Legislative Intent* katika marekebisho yanayokusudiwa.

Mheshimwa Mwenyekiti, kwa mfano katika Kifungu cha nane (8) cha Muswada ambacho kimsingi kinampa madaraka zaidi Rais kufuta hati miliki ya ardhi kwa mtu aliyevunja masharti ya Vifungu vipya vya 120A na 120B vya Sheria ya Ardhi chini ya Kifungu cha 45 cha Sheria mama. Kamati iliona kwamba hakuna haja kabisa ya kuongeza sababu mpya katika Kifungu hiki kwa kuwa sababu zilizotajwa katika Sheria mama kuhusu uwezo wa Rais kufuta hati miliki ya Ardhi kwa sababu za msingi na kwa maslahi ya umma

tayari zinajitosheleza, Kamati imeshauri kwamba Kifungu hicho kiondolewe.

Mheshimiwa Mwenyewe, katika Kifungu cha tisa (9) cha Muswada Kifungu kipya cha 120A Kamati ilihitaji kufahamu maana ya maneno *Local Bank* kama ilivyotumika katika muktadha wa Sheria hii na kama Benki za nje ya nchi zinaruhusiwa kutoa mkopo wa namna hiyo kwa kupokea hati za mali zilizowekwa rehani kwa sababu kifungu hiki ukikisoma kama kilivyo hakihitaji benki za nje yaani *Foreign Banks*, lakini pia hakizuii benki za nje kutoa mikopo kwa utaratibu unaotajwa.

Mheshimwa Mwenyewe, katika Kifungu kipya cha 120A(2), Kamati ilihitaji kufahamu tafsiri ya maneno *undeveloped* na *underdeveloped* kama yalivyotumika katika Sheria hii na upenyo ulioachwa Kisheria yaani *loophole* kwa mkopaji kutumia sehemu ya huo mkopo au mkopo wote kuendeleza ardhi iliyowekwa rehani. (*Makofi*)

Mheshimwa Mwenyewe, Kamati ilikubaliana na masharti ya Kifungu cha 120A(3) cha Muswada kilichotamka aliyeweka ardhi rehani kwa ajili ya kuombea mkopo yaani *Mortgager* kuwasilisha kwa Kamishna wa Ardhi taarifa ndani ya miezi sita kuhusu namna ambavyo fedha iliyopatikana kwa mkopo kwa kutumia ardhi iliyoweka wa rehani imetumika kuendeleza ardhi husika. Kamati inaamini kwamba Kifungu hiki kitaleta uwajibikaji kwa mkopaji na wakopaji wote na kitalinda ardhi ya Tanzania na kuifanya iendelezwe kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa kisheria na kiutaratibu.

Mheshimiwa Mwenyewe, katika Kifungu kipya cha 120B(1) ambacho kinatoa sharti la mkopaji kutumia fedha iliyopatikana na kuweka ardhi rehani kwa kuwekeza Tanzania. Kamati iliona kwamba kifungu hiki kinawabana wawekezaji wa Kitanzania ambao wana nia na uwezo wa kuwekeza nje ya mipaka ya Tanzania hasa kwa ukanda wa Kusini Kati na Mashariki mwa Afrika. Kamati ilishauri Serikali kuandika tena hiki kifungu ili kutoa fursa kwa Watanzania

wenye uwezo wa kuwekeza nje ya Tanzania kwa njia halali kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha 120B(2) Kamati ilijiridhisha kwamba kulikuwa na makosa makubwa ya kimaudhui ambayo kama yakiachwa yanaweza kuharibu maana iliokusudiwa yaani *intent* na ile *Mortgagor* yaani *borrower* ambalo limetumika katika Kifungu hiki limetumika kimakosa na badala yake neno halisi, sahihi ilipaswa kuwa *Mortgagee* yaani *lender* ndiyo neno sahihi iliyotakiwa kutumika ili kuleta tafsiri sahihi inayokusudiwa ambayo inatoa sharti kwa Taasisi za Fedha za Kibenki kuwasilisha kwa Kamishna wa Ardhi taarifa kwamba fedha iliyotolewa kwa ardhi iliyowekwa rehani imetumika katika uwekaji hapa Tanzania. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na kutumia neno *Mortgagee* katika Jedwali la Marekebisho ya Serikali iliyoandaliwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu kipya cha 120C ambacho kinatoa sababu ya kufutwa kwa Hati Miliki ya Ardhi endapo mmiliki ameshindwa kufuata masharti ya Kifungu kipya cha 120A na B cha Sheria ya Ardhi Kamati ilishauri Serikali kutazama kwa upana hatma ya Mabenki na Taasisi ya kifedha ambayo yalitumia Hati hizo katika dhamana. Endapo Hati hizo zitafutwa chini ya Kifungu hiki na endapo Sheria haitaweka utaratibu wa mabenki kurudishiwa fedha zao, basi benki na Taasisi za Kifedha zitapoteza fedha nyingi na pengine zikaacha kabisa kutoa mikopo kwa sababu ya kuogopa kupata hasara kubwa hasa katika muktadha wa Kifungu kinachopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya Tano, ya Muswada huu, iliruhusu marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 katika sehemu hii Kamati ilihitaji maelezo ya kina kutoka Serikalini ili kuelewa sababu za msingi za Serikali kupendekeza kuongeza umri wa hiari na wa lazima kwa wastaafu na Maprofesa Waadhiri Waandamizi kwa upande mmoja na Madaktari Bingwa kwa

upande mwingine kutoka miaka 55 hadi miaka 60 kwa hiari na kutoka miaka 60 mpaka miaka 65 kwa lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ya Serikali ilionekana kwamba kuna uhitaji mkubwa wa Waadhiri, Maprofesa na Madaktari Bingwa nchini na kwamba gharama ya kuwatumia Madaktari hawa kwa utaratibu wa kuwapa Mikataba ya miaka miwili miwili mara tu baada ya kustaafu ni kubwa kwa nchi na kwamba kama muda wa kustaafu ukiongezwa kwa kada hizi Serikali itaweza kuokoa mamilioni ya fedha yanayolipwa kwa mkupuo yaani *gratuity*. Wastaafu wa kada hizi ambao wapo kazini kwa Mikataba mifupi mifupi baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutafakari kwa kina hoja za Serikali na kusikiliza kwa umakini hoja za Wadau mbalimbali waliokuja kwenye Kamati na hasa Chama cha Madaktari Tanzania, Chama cha Madaktari wa Kinywa Tanzania pamoja na Jukwaa la Sera, Chama cha Mawakili Tanganyika na Chama cha Wataalam kutoka Chuo Kikuu (UDOM), Kamati iliona ni vema Serikali ikawashirikisha walengwa wa marekebisho haya kwa kina ili iweze kutunga Sheria inayokidhi maslahi ya walengwa wote katika upana wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uzito wa suala hili hata baada ya Kamati kumaliza vikao rasmi vya uchambuzi wa Muswada huu jitihada zimekuwa zikiendelea kati ya Kamati na Serikali katika kupata muafaka katika maudhui ya Kifungu hiki na hasa kwa kushirikisha walengwa wote wanaoguswa na Kifungu hiki na kwa kuzingatia maoni ya Wahadhiri na Madaktari vijana kwa upande mmoja na Maprofesa na Madaktari Bingwa wazee ambao wameshafika umri wa kustaafu wa miaka 60 na ambao wanaendelea kufanya kazi kwa Mikataba kwa upande mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Serikali tena tarehe 29 Januari, 2018 ili kupata maelezo ya kina kuhusu nia na malengo ya mapendekezo ya marekebisho ya Sheria

hii, uchambuzi wa kitakwimu kuhusu mapendekezo haya na namna jinsi ambavyo Serikali imejipanga kukabiliana na upungufu wa Maprofesa, Waadhiri kwa upande mmoja pamoja na Madaktari Bingwa kwa upande mwingine. Serikali ilitoa maelezo ya kina iliyoishawishi Kamati kwa hoja ya kukubaliana na marekebisho yanayopendekezwa na Serikali katika Kifungu kipyaa cha 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo hili la Serikali linafanana na umri wa kustaafu ulivyo katika nchi nyingine kwa kada za Maprofesa. Kwa mfano Maprofesa na Waadhiri Waandamizi wa nchi za Kenya wanastaafu Kisheria katika umri wa miaka 70. Halikadhalika Nigeria, Botswana pia miaka 70, pia Zimbabwe, Sudan miaka 65 na nchi kama Uingereza, Ujerumani na Marekani. Maprofesa hawana umri wa kustaafu. Ukomo wa Maprofesa kustaafu katika nchi hizi unapimwa na ujuzi, uwezo pamoja na ubobevu katika eneo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu kipyaa cha 25A(2)(b) Kamati ilishauri neno tamu liliotumika katika sentensi hii lifutwe, kwa sababu halina mantiki yoyote ya Kimuundo na mantiki na sentensi inayosomeka *after attaining the age of 65 years isomeke upon attaining the age of 65 years* ili kuleta maana iliyo bora kisarufi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haikuona haja ya kuwa na Kifungu kipyaa cha 25B katika Muswada huu ambacho kinampa Waziri wa Utumishi kwa kushirikiana na Rais mamlaka yaani *discretionary powers* kubadili umri wa kustaafu kwa Mtumishi wa Umma kama ataona ni sawa kufanya hivyo. Kwa maoni ya Kamati Kifungu hiki kinaweza kutumika vibaya na Waziri na hasa kwa sababu mfanyakazi husika hapewi nafasi ya kushirikishwa katika maamuzi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirejee Kamati haikuona haja ya kuwa na Kifungu kipyaa cha 25B katika Muswada huu ambacho kinampa Waziri wa Utumishi kwa kushirikiana na Rais Mamlaka yaani *discretionary powers* kubadili umri wa kustaafu kwa Watumishi wa Umma kama

ataona ni sawa kufanya hivyo kwa maoni ya Kamati Kifungu hiki kinaweza kutumika vibaya na Waziri husika na hasa kwa sababu mfanyakazi husika hapewi nafasi ya kushirikishwa katika kufanya maamuzi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Serikali kuafikiana na Kamati na kwamba Kifungu hiki kimefutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipewa nafasi ya kushiriki katika mchakato wa kupokea maoni ya Wadau waliofika kutoa maoni yao kuhusu maeneo mbalimbali ya Muswada kujadili na kuchambua hoja mbalimbali za Wadau wa Kamati kuhusu Muswada huu na kutolea ufafanuzi wa maelezo yanayohitaji ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 23 Januari, 2018, Mtoa hoja Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Waziri wa Ardhi walifika mbele ya Kamati kwa niaba ya Serikali kujibu hoja mbalimbali za Kamati kuhusiana na Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mengi ambayo Serikali ilikubali maoni na mapendekezo ya Kamati na kuyaweka kwenye Jedwali la Marekebisho kama ilivyowasilishwa na Mtoa hoja katika Bunge lako hili Tukufu Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Yapo maeneo mengi ambayo Serikali iliyatolea maelezo na Kamati kuelewa vema kabisa kuhusu nia ya Serikali katika Muswada huu. Niishukuru Serikali kwa kuwa sikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kamati na Serikali vilifikia muafaka katika maeneo mengi na hasa sababu za Serikali ya kuboresha maeneo yote yaliyokuwa na utata katika mapendekezo ya sheria hususani katika tafsiri ya maneno *Local Bank, undeveloped* na *underdeveloped Land* kama yalivyotumika katika muktadha wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza uchambuzi wa Kamati kwa kina na mchakato uliotumika



katika uchambuzi wa Muswada huu, naomba sasa nijielekeze katika maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na ushauri wa Kamati, utungwaji wa Kanuni husika kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria hii. Kifungu cha 120D cha Muswada kinasema kwamba utekelezaji wa Kifungu kipya cha 120A na 120B cha Muswada utafanyika kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa katika Kanuni. Uzoefu unaonesha kwamba, Taasisi nyingi za Serikali zimekuwa zinachelewa sana katika utengenezaji wa Kanuni hizi. Kamati inaiagiza Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kutengeneza kwa haraka Kanuni zote zinazogusa utekelezaji wa Sheria hii na hasa vifungu vipya vilivyohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa angalizo kwa Wizara ya Ardhi kwamba hata katika utengaji wa Kanuni Wadau wanaoguswa na kanuni hizo wana haki ya Kikatiba kushirikishwa katika utengenezaji wa Kanuni hizo na kwamba mchakato huo uwe ni shirikishi na ufanyike kwa wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikishwaji wa ujumla wa Wadau, katika kupokea na kuchambua maoni ya Wadau katika Muswada huu Kamati iligundua kwamba Wadau hawakushirikishwa kabisa katika mchakato wa marekebisho haya. Kama walishirikishwa basi kiwango cha ushirikishwaji wa Wadau kilikuwa kidogo sana. Kamati inazikumbusha Wizara na Taasisi zote za Serikali kwamba hata katika Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali suala la kuwashirikisha Wadau ni wajibu wa Kikatiba na Watunga Sera na Sheria za nchi chini ya Ibara ya 8(d) pamoja na Ibara 21(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uelewa mpana wa Sheria zinazofanyiwa marekebisho. Kwa kuwa Kamati ya Sheria na Katiba ina jukumu la kujadili na kuchambua Miswada mbalimbali ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali kisékta, kazi ya Kamati hii imekuwa ni mtambuka yaani *multi Sectoral*. Kwa muktadha huu ni vema Wizara na Taasisi zote zinazokusudia kufanya au kuleta mapendekezo ya marekebisho ya Sheria zote za kisékta kutoa mafunzo mahsusi

kwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria ili kujenga uelewa mpana wa Wajumbe kuhusu maeneo yanayokusudiwa kurekebishwa. Hii italetu urahisi kwa Wajumbe wa Kamati katika kujadili na kuchambua Muswada husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Sheria nyingine zinazogusa Sheria hii, marekebisho yanayofanyika katika Muswada huu na hasa yale yanayogusa Sheria ya Ardhi, Sura 113 yanaweza kuwa na athari katika utekelezaji wa Sheria nyingine za nchi katika sekta husika. Kwa mfano, katika Jedwali la Marekebisho linaloletwa na Serikali maana ya neno *Local Bank* limetafsiriwa kuwa na maana inayoelezwa katika Sheria ya Mabenki ya Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 pamoja na Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania mwaka 2006. Hata hivyo, katika Sheria hizo zote mbili tafsiri ya neno *Local Bank* haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri kwamba neno hili lipewe tafsiri ya kuandikwa kabisa yaani *express legal definition* katika Sheria tajwa au Sheria ya Ardhi ili kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo. Serikali itengeneze mikakati endelevu katika kutatua tatizo la upungufu wa Madaktari bingwa na Wahadhiri wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa Serikali kuongeza umri wa kustaafu kwa Maprofesa, Wahadhiri Waandamizi katika Vyuo Vikuu vya Madaktari Bingwa ni uamuzi wenye msingi na ni uamuzi wa Kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 13(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo inahusu Serikali kuchukua hatua za makusudi zenye lengo la kurekebisha matatizo mahsusi katika jamii yaani *affirmative actions*. Hata hivyo ili kukabiliana na pengo hili la ujuzi wa kada hizi yaani *skill gaps* Kamati inaishauri Serikali kuwa na mikakati endelevu wa kuhakikisha kwamba nchi haina pengo la Maprofesa, Wahadhiri Waandamizi na Madaktari Bingwa ili kuepusha kufanya marekebisho ya Sheria ya mara kwa mara ambayo inaweza kutoa tafsiri ya kibaguzi kwa kada nyingine za Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, Kwa mara nyingine tena naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kutoa kibali ili Kamati yangu ya Katiba na Sheria iweze kufanya uchambuzi wa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwatambue na kuwashukuru Wadau mbalimbali waliofika na kutoa maona na ushauri wao kwa Kamati ambao umesaidia kupatikana kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri iliyotukuka na waliyofanya katika uchambuzi wa Muswada huu ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali toka kuundwa kwa Kamati hii miaka miwili iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee Kamati inamshukuru sana aliyekuwa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillah kwa ushirikiano mkubwa aliutoa kwenye Kamati katika utumishi wake katika Bunge hili. Kamati yangu inamtakia utumishi mwema katika nafasi yake mpya ya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majina ya wajumbe wote walio Shiriki katika uchambuzi wa Muswada huu yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususani Katibu wa Bunge Ndugu Steven Kagaigai pamoja na uongozi, kwa uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati hii. Aidha, nimshukuru sana Mkurugenzi wa Idara za Kamati za Bunge Ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Angelina Sanga, Mkurugenzi wa Idara za Sheria, Ndg. Pius Mboya, Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge yaani Hansard Ndugu Hanifa Masaninga na Makatibu wote wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nimshukuru sana Katibu wetu wa Kamati Ndugu Danford Mpelumbe

ambaye alikuwa akifanya kazi usiku kucha kuhakikisha kwamba taarifa hii inakamilika kwa wakati, Ndugu Rehema Kipera, Ndugu Thomas Shawa, Msaidizi wa Kamati Ndugu Rahel Masima kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha kwamba taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.  
(Makofi)

**MWENYEKITI:** Asante Mheshimiwa Mwenyekiti Mchengerwa, tunakushukuru sana kwa taarifa yako ya Kamati yako.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA  
KATIBA NA SHERIA KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA  
MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI, (NA. 5) WA MWAKA  
2017, THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS)  
BILL, NO. 5 OF 2017 – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZENI**

---

## **1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Mheshimiwa Spika**, Kwanza kabisa napenda kutumia nafasi hii kumshukuru mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima hata kuweza kusoma Taarifa hii ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho mbalimbali, Na. 5 wa Mwaka 2017. Hii ni mara ya mwisho kufanya hivi katika kipindi cha takribani miaka miwili toka kuundwa kwa Kamati hii ya Katiba na Sheria ambayo Kikanuni imepewa jukumu kubwa sana la kujadili na kuchambua Miswada ya Sheria zote za Marekebisho ya Sheria mbalimbali kabla hazijasomwa Bungeni kwa mara ya pili na ya tatu na kupitishwa kuwa Sheria rasmi za nchi.

**1.2 Mheshimiwa Spika**, kwa sababu hii nakushukuru sana wewe mwenyewe, mheshimiwa naibu spika, wenyeviti wote wa Bunge na kwa upekee kabisa, wajumbe wote wa Kamati hii ya Katiba na Sheria ambao wamefanya kazi hii kubwa kwa kujitoa sana na kwa weledi wa hali ya juu katika

kuhakikisha kwamba Sheria zote za Marekebisho ya Sheria Mbalimbali zinazopitishwa na Bunge ili zinakua na ubora wa kimaudhui unaotakiwa na zinazokidhi matakwa ya Kikatiba, Kisheria, Kikanuni na Misingi mbalimbali ya Sheria za Kimataifa (International Law principles).

**1.3 Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa Mwaka 2017 [The Written Laws (Miscellaneous Amendment) (No.5) Act of 2017.

**1.4 Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016 Kamati ya Katiba na Sheria iliupokea Muswada huu Tarehe 17 Novemba, 2017 baada ya kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Tisa wa Bunge ili iufanyie kazi, na mnamo tarehe 17 Januari, 2018, Waziri wa Habari,Utamaduni,Sanaa na Michezo Dr. Harrison George Mwakyembe kwa niaba ya Mtoa Hoja ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria (Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi) pamoja na Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Mhe.William Lukuvi walifika mbele ya Kamati iliyoketi Dodoma na kutoa maelezo kuhusu Malengo na Madhumuni ya Muswada huu wenye lengo la kufanya marekebisho mbalimbali katika Sheria husika kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu ama kasoro zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo.

**1.5 Mheshimiwa Spika**, Sheria zinazokusudiwa kufanyiwa marekebisho katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

- (i) Sheria ya Ufilisi, (Sura ya 25);
- (ii) Sheria ya Bajeti (Sura ya 439),
- (iii) Sheria ya Ardhi (Sura ya 113),
- (iv) Sheria ya Utumishi wa Umma (Sura 238),

**1.6 Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 na kuzingatia matakwa ya Ibara ya Nane (d) na Ibara ya 21(2) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano inayowapa wananchi nafasi ya kushiriki katika masuala mbalimbali yanayowahusu, Kamati iliwaalika Wadau mbalimbali ili waweze kufika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu.

**1.7** Napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru kwa dhati Wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao katika Muswada huu. Naomba kutambua mchango wa Wadau wafuatao:-

- i) Chama cha Mwakili wa Tanganyika (TLS),
- ii) Chama cha Wanataaluma Chuo Kikuu UDOM (UDOMASA),
- iii) Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF),
- iv) Jukwaa la Sera (PF),
- v) Chama cha Wataalamu wa Sekta ya Benki Tanzania (TBA)
- vi) Chama cha Madaktari Tanzania (MAT)
- vi) Chama cha Madaktari wa Meno Tanzania (DAT)

## **2.0 MALENGO NA MADHUMUNI YA MUSWADA**

**Mheshimiwa Spika**, maelezo ya Jumla ya Muswada huu yapo katika taarifa ya Mtoa Hoja, Waziri wa Katiba na Sheria iliyosomwa leo hapa Bungeni pamoja na maelezo ya Malengo na Madhumuni ya Muswada yaliyomo kwenye Muswada kuanzia Ukurasa wa Saba mpaka wa Kumi na Moja na kwa faida ya muda naomba nisirudie tena maelezo haya na sehemu hii yote iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge.(Hansard)

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo ya utangulizi naomba sasa nijielekeze katika Uchambuzi wa Jumla wa Muswada katika sehemu ya Tatu ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria mbalimbali Nne ambazo ni Sheria ya Ufilisi, Sura ya 25, Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 na Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 238. Mapendekezo ya marekebisho haya yalitokana na mapungufu mbalimbali yaliyoonekana katika utekelezaji wa sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umegawanywa katika Sehemu Nne. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha, jina la Muswada na namna ambavyo Sheria zinazopendekezwa kurekebisha zitakavyorekebisha ndani ya Muswada huu.

Sehemu ya Kwanza inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 2 cha Sheria ya Ufilisi, Sura ya 25 kwa kupangilia mtiririko wa maneno ya kialphabeti katika kifungu cha 2 na kutoa tafsiri ya neno Mpokezi Mkuu kuwa na maana ya neno Kabidhi Wasii Mkuu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa shughuli zote za “Mpokezi Mkuu” zinafanywa na “Kabidhi Wasii Mkuu” ambaye anapendekezwa ateuliwe na Rais ili aweze kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na hili.

Sehemu ya Pili inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 21(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 kwa kuandika upya muda wa kuwasilisha Bungeni muongozo wa kuandaa mpango wa bajeti lengo la marekebisho hayo ni kuondoa mkinzano na kuoanisha na muda uliorejewa katika kanuni za Bunge, Kanuni ya 94(1) na (2) ya Kanuni hizo, toleo la Januari 2016.

Sehemu ya Tatu inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura 113 ambapo kifungu cha 45

kimerekebishwa kwa kuongeza masharti ya adhabu inayotokana na ukiukwaji wa masharti kwa mtu anayeweka dhamana ya milki ya ardhi.

Vifungu vya 120A, 120B na 120C navyo vimeongezwa ili kuwezesha fedha zinazopatikana kutokana na mkopo uliyotolewa kwa dhamana ya milki ya ardhi ya Tanzania zitumike kuendeleza sehemu au ardhi yote iliyowekwa rehani. Sharti hili litahusu milki ambazo hazijaendelezwa. Aidha, marekebisho haya pia yanakusudia kuweka wajibu kwa mkopaji na mkopeshaji kuwasilisha taarifa kwa Kamishna wa Ardhi kuhusu fedha zilizopatikana kutokana na dhamana ya milki ya ardhi zilivyowekezwa kwa ajili ya kuendeleza ardhi husika. Aidha, marekebisho haya yanalenga pia kuweka wajibu kwa fedha zinazokopeshwa kutokana na dhamana ya milki ya ardhi ya Tanzania ziweze kuwekezwa Tanzania.

Aidha, Benki na Taasisi za fedha za ndani na nje ya nchi nazo zinatakiwa kuwasilisha kwa Kamishna wa Ardhi tamko kwamba fedha inayotolewa kutokana na dhamana ya milki ya ardhi ya Tanzania zinawekezwa Tanzania. Kwa maudhui ya marekebisho haya, uwekaji rehani milki ya ardhi katika Benki au Taasisi ya Fedha za ndani au nje ya nchi ambapo fedha zimepatikana haitawekezwa Tanzania zitakuwa ni batili. Jambo jingine katika marekebisho haya ni kuwezesha kutungwa kwa kanuni za utekelezaji wa masharti ya fungu hili na kuhalalisha rehani za milki za ardhi zilizofanyika kabla ya marekebisho haya.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya Marekebisho kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 ambapo kifungu kipya cha 25A kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuweka kwenye Sheria masharti ya umri wa kustaafu kwa watumishi wa Umma, Masharti haya hayapo ndani ya Sheria kwa sasa. Aidha, mapendekezo ya kuongeza kifungu kipya yanalenga kuweka utaratibu mpya wa umri wa kustaafu kwa maprofesa na wahadhiri waandamizi wa vyuo vikuu vya umma na madaktari bingwa wa magonjwa ya binadamu wa hospitali za umma.



Mfumo huu mpya unalenga kuongeza umri wa kustaafu Utumishi wa umma kwa ridhaa kwa maprofesa na wahadhiri waandamizi wa vyuo vikuu vya umma na madaktari bingwa wa magonjwa ya binadamu wa hospitali za umma ili umri huo uweze kuwa ni miaka sitini kwa wale ambao wanastaafu kwa hiari na kwa wale ambao wanastaafu kwa lazima iwe ni miaka sitini na tano. Marekebisho haya yanalenga kutekeleza maamuzi ya Serikali yanayolenga kuongeza umri wa kustaafu kwa maprofesa, wahadhiri waandamizi wa madaktari bingwa wa binadamu kutoka vyuo vikuu vya umma na hospitali za umma. Kuongeza umri kwa kada hizi kutapunguza gharama kwa Serikali ya kuingia mikataba na wataalamu hawa mara tu wanapostaafu, na pia kutaongeza muda kwa wataalamu, wengine kuweza kulitumikia Taifa kwa muda mrefu zaidi na pia kusaidia kufundisha na kukuza wataalam wachanga walioko nchini.

### 3.0 UCHAMBUZI WA JUMLA WA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba Muswada huu unaonekana ni mfupi na usio na mambo mengi ukiutazama kwa haraka haraka, lazima nikiri kwamba huu ni mmoja kati ya Miswada ambayo Kamati yangu imetumia muda mwingi na umakini wa kutosha katika kuujadili na kuuchambua. Hii ni kwa sababu ya uzito wa mapendekezo ya Marekebisho ambayo serikali imekusudia kufanya katika Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 na Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 238.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua vifungu 12 vyote vya Muswada kwa kutazama usahihi wa kimaudhui, kisarufi na kimuundo wa kila kifungu kwa kulinganisha na malengo na madhumuni ya Muswada pamoja na Sheria mama zinazofanyiwa marekebisho. Kamati pia katika uchambuzi huu ilijiridhisha kama marekebisho yanayopendekezwa na Serikali yanaendana na Katiba ya Nchi, Sheria nyingine za nchi na matakwa ya Sheria na Mikataba ya Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maudhui ya Sheria kwa ujumla wake, kamati ilitazama mchakato mzima wa marekebisho ya Sheria hizi na hasa kama walengwa au watu wanaoguswa na marekebisho ya Sheria hizi walishirikishwa katika kiwango cha kutosha katika hatua za awali za marekebisho ya Sheria hizi kabla Muswada husika haujasomwa Bungeni kwa mara ya kwanza tarehe 17 Novemba, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya vifungu katika Muswada huu havikua na mjadala wowote katika Kamati kwa sababu ni vifungu vya utangulizi na vya muundo na visivyo na athari zozote katika maudhui ya msingi ya Muswada. Kwa mfano Kifungu cha 1,2,3,4,5,7 na cha 11.

**Mheshimiwa Spika**, Vifungu vilivyohitaji mjadala mpana kati ya Serikali na Kamati ni vifungu vya 8,9 na 10 vinahusiana na marekebisho ya Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 na Kifungu cha 12 kinachohusiana na Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 238.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Serikali katika Marekebisho yanayokusudiwa katika Sheria ya Ufilisi, Sura ya 25 na Marekebisho yanayokusudiwa katika Sheria ya Bajeti, Sura ya 439.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Kifungu cha 6 cha Muswada ambacho kinarekebisha Kifungu cha 21(2) cha Sheria ya Bajeti, kamati ilikubaliana na pendekezo la Serikali kuwasilisha Bungeni muongozo wa Mpango wa Bajeti mwezi Oktoba/Novemba badala ya Mwezi Februari kama ilivyo sasa katika Sheria ya Bajeti ili kuendana na muda uliotajwa katika Kanuni ya 94(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 ambayo inasema kwamba Muongozo wa Mpango wa Bajeti utawasilishwa Bungeni katika Bunge la Oktoba/Novemba.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo uzoefu umeonyesha kwamba katika mwaka wa uchaguzi wa Rais na wabunge;

na hasa Bunge jipya linapoanza, kipaumbele cha kwanza cha shughuli za Bunge siyo kujadili Muongozo wa Mapendekezo ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata na badala yake mapendekezo haya yamekua yanawasilishwa na kujadiliwa Bungeni katika Mkutano wa Bunge unaofuata. Kwa mantiki hii Kamati ilishauri Serikali iongeze Kifungu kitakachosomeka ifuatavyo;

*‘Notwithstanding the provisions of Sub section (2), the provisions of section 21 shall not apply during the election year’.* Kifungu hiki kittoa nafasi kwa Bunge kuendelea na Shughuli zenye kipaumbele cha kwanza wakati wa kuanza kwa Bunge jipya lolote mara tu baada ya uchaguzi ambapo masharti ya Kanuni ya 23 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 yatumika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliitaka Serikali ijielekeze tena katika muundo, maudhui, malengo na madhumuni ya Vifungu vya 8,9,10 na 12 vya Muswada ili kujiridhisha hasa na nia na dhamira ya Serikali (Legislative Intent) katika Marekebisho yanayokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mfano, Katika Kifungu cha Nane cha Muswada, ambacho kimsingi kinampa madaraka zaidi Rais kufuta hati miliki ya ardhi kwa mtu aliyevunja masharti ya Vifungu vipya vya 120A na 120B vya Sheria ya Ardhi, chini ya Kifungu cha 45 cha Sheria mama, Kamati iliona kwamba hakuna haja kabisa ya kuongeza sababu mpya katika Kifungu hiki kwa sababu sababu zilizotajwa katika Sheria mama kuhusu uwezo wa Rais kufuta hati miliki ya ardhi kwa sababu za msingi na kwa maslahi ya umma tayari zinajitosheleza. Kamati ilishauri kwamba Kifungu chote hiki kiondolewe.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Kifungu cha Tisa cha Muswada, Kifungu kipyua cha 120A Kamati ilihitaji kufahamu maana ya maneno ‘‘Local bank’’ kama yalivyotumika katika Muktaba wa Sheria hii na Kama benki za nje ya nchi zinaruhusiwa kutoa mikopo ya namna hiyo kwa kupokea hati za mali zilizowekwa rehani kwa sababu Kifungu hiki ukikisoma

kama kilivyo **hakitaji** benki za nje (Foreign banks) lakini pia hakizuii benki za nje kutoa mikopo kwa utaratibu unaotajwa.

**Mheshimwa Spika**, katika Kifungu kipya cha 120A (2) Kamati ilihitaji kufahamu tafsiri na maana ya neno "Undeveloped" na "Underdeveloped" kama yalivyotumika katika Sheria hii na upenyo ulioachwa Kisheria (Loophole) kwa mkopaji kutumia sehemu ya huo mkopo au mkopo wote kuendeleza ardhi iliyowekwa rehani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikubaliana na masharti ya Kifungu cha 120A (3) cha Muswada kinachomtaka aliyeweka ardhi rehani kwa ajili ya kuombea mkopo (Mortgagor) kuwasilisha kwa kamishna wa ardhi taarifa ndani ya miezi sita kuhusu namna ambavyo fedha iliyopatikana kwa mkopo kwa kutumia ardhi iliyowekwa rehani imetumika kuendeleza ardhi husika. Kamati inaamini kwamba kifungu hiki kitaleta uwajibikaji kwa wakopaji wote na itailinda ardhi ya Tanzania na kuifanya iendelezwe kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa kisheria na kitaratibu.

**Mheshimiwa Spika**, katika kifungu kipya cha 120B(1) ambacho kinatoa sharti kwa mkopwaji kutumia fedha iliyopatikana kwa kuweka ardhi rehani kwa kuwekeza Tanzania, Kamati iliona kwamba Kifungu hiki kinawabana wawekezaji wa Kitanzania ambao wana nia na uwezo wa kuwekeza nje ya mipaka ya Tanzania hasa katika ukanda wa kusini, kati na mashariki mwa Afrika. Kamati iliishauri Serikali kukiandika tena hiki kifungu ili kutoa fursa kwa Watanzania wenye uwezo wa kuwekeza nje ya Tanzania kwa njia halali kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Kifungu cha 120B (2) Kamati ilijiridhisha kwamba kulikuwa na makosa makubwa ya kimaudhui ambayo kama yakiachwa yanaweza kuharibu maana iliyokusudiwa (Intent). Neno "Mortgagor-borrower" ambalo limetumika katika Kifungu hiki limetumika Kimakosa na badala yake neno sahihi "Mortgagee-lender" ndio neno sahihi linalotakiwa kutumika ili kuleta tafsiri sahihi iliyokusudiwa ambayo inatoa sharti kwa taasisi za fedha au mabanki

kuwasilisha kwa kamishna wa ardhi taarifa kwamba fedha iliyotolewa kwa ardhi iliyowekwa rehani imetumika katika uwekezaji hapa Tanzania. Serikali ilikubaliana na ushauri wa Kamati na kutumia neno "Mortgagee" katika jedwali la Marekebisho ya Serikali lililoandaliwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, katika Kifungu kipya cha 120C ambacho kinatoa sababu ya kufutwa kwa hati miliki ya ardhi endapo mmiliki ameshindwa kufuata masharti ya Kifungu kipya cha 120A na 120B cha Sheria ya Ardhi, Kamati iliishauri Serikali kutazama kwa upana hatma ya mabenki na taasisi za fedha ambayo yalitumia hati hizo kama dhamana. Endapo hati hizo zitafutwa chini ya Kifungu hiki na endapo Sheria haitaweka utaratibu wa mabenki kurudisha fedha zao, basi benki na taasisi za fedha zitapoteza fedha nyingi na pengine zikaacha kabisa kutoa mikopo kwa sababu ya kuogopa kupata hasara hasa katika muktadha wa kifungu kinachopendekezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Tano ya Muswada huu ilihusu marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298. Katika sehemu hii Kamati ilihitaji maelezo ya Kina kutoka Serikalini ili kuelewa sababu za msingi za Serikali kupendekeza kuongeza umri wa hiari na wa lazima wa kustaafu kwa maprofesa na wahadhiri waandamizi kwa upande mmoja na kwa madaktari bingwa kwa upande mwingine kutoka miaka 55 mpaka 60 kwa hiyari na kutoka 60 mpaka 65 kwa lazima.

**Mheshimiwa Spika**, katika maelezo ya Serikali ilionekana kwamba kuna uhitaji mkubwa wa wahadhiri maprofesa na madaktari bingwa nchini na kwamba gharama ya kuwatumia madaktari hawa kwa utaratibu wa kuwapa mikataba ya miaka miwili miwili mara tu baada ya kustaafu ni kubwa kwa nchi na kwamba kama muda wa kustaafu ukiongezwa kwa kada hizi Serikali itaweza kuokoa mamilioni ya fedha yanayolipwa kwa mkupuo (*Gratuity*) kwa wastaafu wa kada hizi ambao wapo kazini kwa mikataba mifupi mifupi baada ya kustaafu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kutafakari kwa kina hoja za Serikali na kusikiliza kwa umakini hoja za wadau mbalimbali waliokuja kwenye Kamati, hasa chama cha madaktari Tanzania (MAT), Chama cha Madaktari wa Kinywa Tanzania (Dental Association of Tanzania), Jukwaa la Sera (Policy Forum), Chama cha Mwakili Tanzania (Tanganyika Law Society) na Chama cha Wanataaluma kutoka Chuo Kikuu UDOM (UDOMASA), Kamati iliona ni vema Serikali ikawashirikisha walengwa wa marekebisho haya kwa kina ili iweze kutunga Sheria inayokidhi maslahi ya walengwa wote katika upana wake.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uzito wa suala hili, hata baada ya Kamati kumaliza vikao rasmi vya uchambuzi wa Muswada huu jitihada zimekua zikiendelea kati ya Kamati na Serikali katika kupata mwafaka katika maudhui ya Kifungu hiki na hasa kwa kushirikiana na walengwa wote wanaoguswa na kifungu hiki na kwa kuzingatia maoni ya wahadhiri na madaktari vijana kwa upande mmoja na maprofesa na madaktari bingwa wazee ambao wameshafikia umri wa kustaafu wa miaka 60 na ambao wanaendelea kufanya kazi kwa mikataba kwa upande mwingine.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Serikali tena tarehe 29 Januari, 2018 ili kupata maelezo ya kina kuhusu nia na malengo ya mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria hii, uchambuzi wa Kitakwimu kuhusu mapendekezo haya na namna jinsi ambazo Serikali imejipanga kukabiliana na upungufu wa maprofesa/wahadhiri kwa upande mmoja pamoja na madakari Bingwa kwa upande mwingine. Serikali ilitoa maelezo ya kina yaliyoishawishi Kamati kwa hoja kukubaliana na marekebisho yanayopendekezwa na Serikali katika kifungu kipyua cha 12.

**Mheshimiwa Spika**, pendekezo hili la Serikali linafanana na umri wa kustaafu ulivyo katika nchi nyingine kwa kada ya maprofesa. Kwa mfano, maprofesa na wahadhiri waandamizi kwa nchi ya Kenya wanastaafu

Kisheria katika umri wa Miaka 70, Nigeria na Botswana ni miaka 70, Zimbabwe na Sudan ni miaka 65 na nchi kama Uingereza, Ujerumani na Marekani maprofesa hawana umri wa kustaafu. Ukomo wa maprofesa kustaafu katika nchi hizi unapimwa na ujuzi, uwezo na ubobevu katika eneo lake.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kifungu kipya cha 25A (2) (b) Kamati ilishauri neno "**the term**" lililotumika katika sentensi hii lifutwe kwa sababu halina mantiki yeyote ya kimuundo na kimantiki na sentensi inayosomeka "**after** attaining the age of sixty five years" isomeke "**Upon**" attaining the age of sixty five years" ili kuleta maana iliyo bora kisarufi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuona haja ya kuwa na Kifungu kipya cha 25B katika Muswada huu ambacho kinampa Waziri wa Utumishi, kwa kushirikiana na Rais, mamlaka (Discretionary powers) kubadili umri wa kustaafu kwa mtumshi wa Umma kama ataona ni sawa kufanya hivyo. Kwa maoni ya Kamati Kifungu hiki kinaweza kutumika vibaya na Waziri na hasa kwa sababu mfanyakazi husika hapewi nafasi ya kushirikishwa katika maamuzi haya.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilipewa nafasi ya kushiriki katika mchakato wa kupokea maoni ya wadau waliofika kutoa maoni yao kuhusu maeneo mbalimbali ya Muswada huu, kujadili na kuchambua hoja mbalimbali za wadau na Kamati kuhusu Muswada huu na kutolea ufafanuzi wa maeneo yaliyohitaji ufafanuzi zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 23 Januari, 2018 Mtoa hoja (Waziri wa Katiba na Sheria) pamoja na Waziri wa Ardhi walifika mbele ya Kamati kwa niaba ya Serikali kujibu hoja mbalimbali za Kamati kuhusiana na Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, yapo maeneo mengi ambayo Serikali ilikubali maoni na mapendekezo ya Kamati na kuyaweka kwenye Jedwali la marekebisho kama lilivyowasilishwa na Mtoa hoja katika Bunge lako tukufu. Yapo

maeneo mengine ambayo Serikali iliyatolea maelezo na Kamati kuelewa vema kuhusu nia ya Serikali katika Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati na Serikali vilifikia muafaka katika maeneo mengi na hasa kwa sababu Serikali iliyaboresha maeneo yote yaliyokua na utata katika mapendekezo ya Sheria hususani tafsiri ya maneno "**local bank**","**undeveloped land**" na "**underdeveloped land**" kama ilivyotumika katika muktadha wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuelezea uchambuzi wa Kamati kwa kina na mchakato uliotumika katika kuchambua Muswada huu, naomba sasa nijielekeze katika Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Muswada huu;

#### 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo Kamati inatoa maoni ya jumla ya kuzingatiwa kama ifuatavyo:-

##### 4.1 UTUNGWAJI WA KANUNI HUSIKA KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA SHERIA HII

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 120D cha Muswada kinasema kwamba utekelezaji wa Kifungu kipyua cha 120A na 120B cha Muswada utafanyika kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa katika Kanuni. Uzoefu unaonyesha kwamba Taasisi nyingi za Serikali zimekua zinachelewa sana katika utengenezaji wa Kanuni hizi. Kamati inaiagiza Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kutengeneza kwa haraka Kanuni zote zinazogusa utekelezaji wa Sheria hii na hasa vifungu vipya vilivyohusika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa angalizo kwa Wizara ya Ardhi kwamba hata katika utengenezaji wa Kanuni hizi wadau wanaoguswa na Kanuni hizo wana haki ya



Kikatiba kushirikishwa katika utengenezaji wa Kanuni hizo na kwamba mchakato huo uwe ni shirikishi na ufanyike kwa uwazi.

#### **4.2 USHIRIKISHWAJI WA UJUMLA WA WADAU**

**Mheshimiwa Spika**, katika kupokea na kuchambua maoni ya wadau katika Muswada huu, Kamati iligundua kwamba wadau hawakushirikishwa kabisa katika mchakato wa marekebisho haya na hata kama walishirikishwa, basi kiwango cha Ushirikishwaji wa wadau kilikua kidogo sana. Kamati inazikumbusha Wizara na Taasisi zote za Serikali kwamba hata katika Sheria za Marekebisho ya Sheria mbalimbali suala la kuwashirikisha wadau ni wajibu wa Kikatiba wa watunga sera na sheria za nchi chini ya Ibara ya 8(d) na Ibara ya 21(2) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

#### **4.3 UELEWA MPANA WA SHERIA ZINAZOFANYIWA MAREKEBISHO**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Kamati ya Sheria na Katiba ina jukumu la kujadili na kuchambua Miswada mbalimbali ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali za Kisekta, kazi ya Kamati hii imekua ni mtambuka (Multi-sectoral).Kwa muktadha huu ni vema Wizara na Taasisi zote zinazokusudia kuleta mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria zao za Kisekta kutoa mafunzo mahsusi kwa wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria ili kujenga uelewa mpana wa wajumbe kuhusu maeneo yanayokusudiwa kurekebishwa. Hii italetu urahisi kwa wajumbe wa Kamati hii katika kujadili na kuchambua Muswada husika.

#### **4.4 MAPITIO YA SHERIA NYINGINE YANAYOGUSWA NA SHERIA HII**

**Mheshimiwa Spika**, marekebisho yaliyofanyika katika Muswada huu na hasa yale yanayogusa Sheria ya Ardhi, Sura

ya 113 yanaweza kuwa na athari katika utekelezaji wa Sheria nyingine za nchi katika sekta husika. Kwa mfano, katika Jedwali la Marekebisho lililoletwa na Serikali maana ya neno "Local bank" limetafsiriwa kuwa na maana iliyoielezwa katika Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006 Pamoja na Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006. Hata hivyo katika Sheria zote hizi mbili tafsiri ya neno "Local bank" haipo. Kamati inashauri kwamba neno hili lipewe tafsiri ya kuandikwa kabisa "Express legal definition" katika Sheria tajwa au Sheria ya Ardhi ili kuondoa mkanganyiko unaoweza kujitokeza katika utekelezaji wa Sheria hii.

#### 4.5 SERIKALI ITENGENZE MKAKATI ENDELEU KUTATUA TATIZO LA UPUNGUFU WA MADAKTARI BINGWA NA WAHADHIRI WA VYUO VIKUU

**Mheshimiwa Spika**, uamuzi wa Serikali kuongeza umri wa kustaafu kwa maprofesa/wahadhiri waandamizi katika vyuo vikuu na madaktari Bingwa ni uamuzi wenye msingi wa Kikatiba katika Ibara ya 13(5) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ambayo inairuhusu

*"...Serikali kuchukua hatua za makusudi zenye lengo la kurekebisha matatizo mahususi katika jamii" (Affirmative Actions)*. Hata hivyo, ili kukabiliana na pengo hili la ujuzi kwa kada hizi (Skills gap) kamati inaishauri Serikali kuwa na mkakati endelevu wa kuhakikisha kwamba nchi haina pengo la maprofesa, wahadhiri waandamizi na madaktari Bingwa ili kuepusha kufanya marekebisho ya Sheria ya mara kwa mara ambayo yanaweza kutoa tafsiri ya kibaguzi kwa kada nyingine za utumishi wa umma.

#### 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana wewe kwa kutoa kibali ili Kamati ya Katiba na Sheria iweze kuufanyia uchambuzi Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba niwatambue na kuwashukuru Wadau mbalimbali waliofika na kutoa maoni na ushauri wao kwa Kamati ambao umesaidia kupatikana kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri na kutukuka waliyofanya katika Uchambuzi wa Miswada ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali toka kuundwa kwa Kamati hii miaka miwili iliyopita.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee Kamati inamshukuru sana aliyekua Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kashiilah kwa ushirikiano mkubwa aliutoa kwenye Kamati katika utumishi wake katika Bunge hili na inamtakia Utumishi mwema katika nafasi yake mpya ya naibu katibu mkuu Wizara ya Kilimo.

**Naomba Majina ya Wajumbe walioshiriki kwenye uchambuzi wa Muswada huu yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD).**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb- M/Mwenyekiti
3. Mhe Ally Saleh Ally, Mb –Mjumbe
4. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb –Mjumbe
5. Mhe Taska Restituta Mbogo, Mb –Mjumbe
6. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb –Mjumbe
7. Mhe. Seif Ungando Ally, Mb- Mjumbe
8. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb- Mjumbe
9. Mhe. George Simbachawene, Mb –Mjumbe
10. Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb-Mjumbe
11. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb –Mjumbe
12. Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb- Mjumbe
13. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb- Mjumbe
14. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb –Mjumbe
15. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb- Mjumbe

16. Mhe. Joram Ismail Hongoli, Mb- Mjumbe
17. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb –Mjumbe
18. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb –Mjumbe
19. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb –Mjumbe
20. Mhe. Selemani Zedi, Mb –Mjumbe
21. Mhe. Juma Kombo Hamad, Mb –Mjumbe
22. Mhe. Zainab Mndolwa, Mb-Mjumbe
23. Mhe. Ussi Pondezza, Mb-Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge hususani Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa Uongozi thabiti ambao umerahisisha utendaji kazi wa Kamati. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Mkurugenzi wa Idara ya Sheria ya Bunge Ndg. Pius Mboya, Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) Ndg. Hanifa Masaninga Makatibu Kamati waliofanikisha kazi hii ambao ni Ndg. Dunford Mpelumbe, Ndg. Rehema Kipera, Ndg. Thomas Shawa na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**

**KATIBA NA SHERIA**

**30 JANUARI 2018**

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Taarifa Mheshimiwa Ali Salehe, karibu. Karibu sana Mheshimiwa.

**MHE. ALLY SALEHE ALLY – (K.n.y. MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WIZARA YA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 5 ya mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara ya kwanza nawasilisha maoni ya Kambi rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada uliopo mezani kwa mwaka huu mpya 2018, naomba kutumia fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote kuuona mwaka huu mpya tukiwa salama. Kwa jinsi hiyo nawatakia nyote Heri ya Mwaka Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati sisi tunafurahia kuuona mwaka huu mpya tukiwa salama Msemaji Mkuu wa Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Tundu Lissu ambaye kwa hakika ndiye aliyetakiwa kutoa maoni haya leo hii, mwaka huu mpya umemkuta hospitalini akipatiwa matibabu baada ya kujeruhiwa vibaya kwa risasi katika jaribio lililoshindwa la kutaka kuondoa uhai wake, jaribio lililofanywa na watu ambao mpaka leo hawajulikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si nia yangu kurudia historia ya matukio mabaya ya kihalifu dhidi ya binadamu yaliyotokea katika nchi yetu bila Serikali kuchukua hatua zozote, ila ni nia yangu kusema kwamba hakuna jambo lililostirika au lililofanywa sirini ambalo halitadhihirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali hii ya CCM kuendelea kukaidi kufanyia kazi ushauri wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa kuunda Tume huru ya Kimahakama kuchunguza vifo vyenye utata na matukio mengine ya...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, nisaidie tu, umeanza vizuri sana nilikuwa nakushauri sasa hotuba yako ukurasa wa kwanza. Nitakutunzia muda wako tu usiwe na shida.

Kwenye maoni yetu ya Kambi ningependa tutumie lugha za Kibunge na ndio Kanuni hizi, ukienda hivyo umefika nilikuwa naangalia *paragraph* ya kwanza, kwenye utangulizi tuko pamoja? *Paragraph* ya kwanza, ya pili, *paragraph* ya tatu. Ulianza sasa kusoma Serikali hii ya CCM ni Serikali ya CCM ndio! Sasa yale yanayofuata nilikuwa nakushauri na hapa sasa nasema sio kukushauri naagiza tu tuyaondoe ili sasa tujielekeze katika uchambuzi wa Muswada ulioletwa mbele ya Bunge kupitia sasa taarifa ya Kamati. Kwa hiyo, Sheria zinazofanyiwa marekebisho ndio uendelee sasa kwenye mtiririko wako. Endelea Mheshimiwa.

**MHE. ALLY SALEHE ALLY – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa kile ambacho umesema tukitoe ndio kile ambacho tunaamini na ndio kile Kambi ya Upinzani inachokisimamia naomba kwamba taarifa yangu ipokelewe kama ilivyo kwa sababu Wabunge wote wanayo na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante! Tunaendelea. Sehemu hiyo haitaingia haitakuwa sehemu ya Hansard.

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, KUHUSU  
MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA  
MBALIMBALI NA. 5 WA MWAKA 2017 KAMA  
ULIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni,

kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 ya Mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa ni mara ya kwanza nawasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada uliopo mezani kwa mwaka huu mpya wa 2018, naomba kutumia fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujali sote kuuona mwaka huu mpya tukiwa salama. Kwa jinsi hiyo, nawatakia nyote heri ya Mwaka Mpya.

**Mheshimiwa Spika**, wakati sisi tunafurahia kuuona mwaka huu mpya tukiwa salama; Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu (Mb) ambaye kwa hakika ndiye aliyetakiwa kutoa maoni haya leo hii, mwaka huu mpya umemkuta hospitalini akipatiwa matibabu baada ya kujeruhiwa vibaya kwa risasi katika jaribio lililoshindwa la kutaka kuuondoa uhai wake – jaribio lililofanywa na watu ambao mpaka leo hawajullikani.

**Mheshimiwa Spika**, si nia yangu kurudia historia ya matukio mabaya ya kihalifu dhidi ya binadamu yaliyotokea katika nchi yetu bila Serikali kuchukua hatua zozote; ila ni nia yangu kusema kwamba hakuna jambo lililositirika au linalofanywa sirini ambalo halitadhihirika.

#### **[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**Mheshimiwa Spika**, kabla sijatoa maoni ya Kambi kuhusu Muswada uliopo mezani, napenda pia kuchukua nafasi hii kukitakia chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa niaba ya UKAWA ushindi mkubwa katika chaguzi za marudio za ubunge katika majimbo ya Siha na Kinondoni. Napenda kuwaasa wananchi wa majimbo hayo kutumia tathmini ya hali yao ya maisha tangu Serikali hii ya CCM iingie madarakani na kufanya uamuzi sahihi katika uchaguzi huo. Pia wawachunguze kwa makini wawakilishi wao wa awali, waliowapa ridhaa ya kuwawakisha kupitia tiketi za vyama fulani ambao wamewageuka na kuchukua tiketi za vyama

vingine na kuwapima kama bado wanafaa kuendelea kuwa wawakilishi wao.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nitoe maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 5 ya Mwaka 2017.

## 2. SHERIA ZINAZOFANYIWA MAREKEBISHO

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 5 ya Mwaka 2017 ukiwa na sheria kadhaa zinazotakiwa kufanyiwa marekebisho. Sheria hizo ni Sheria ya Ufilisi sura ya 25 ya Sheria za Tanzania, Sheria ya Bajeti Sura ya 439, Sheria ya Ardhi Sura ya 113 na Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298.

## 4. UCHAMBUZI NA MAONI YA YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA BAADHI YA SHERIA ZINAZOFANYIWA MAREKEBISHO

### 4.1. Sheria ya Bajeti Sura ya 439

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya pili ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 21(2) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 kwa kuandika upya muda wa kuwasilisha Bungeni muongozo wa kuandaa mpango wa bajeti. Lengo la Marekebisho hayo ni kuondoa mkinzano na kuoanisha na muda uliorejewa katika kanuni za Bunge Kanuni ya 94(1) na (2) ya Kanuni hizo toleo la 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imefarijika kuona kwamba Serikali hatimaye imepokea na kutekeleza ushauri wa uliotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa kuondoa mgongano wa sheria ya Bajeti na Kanuni za Bunge kuhusu uwasilishwaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo.



**Mheshimiwa Spika**, wakati akiwasilisha hotuba yake kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa sana Halima James Mdee (Mb) alisema kwamba; naomba kunukuu: "....."kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa Katiba, Sheria na hata Kanuni za Bunge katika uwasilishaji wa Mapendekezo ya Mipango ya Maendeleo ya Taifa jambo ambalo limechangia kwa kiasi kikubwa utekelezaji hafifu wa Mipango hiyo. Alisema kwamba; wakati Kanuni ya 94(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inaelekeza kwamba Bunge litakaa kama Kamati ya Mipango katika mkutano wake wa mwezi Oktoba – Novemba kila mwaka ili kujadili na kuishauri Serikali kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata; kifungu cha 21(2) cha Sheria ya bajeti ya mwaka 2015 kinaelekeza kwamba mapendekezo ya Mpango pamoja na makisio ya bajeti yatawasilishwa katika mkutano wa Bunge wa mwezi Februari kila mwaka au kama Bunge halipo kwenye mkutano katika mwezi wa februari basi katika wiki ya kwanza ya mkutano huo utakapoitishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Mdee alibainisha kuwa huo ulikuwa ni mgongano wa wazi kati ya Kanuni za Bunge na Sheria ya bajeti kuhusu uwasilishwaji wa Mpango na makisio ya bajeti katika mwaka wa fedha unaofuata. Kutokana na mgongano huo wa Kanuni za Bunge na Sheria ya bajeti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitoa wito kwa Mheshimiwa Spika, kuiagiza Kamati ya Kanuni kufanya marekebisho ya Kanuni ya 94(1) ili izingatie matakwa ya kifungu cha 21 (2) cha Sheria ya bajeti ya 2015 kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge kwa manufaa ya wananchi"

**Mheshimiwa Spika**, Ni bahati nzuri kwamba kabla spika hajachukua hatua hiyo, Serikali imekuwa pro-active kwa kuleta marekebisho ya sheria ya bajeti ili kuondoa mgnongano huo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inapaswa kuona kuwa ushauri unaotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni mzuri na si vibaya kuutambua inapoufanyia kazi.

#### 4.2. Sheria ya Adhi Sura ya 113

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya tatu ya muswada inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999 sura ya 113 ikiwa na lengo la kuweka utaratibu na adhabu kuhusu utaratibu wa namna ya kutumia ardhi kama rehani kwa ajili ya kupata mikopo ya kibiashara. Ibara ya 9 ya muswada inaongeza vifungu vipya vya 120 A, 120 B, 120 C na 120 D.

**Mheshimiwa Spika**, ukiangalia lengo la marekebisho haya kwa haraka utaona kuna nia njema ndani yake kwa sababu kwa muda mrefu Kambi Rasmi ya Upinzani tumepiga kelele kuhusu changamoto zilizopo nchini kwenye masuala ya uwekezaji ikiwemo katika sekta ya ardhi.

**Mheshimiwa Spika**, mwaka 2012 wakati wa Bunge la kumi, Mheshimiwa Halima James Mdee (Mb) aliwasilisha hoja binafsi kuhusu umuhimu wa serikali kufanya ukaguzi na tathmini kwenye uwekezaji katika mashamba makubwa nchini ili kama Taifa tuweze kujua mwelekeo wetu kuhusu uwepo wa ardhi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi; moja ya changamoto ambayo ilielezwa wakati huo ni uwepo wa tabia miongoni mwa wawekezaji kutumia ardhi na mali zingine walizopewa kwa ajili ya uwekezaji kama rehani na kupata mikopo ya kibiashara na kuwekeza katika biashara tofauti na zile ambazo waliahidi kufanya wakati wa kuingia makubaliano na serikali.

**Mheshimiwa Spika**, ilifikia hatua wawekezaji wengine kuchukua mikopo ya ndani na kuwekeza kwenye biashara zingine nje ya Tanzania, jambo hili lilipigiwa kelele lakini Serikali iliweka pamba masikioni mpaka sasa.

**Mheshimiwa Spika**, mapendekezo ya muswada huu hayaondoi changamoto hiyo kwa sababu imeweka utaratibu ambao ukisoma kwa makini ni kukurupuka na sio kufanya tathmini na ushirikishwaji wa wadau kutatua changamoto hiyo. Hii ni kutokana na masuala yafuatayo ambayo yanapendekezwa katika muswada huu;

**Mheshimiwa Spika**, serikali inaweka masharti kwenye ibara ya 9 ya muswada kuwa fedha za mkopo uliopatikana kutokana na ardhi iliyokwa rehani ambayo haijaendelezwa itumike kuendeleza sehemu au ardhi hiyo. Hapa kuna haja ya kuhoji ukubwa wa sehemu hiyo ya ardhi na namna ya kuiendeleza. Aidha ijulikane pia kuwa kukopa kwa kutumia rehani ya ardhi itategemea na malengo ya mkopo na mpango wa biashara ya mwekezaji na sio kumlazimisha kuwekeza sehemu ambayo haitakuwa na tija kwake.

**Mheshimiwa Spika**, masharti haya inabidi yawekwe katika sura ambayo haitaumiza pia wawekezaji wa ndani ambao hutumia ardhi kama sehemu ya kupata fedha kwa ajili ya kuendeleza biashara yao tofauti na kwenye ardhi husika.

**Mheshimiwa Spika**, aidha ni vema serikali ikaweka ufafanuzi wa maana ya benki za ndani ili kuweka sawa mkanganyiko ambao unaweza kujitokeza huko baadae wakati wa utekelezaji wa Sheria hii. Suala la msingi ni kuwa mitaji mikubwa ya uwekezaji haitoki ndani ya nchi, kama mnajinasibu kuwa serikali ya viwanda msitegemee wawekezaji wakubwa wa viwanda vikubwa kupata mikopo kwenye hizi benki zenu ambao nyingi zinapumulia mashine na nyingine mmezitangaza mufilisi.

**Mheshimiwa Spika**, aidha uhalisia uliopo kwa sasa ni kuwa Benki hawatoi mikopo kwa ardhi ambayo haijaendelezwa. Wataalam wa Benki wanaohusika na mikopo ya biashara wanakataa kutoa mikopo kwa wawekezaji au wajasiriamali wakubwa ambao hawajaendeleza ardhi zao. Pendekezo hili la Serikali halijazingatia utaratibu uliopo, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza Serikali kupitia upya pendekezo hili kwa mujibu wa hali halisi. Masharti ya Sheria yanaweza

yakawa yanaruhusu rehani kuwekwa kwenye ardhi ambayo haijaendelezwa lakini uhalisia katika masuala biashara na namna benki watakvoyoweza kulipwa mikopo yao ni tofauti na fikra na mtazamo wa Serikali na Sheria zilizopo.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu kipya cha 120 D kinachopendekezwa kinatoa masharti ya jumla kuwa utaratibu na masharti ya utekelezaji wa vifungu vipya vinavyopendekezwa na muswada huu utafafanuliwa kwenye Kanuni, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha masuala ya msingi yanawekwa kwenye Sheria na sio kujificha katika Kanuni ambazo zitatungwa na Serikali baadae.

### 4.3. Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya nne ya Muswada huu inapendekeza kufanya marekebisho kwenye sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 ambapo kifungu kipya cha 25A Kinapendekezwa kuongezwa kwa lengo la kuweka kwenye sheria masharti ya umri wa kustaafu kwa watumishi wa umma. Kifungu hicho kinaongeza umri wa kustaafu kwa maprofesa na wahadhiri waandamizi wa vyuo vikuu vya umma na madaktari bingwa wa magonjwa ya binadamu wa hospitali za umma ili umri huo uweze kuwa miaka sitini kwa wale wanaostaafu kwa hiari na kwa wale wanaostaafu kwa lazima iwe ni miaka sitini na tano.

**Mheshimiwa Spika**, sababu kubwa inayotolewa na Serikali kuhusu kuongeza umri wa kustaafu kwa kada tajwa, ni kupunguza gharama kwa Serikali ya kuingia mikataba na wataalamu hawa mara tu wanapostaafu na pia kuongeza muda kwa wataalamu wengine kuweza kutumikia Taifa kwa muda mrefu zaidi na pia kusaidia kufundisha na kukuza wataalamu wachanga walioko chini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa sana na sababu dhaifu zinazotolewa na Serikali kama kigezo cha kuongeza umri wa kustaafu kwa kada zilizotajwa. Tafiti zilishafanyika na zikabaini kwamba mtu anapofikia umri wa miaka sitini uwezo wake wa kufikiri na

kufanya kazi unaanza kupungua. Hali kadhalika nguvu za mwili hupungua pia. Ni kipindi ambacho hata magonjwa mbalimbali huwashambulia sana watu wenye umri huo na kuendelea.

**Mheshimiwa Spika**, ni tafiti hizo hizo zilizofanya sheria ya utumishi wa umma iweke ukomo wa umri wa kufanya kazi kuwa miaka 55 kwa hiari na miaka 60 kwa lazima. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, hivi wale waliotunga sheria ya utumishi wa umma iliyoweka ukomo huo wa mika 55 kwa 60 wamebadili mtazamo, au wamekufa wakaja wengine wenye mtazamo mpya au kuna utafiti mwingine uliogundua kuwa kadiri mtu anavyozidi kuzeeka ndivyo nguvu zake, uwezo wake wa kufikiri na kufanya kazi unavyozidi kuongezeka?.

**Mheshimiwa Spika**, waingereza wana usemi usemao *“cheap is always expensive”* Ni jambo lisilo na tija kiuchumi kukwepa gharama ndogo sasa na hatimaye kuja kuliingiza taifa kwenye hasara kubwa itakayosabishwa na watendaji ambao weledi na ufanisi wao tayari umefikia ukomo na unaanza kupungua. Ipi ni gharama kubwa; kumpatia daktari bingwa mmoja mkataba utakaoinisha kazi anayotakiwa kufanya kwa kipindi cha mwaka mmoja au kulipa fidia ya vifo vitakavyosababishwa na daktari huyo kutokana na uwezo wake wa kufanya kazi kupungua? Au ipi ni gharama kubwa; kumpatia mkataba wa mwaka mmoja profesa wa chuo kikuu aliyestaafu au kulipia uharibifu mkubwa utaofanywa na vijana waliofundishwa visivyo na profesa huyo kutokana na uwezo wake wa akili kupungua.

**Mheshimiwa Spika**, ulimwengu wa sayansi na teknoojia unakuwa kwa kasi sana. Kila siku kuna teknolojia mpya na kila siku yanahitajika maarifa mapya ili kuweza kumudu teknolojia mpya. Kwa sababu hiyo, wataalamu wetu wana changamoto ya kujifunza kila mara ili kuweza kukabiliana na changamoto mpya zinazotokana na teknolojia mpya. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, hawa wazee wetu waliofikia ukomo wa kulitumikia taifa ambao tunataka kuwaongezea muda watakuwa na uwezo wa kukaa tena darasani kujifunza mbinu

mpya zinazotokana na mabadiliko ya teknolojia? Au watakuwa wanafanya kazi kwa uzoefu?

**Mheshimiwa Spika**, hoja hii ya kuongeza umri wa kustaafu, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haina mashiko yoyote. Yamkini ni hoja ya watu wachache wavivu na wasio na mawazo mapana ya kujitegemea na wanataka maisha yao yakome wakiwa kazini ili wasipate shida ya kutafuta maisha baada ya kustaafu.

**Mheshimiwa Spika**, wastaafu wengi wanaojishughulisha na kazi za ujasiriamali baada ya kustaafu wameanza kubaini kwamba walipoteza muda mwingi kukaa katika ajira rasmi na wangetamani kama wangestaafu mapema zaidi kwa kuwa wameona mafanikio makubwa katika kujajiri.

**Mheshimiwa Spika**, hili linadhihirishwa pia na maoni ya wadau ambao wengi wao hawakufurahishwa na hoja hii ya kuongeza umri wa kustaafu. Mdau mmoja aliyewakilisha chama cha madaktari bingwa; alisema bayana kwamba; daktari wa upasuaji ambaye ameshafikia umri wa miaka sitini ambaye kwa sasa anatakiwa kuongezewa muda wa kustaafu hadi miaka sitini na tano hawezi kufanya upasuaji kwa ufanisi na kwa muda unaotakiwa kama ambavyo anageweza kufanya akiwa na mika 40 mpaa 50. Alisema kuwa umakini wake umepungua, nguvu zake za mwili zimepungua, uoni wake ni hafifu, uharaka wake wa kufanya upasuaji nao umepungua. Hivyo kumruhusu mzee huyu kuendelea kufanya kazi ya upasuaji ni kusababisha hatari kubwa kwa mgonjwa ikiwa ni pamoja na kupoteza maisha.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, hivi kama hawa maprofesa na madaktari bingwa tunaowapigia upatu wa kuongeza umri wao wa kustaafu wao wenyewe wamepinga hoja hiyo, Serikali inalazimisha hoja hii kwa maslahi ya nani?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri na kupendekeza kufuta kabisa kifungu kipya cha 25 kinachopendekeza kuongeza umri wa kustaafu. Aidha, Kambi

Rasmi ya Upinzani inakusudia kuleta jedwali la marekebisho ili kufuta kifungu hicho.

## 5. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, sheria bora ni ile inayogusa makundi yote ya jamii. Sheria inayobagua baadhi ya makundi na kada katika jamii ni sheria mbaya. Nimesema hivyo, kwa kufanya rejea ya marekebisho ya sheria ya utumishi wa umma ambayo imefanya ubaguzi wa baadhi ya kada kwa kuzingeeza umri wa kustaafu na nyingine kubaki katika umri wa zamani. Jambo hili halina afya sana katika utekelezaji bora wa sheria. Hata hivyo sababu zilizotolewa nazo hazikidhi haja ya kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani pia inaishauri Serikali kutambua mchango wa Upinzani pale inapotekeleza mapendekezo na ushauri mzuri unaotolewa na Kambi ya Upinzani kwa kuwa upinzani una nia njema ya kuona Tanzania Mpya ya mifumo bora ya sheria. Narudia kusema kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani imefarijika kuona mapendekezo yake ya muda mrefu ya kuondoa mgongano uliokuwepo kati ya sheria ya bajeti na kanuni za Bunge ukifanyiwa kazi na Serikali. Lipo moja tu, ambalo Kambi ya Upinzani imekuwa ikilipigia kelele ambalo mpaka sasa halijatekelezwa nalo ni kutunga sheria ya kusimamia mipango ya maendeleo kwa mujibu wa ibara ya 63(3) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni matumaini yetu tutaona hilo likitekelezwa kwa mwaka mpya wa fedha 2018/19.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

Ally Saleh Ally (Mb)  
Kny: **MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI**  
**BUNGENI KATIKA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**  
30 Januari, 2018

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tunaendelea. Katika orodha ambayo ninayo hapa, naangalia muda. Nadhani tungeweza kufanya vizuri sana tumalize, lakini naona ngumu. Wachangiaji ni dakika 15 lakini sio lazima, mnaweza mkagawana gawana kama hoja imethibiti imeeleweka. Nianze na Mheshimiwa Joseph Mhagama atafuatiwa na Mheshimiwa Najma Giga. Tuanze na hawa wawili tuone tunakwendaje. Mheshimiwa Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa hii nafasi. Pili nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuwa mmoja katika wachangiaji wa kwanza kabisa wa Muswada huu muhimu sana wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia kwa makini sana mawasilisho yaliyofanywa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pia na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria. Pia nimebahatika kusoma mambo mbalimbali ili nione namna gani naweza nikaishauri Serikali kwenye jambo hili mahususi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niipongeze sana Serikali yetu ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli. Ukisoma Muswada huu unapata picha iliyo dhahiri kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga vizuri sana kurudisha rasilimali za Watanzania mikononi mwa Watanzania na kuwajenga Watanzania kiuchumi. Sheria ya Ardhi, Sura namba 113 marekebisho yaliyoletwa hapa yanalenga kwenda kulinda rasilimali ardhi ambayo kwa sehemu kubwa imetumika vibaya sana na watu wasioitakia mema Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Sheria hii sitachambua maeneo mengi kwa sababu nataka nijikite kwenye eneo lingine, lakini niwashawishi Waheshimiwa Wabunge tuiptishe kama ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo nataka kwa muda mfupi niliopewa nijikite zaidi ni kwenye hii Sheria ya



Utumishi wa Umma, Sura 298. Ukisikiliza mawasilisho yaliyofanywa unapata picha dhahiri kwamba katika kipindi fulani tulijisahau kidogo kuweka ajira za kutosha kwenye eneo hili mahususi kabisa linalogusa Wahadhiri wa Vyuo Vikuu lakini na Madaktari. Matokeo yake leo tuna upungufu mkubwa sana wa kada hiyo. Kati ya mwaka 2012 mpaka 2015 watumishi katika kada hiyo waliofikia umri wa kustaafu walifika 395. Katika kipindi hicho hicho Serikali ililazimika kuingia mkataba na watumishi hao hao waliostaafu na kufikia idadi ya 324.

Sasa unapata picha kwamba waliofikia umri wa kustaafu 395 wanaoombwa kurudi kuendelea na majukumu 324 sawa sawa na asilimia 82. Sasa huu ni ushahidi kwamba kada hiyo ina upungufu mkubwa sana wa watu. Sasa Serikali imechukua hatua hiyo kwa muda mrefu, imeendelea kuwa-*retain* wale waliostaafu kwa asilimia 82.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara yake ni matumizi makubwa ya fedha za Serikali, hawa watumishi wanapostaafu wanalipwa mafao yao yote, wanapewa stahiki zao zote ikiwemo kiinua mgongo. Tunapowaomba sasa warudi kazini kuendelea na kazi tuna-*negotiate* upya mikataba na masharti yanakuwa mapya wakati mwingine, na gharama pengine zinakuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi wanapomaliza kipindi, kila kipindi cha miaka miwili kinapoisha sasa Serikali inalazimika kuwalipa tena *gratuity* ambayo kimsingi ni kubwa sana. Ukisoma katika makabrasha mbalimbali katika kipindi cha miaka miwili tu Serikali imetumia zaidi ya bilioni 2.9. Sasa kimsingi hizo ndizo hoja za msingi ambazo binafsi naziona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine kubwa inahusu gharama ambazo Serikali inatumia kuwekeza kwenye kujenga hiyo kada. Hawa Madaktari na Maprofesa, Wahadhiri na Madaktari Bingwa ni kada ambayo ni *rare* sana katika Taifa lolote. Fedha inayotumika kuwafikisha hapo ni kubwa sana, lakini pia muda tunaotumia kuwajenga na kuwaelimisha ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa wa kawaida wengi wanafikia nafasi hiyo wakiwa na miaka 35 hadi 50 na muda wa kulitumikia Taifa unabaki labda miaka mitano, kitu ambacho ni hasara kubwa kwa Watanzania lakini pia hasara kubwa sana kwa Taifa. Pia gharama za kumsomesha daktari bingwa mmoja tu na taaluma hizi hapa hatuna, tunawapeleka nje ya nchi, ambapo UK peke yake inagharimu milioni mia moja thelathini na tisa, ni kiasi kikubwa sana cha pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Wahadhiri wa vyuo vikuu, wale ambao tunataka waweze kuwapeleka vijana wetu kwenye soko la ushindani wa ajira kwa nchi ya Uingereza peke yake inagharimu milioni themanini na nane kumpata mtaalam mmoja mwenye hizo sifa. Kwa hiyo, unaona ni uwekezaji mkubwa sana ambao mtu binafsi anaufanya lakini pia Serikali inaufanya. Itakuwa si jambo la hekima na la busara kuifanya hii rasilimali watu ambayo tunaijenga kwa muda mrefu itumike katika muda mfupi tu kwa maslahi makubwa ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna maeneo ambayo tunaweza tukajifunza; sisi Watanzania si watu wa kwanza kufikia maamuzi kama hayo. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria ameeleza bayana, ametupa mifano, kwamba Nigeria muda wa kustaafu miaka 70 kwa hiyari lakini anakwenda mpaka miaka 75, nchi jirani ya Kenya miaka 70 kwa kada kama hiyo. Nchi zingine ambazo zimeendelea zaidi Ujerumani hata Uingereza hawana kipindi cha kustaafu inategemea uwezo wa mhusika lakini pia mahitaji ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, hiyo ni kada ambayo tukiziondoa na kada zingine zote ambazo zina haki sawa katika Taifa, hii ni kada adimu sana kuipata katika historia ya nchi yetu na ndiyo maana unaona wanatoka, wanamaliza watu 395 wanarudishwa kazini watu 324 asilimia 82. Kwa hiyo, naunga mkono hoja kwamba huu Muswada upite ili taifa letu liweze kunufaika na rasilimali watu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kwa Serikali ni hii, tunakwenda, naamini Waheshimiwa Wabunge tutakubali kuipitisha na sasa itakuwa sheria, lakini ni vyema sasa Serikali tukaja na mkakati mahsusi kabisa wa kupunguza hili tatizo. Hii ni kwa sababu kuna Watanzania wengi wanakosa fursa kama hizo kwenye maeneo mbalimbali. Hatua ambayo Serikali inaichukua kwanza itajenga motisha kwa vijana kuwekeza katika elimu ili waweze kuwa madaktari bingwa lakini pia wafikie hadhi ya uprofesa katika shughuli zao, itawapa hiyo motisha. Pia Serikali sasa ije na *succession plan* ya eneo hilo la elimu na eneo la afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndio ulikuwa mchango wangu wa leo. Nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhagama kwa mchango wako. Mheshimiwa Najma Giga atafuatiwa na mheshimiwa Taska Mbogo

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na natumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwanza lakini kuwatakia Waheshimiwa Wabunge wote heri zote za mwaka mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache tu ya kuchangia katika Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa mwaka 2017. Sheria hizi ukitazama zimeletwa kwa uchache kwa maana ni kidogo lakini zina *impact* kubwa na maslahi mapana sana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa sheria hii ya Ufilisi ni sehemu ndogo tu lakini lengo lake nalo pia ni zuri katika kufanya utekelezaji uwe mwepesi katika Sheria ya Ufilisi kwa kuweka tafsiri ya neno hili la *official receiver*. Kwa hiyo hili halina mjadala mkubwa na naamini wote mtakubalina na mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Sheria ya Bajeti hii inadhamiria kuweka hali sawa katika Bunge letu baina ya kanuni zetu na sheria. Kwa hiyo hili nalo nafikiri ni jambo zuri na naamini wote tutakubaliana, kwamba kupokea Mpango wa Bajeti wa Serikali katika kipindi cha Oktoba na Novemba itakuwa ni vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naishukuru Serikali kwa kuona kwamba kuna umuhimu wa kuweka *exception* katika ule mwaka ambao tutafanya uchaguzi na kuweza kupokea mpango huu sasa katika mkutano wa pili wa Bunge. kwa hiyo, nalo hilo limekaa vizuri halina tatizo lolote na naamini wote tutakubaliana hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye suala la ardhi, yaani masharti kuhusu kutumia ardhi kwa ajili ya kupata mkopo. Hapa lazima niseme kidogo zaidi. Kwanza naiunga mkono na kuipongeza sana Serikali kwa kuweza kuona kwamba umuhimu wa kuendeleza ardhi yetu ya Tanzania. Hili ni jambo muhimu sana, tusilione kwa udogo tukaitizama kwa urahisi lakini inaonekana muda mrefu Serikali yetu inapata hasara, watu wanakopa kwa kutumia ardhi iliyopo Tanzania ambayo haijaendelezwa na wanaweza kuendeleza maeneo mengine ambayo yapo nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuwepo au kuletwa kwa marekebisho ya sheria hii, yatasaidia ardhi ya Tanzania kuweza kuendelezwa. Haiwezekani leo mtu anakopa kwa kutumia rasilimali ya ardhi ya Tanzania na kuendeleza sehemu nyingine ambayo si ya Tanzania. Kwa hiyo, sheria hii naamini Watanzania wote wazalendo wa nchi hii wataunga mkono na kukubaliana na marekebisho haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye sehemu ya mwisho ambayo ni Sheria ya Utumishi wa Umma, kuongeza umri wa wastaafu hasa tukienda kwenye kada ya maprofesa na madaktari bingwa. Kuhusiana na hili Serikali pia imeleta hoja nzito na hoja za msingi. Ni kweli kabisa kada hii ni muhimu sana kwa Taifa letu na hao watu bado tunawahitaji kwa uchache wao kwa maslahi ya Taifa letu, hii haina mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa tunakubali kurekebisha sheria hii kwa maslahi mapana ya Taifa letu lazima Serikali ione namna mbadala wa ku-*fill gap*, hiyo ndiyo itakuwa *solution* ya kudumu. Tutaenda na sheria hii tutarekebisha leo, tutaweza kuitumia na naamini itatufikisha pazuri ili kuondoa gharama kubwa ambayo tumeitumia siku zote katika Serikali yetu katika kuongeza mikataba ya watu hawa ambao tunawahitaji katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida zipo pande mbili, kwamba kuna wengine ambao wanaongezewa muda wanajiweza bado wapo na afya nzuri na bado wataleta maendeleo katika Taifa letu. Pia tutawakwepa wale ambao wanasomeshwa na Taifa hili halafu wanafika umri wa miaka 55 wanasema wanataka kustaafu kwa hiyari anakwenda kutafuta mpango mwingine wa binafsi na anaacha maslahi mapana ya Taifa letu yanakwenda pembeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mambo hayo mawili yamesaidia kuonesha hoja ya msingi ya Serikali na kwa kweli naunga mkono suala hili, lakini narudi pale pale tena, Taifa letu bado lina uchache wa kada hizi, kwa hiyo naomba tupange tu mpango endelevu wa kuona kwamba tunaondoa urasimu kwanza katika kuhakikisha hawa wasomi wetu wanafikia *level*/hizi ambazo tumezikusudia za Maprofesa na Madaktari Bingwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu pia kwa upande mmoja urasimu ndio unaosababisha, mtu anaandika *paper* miaka mitatu mizima hasogezwi popote au hajibiwi lolote. Kwa hiyo hii inarudisha nyuma kuongeza hizi kada za Mprofesa au *Lectures* wa vyuo vyetu. Kwa hiyo, naomba hilo suala la urasimu liangaliwe sana na Serikali ili tuweze kuwasogeza mbele hawa wasomi wetu ambao wanatakiwa wafike katika kada hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba gharama ya kusomesha Madaktari bingwa nje ya nchi ni kubwa sana lakini bado nasisitiza kuna umuhimu mkubwa sana wa Serikali yetu kupanga fungu maalum la kuweza

angalau basi tusiwafikie wenzetu wa nchi nyingine za jirani ambao wanaweza kupeleka wasomi wetu kwenda kutafuta hii fani ya udaktari bingwa nje ya nchi, basi angalau na sisi tuweze kufanya japo kidogo tuanze taratibu ili kuona kwamba *gap* hili linaweza kuondoka miaka ya mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini nimeeleweka kwa machache haya, naomba na wengine waweze kuchangia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Najma kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Muswada huu. Napenda kuipongeza Serikali kwa kuja na marekebisho ya sheria hizi. Ningeomba tu Serikali iendeele kuboresha Muswada huu kwa kushirikisha wadau mbalimbali ili uweze kukaa vizuri zaidi. Hii ni kwa sababu kanuni ya kushirikisha wadau ni kanuni ya 84 na Ibara ya Katiba ya 8 na 21 inatuambia kwamba tunapotunga sheria lazima tushirikishe wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu sheria hizi zinakwenda kutumika kwa wananchi wote wa Tanzania. Sisi tukiwa kama wawakilishi wao tunakuja tu kuleta mawazo ya wananchi wanasemaje, lakini tunapowaleta wadau kuja kutoa maoni yao kuhusu sheria fulani inasaidia kuelewa zaidi undani wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda niipongeze Serikali kwa kubadilisha umri wa kustaafu kwa Maprofesa na Madaktari, kutoka umri wa miaka 55 mpaka 60 kwenda umri wa miaka 60 mpaka 65. Naipongeza Serikali kwa sababu hizi *profession* za udaktari na uprofesa unaweza ukasema ni *rare professions* kwa sababu si kila mtu anaweza kufika *level* ya uprofesa na sio kila mtu anaweza akafika *level* ya kuwa daktari bingwa. Kwa hiyo ili tuweze kuwatumia hawa madaktari bingwa vizuri na

tuweze kuwatumia maprofesa wetu vizuri, naipongeza Serikali kwa kubadilisha huo umri kutoka miaka 60 mpaka miaka 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata kule *UN*sasa hivi wanastaafu wakiwa na miaka 65 na *voluntary retirement* ni miaka 62. Kwa hiyo, kwa kuleta Muswada huu ni muafaka, sisi tungebaki peke yetu kufika kwenye miaka kustaafu na miaka 55. Kwa kuja na wazo la miaka 60 mpaka 65 kwa maprofesa na madaktari ni wazo jema. Tena nafikiri kwa profesa na daktari kwa sababu mtu akishajifunza kitu kinakaa kichwani maisha na hakibadiliki labda Serikali ingefikiria kutoka 65 kupeleka 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu unamkuta profesa ana miaka 72 lakini bado ana nguvu zake, anastaafu Serikalini na anakwenda kufanya kazi kwenye *private institution*. Tunavyo vyo vya *private* unakuta profesa ametoka pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam lakini unamkuta amekwenda pale Tumaini *University* anafundisha au amekwenda *university* nyingine kama za Makumira kule Arusha anafundisha pale. Sisi kama Wabunge tunatakiwa tulifikirie hili na tu-*support* Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Serikali inaweza siku nyingine ikaja na miaka 65 kwenda 70 kwa maprofesa na madaktari. Hii ni kwa sababu ujuzi wanakuwa nao kichwani na ujuzi wa mtu unakaa *lifetime*, si kwamba mtu anazeeka anatoa ujuzi, mtu anapokuwa mzee nafikiri ule ujuzi ndio unazidi kushamiri vizuri pale kichwani kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Serikali kwa kuja na marekebisho ya ibara ya 120 na naipongeza Serikali kwa kuwa haijafanya marekebisho kwenye zile hati za kimila ila ningeomba baadaye Serikali ifikirie pia kuweka sheria, kuzijumuisha zile hati za kimila ili wazawa wa Tanzania na wananchi wa vijijini waweze kutumia zile hati zao za kimila kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu katika Muswada huu hati za kimila hazipo, hazihusiki kwenye Muswada huu, lakini kwa baadaye kadri Serikali itakavyoona, kwa sababu wananchi wengi walio na mashamba makubwa wengi wameyarithi kutoka kwa wazazi wao. Shamba unakuta lilikuwa la babu yake ndio pale ambapo kila kitu kipo, makaburi ya babu zake yapo pale, ni mashamba ambayo wamegawana pale kiukoo na wana hati ya kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa baadaye Serikali iangalie jinsi gani ya kujumuisha hizi hati za kimila ziweze kutumika ili wananchi wa vijijini nao waweze kutumia hati zao za kimila kupata mikopo benki na kuweza kupata mitaji ya kufanyia biashara kubwa. Pia wananchi wa vijijini wapate *opportunity* ya kuweza kuwekeza nje ya nchi kwa kutumia hati zao za kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kufuata maoni ya Kamati ya Katiba na sheria kwa kuondoa kifungu namba 25B ambacho kilikuwa kinampa mamlaka Waziri kutoa maoni yake kwamba mtu anapotaka kustaafu kilikuwa kinampa *power* Waziri ya kuweza ku-*determine* umri wa mtumishi kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ulipokuja kwenye Kamati yetu, tulipendekeza kwamba kifungu hiki namba 25B kiondolewe kwa sababu Waziri mhusika anaweza akakitumia vibaya, anaweza akawa hampendi profesa fulani au hampendi mwajiriwa fulani akakitumia vibaya kwa sababu ana mamlaka ya kuongea na Rais akapendekeza kwamba yule mtu astaafishwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kilipokuja kwenye Kamati yetu tulipendekeza kwamba kiondolewe kwa sababu tuliona kwamba kwanza kina ubaguzi halafu kinampa Waziri *excess power* ambayo anaweza akaitumia vibaya. Nashukuru katika marekebisho yaliyowekwa hapa kwenye jedwali, Serikali imekuwa sikivu na imekiondoa kifungu hiki. Sababu zilizofanya tukiondoe zilikuwa ni sababu hizo.



Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Serikali hapo baadaye iendelee kuongea na wadau wa benki, nikimaanisha kwamba benki tofauti, iendelee kujadiliana nao kuhusu suala la wakopaji. Katika Muswada huu tumeona kwamba benki wanao wajibu wa kupeleka ripoti Serikalini kuhusu pesa ambazo wanamkopesha huyo mtu aliyenda kukopa pesa na kuweka dhamana ya shamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mifano mingi ambayo tumeona, yapo mashamba mengi ambayo watu wanazo hati za hayo mashamba na wameweza kwenda benki na wakachukua pesa nyingi benki na baadaye tumeona kwamba wale watu ambao wapo nje ya Tanzania wamekuwa ni mabilionea kwa kutumia ardhi ya Tanzania kupata huo ubilionea. Wameweza kutumia haya haya mashamba yetu yalipo humu nchini, wamepeva yale mashamba, walipewa hizo hati miliki na wakazipeleka benki wakachukua pesa. Baada ya hapo wameenda nje wanafanya biashara nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiombe sasa Serikali kwa kutumia Muswada huu na kwa kutumia sheria hii itakapopita iweze kuwafuatilia wale wote ambao walichukua mashamba humu nchini Tanzania na wakachukua hizo hati wakaenda benki wakazoa mamilioni ya pesa na sasa hivi ni mabilionea nje ya nchi hii ya Tanzania; wawafuatilie ili waweze kurudisha hizo pesa zetu. Nafikiri sheria iweze kuchukua mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sheria hii baada ya kupita tunaiomba Serikali ichukue jukumu la kurudisha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja *a hundred percent*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hii hoja ni nzuri sana na ndio mnaisaidia nchi. Nadhani muda ni muhimu tukauangalia, nitamwita Waziri wa Nchi atoe hoja, itafurahisha kama tutaimaliza hoja hii tusirudi saa 11, mnaonaje?

**WABUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

**MWENYEKITI:** Sawa kabisa, sasa ili twende vizuri Waheshimiwa Wabunge, mnaonaje kama tutapiga dakika tano tano anayechangia badala ya dakika 15. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

### HOJA YA KUTENGUA KANUNI

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Mtemi Chenge, naomba kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) nitoe hoja mbele ya Bunge lako Tukufu ili Bunge liendelee na mjadala wa shughuli hii mpaka pale tutakapokuwa tumeukamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono na zaidi ya Wabunge 10, nawashukuru, sasa nitawahoji.

*(Haja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Walioafiki wameshinda.

Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea, ahsanteni sana. Sasa ni dakika tano tano, ninaye Mheshimiwa Salome Makamba dakika tano, ninaye Mheshimiwa Joram Hongoli dakika tano.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nami nichangie Muswada huu kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kumshauri Waziri mwenye dhamana kwamba muda uliowekwa kwa ajili ya kutoa taarifa ya kuendeleza ardhi kwenye Sheria ya Mabadiliko ya Ardhi wa miezi sita ni mchache sana. Sote tunafahamu kwamba lengo la mkopo ni kufanya biashara, sheria imelazimisha mtu achukue mkopo na aende akaendeleze eneo ambalo amekopea, kitu ambacho kwangu naona si sahihi kwa sababu akiwekeza au akiendeleza eneo lile inawezekana haikuwa malengo ya mkopo ule na hivyo anaweza akashindwa kurejesha, jambo ambalo linaweza likasababisha akanyang'anywa ardhi pia na hiyo *financial institution*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme, ama kifungu hiki kiangaliwe kwa umakini zaidi au kama itawezekana muda wa kutoa taarifa ya uendelezaji uongezwe ili yule mtu aweze kuiwekeza ile pesa kwenye eneo lile kwa awamu ndogo ndogo wakati anakamilisha malengo yake ya kuchukua mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niseme kuna mkinzano mkubwa sana kati ya Sheria ya Uendeshaji wa Mabenki Tanzania na sheria hii kwa sababu benki hazitoi mkopo kwa ardhi ambayo haijaendelezwa. Kwa sababu hiyo, ni lazima ili tuweze kupata maelewano kati ya sheria hizi mbili, Serikali ione umuhimu wa kuongea na watu wa benki waelewe nini lilikuwa lengo la kuweka sheria hii ili inapofikia kwamba wanatakiwa kuwakopesha watu ambao hawajaendeleza ardhi, pesa ziweze kutolewa kwa watu wale kama ambavyo sheria inaeleza, lakini mpaka sasa bado kuna ukinzani mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe mawazo yangu kwenye huu Muswada wa Utumishi wa Umma. Nadhani wadau katika Muswada huu hawajashirikishwa vizuri. Serikali imefikia maamuzi ya kuongeza kuanzia miaka 60 kwa hiari

na miaka 65 kwa lazima lakini bado ipo haja kubwa sana ya kuweza kuangalia maoni ya wadau. Kwa sababu kuna mafunzo mbalimbali yatatoka hapo watapewa wale wataalam ambao wamefikisha miaka 65, tunadhani yatafanyika kwa ufanisi na wakati mtu huyu tayari ana umri mkubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiachana na hilo; unadhani kwa kuongeza mkataba, kwamba mtu atastaafu kwa miaka 65 kwa lazima, unadhani ndiyo inaleta ufanisi au unamlazimisha yule mtu afanye kazi hata kama hataki? Ndiyo tunarudi kwenye suala la *morale; professionalism* inakwenda na *morale*. Kwa hiyo nimshauri sana Mheshimiwa Waziri akazungumze vizuri na wadau kuhusu kuongeza umri, kwa sababu mimi naamini si wote ambao wanapendezwa na suala la kuongezwa umri wa kustaafu kama ambavyo imeelezwa katika *proposal* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nimalizie kwa kusema kwamba hii Sheria ya Ardhi kuna jambo la msingi ambalo tumelikwepa la zile ardhi ambazo zinamilikiwa kimila; bado nahitaji ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana. Anasema wale wanaomiliki kimila, mabadiliko ya sheria hii hayatawagusa, lakini wapo watu wanamiliki maekari ya ardhi kimila na wanatamani kufanya uwekezaji kwa kuchukua mikopo; na hizi ndiyo zimekuwa kelele za Wabunge wengi humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi ardhi zao wanamiliki kimila na si kwa utaratibu wa Serikali na wakati mwingine sio kwa kutaka kwao, ni kwa sababu mfumo wa kupata hatimiliki ya Kiserikali bado haujakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili la wale wanaomiliki zile hati kimila; naamini ipo sababu ya msingi kama kweli tunataka kufanya uwekezaji wa ndani, kama kweli tunataka kujenga Tanzania ya viwanda na kuwapa uwezo watu ambao wanawekeza, ipo sababu ya kuzingatia umiliki wa kimila. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia Muswada uliopo mbele yetu. Nami nianze kuipongeza Serikali kwa kuleta mabadiliko haya, ni ya muhimu sana kwa kufikia malengo ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite pale kwenye Sheria ile ya Ardhi ya Marekebisho, Sura ya 113 (*The Land Act CAP, 113*), masharti yanayohusu matumizi ya ardhi, hasa kwenye kupata mikopo kwa maana ya *mortgage*. Ni kweli tumeona wawekezaji wengi wamekuwa wakitumia ardhi kwa ajili ya kupata fedha kupata mikopo kwenye benki mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, fedha hizi mara nyingi zimekuwa haziendi kwa ajili ya kuendeleza maeneo au mashamba yale ambayo wamekopea fedha na badala yake wamekuwa wakifanyia shughuli nyingine au wamekuwa wakipeleka nje kuwekeza huko nje ya nchi na hatimaye sisi kama nchi tumekuwa tukikosa ajira kwa maana ya yale mashamba ambayo wamekopea fedha yamekuwa hawaendelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa mfano mengi ya mashamba ya mikonge yaliyopo kule Tanga, mashamba ya chai yaliyopo Tanga na maeneo ya Lupembe kule; unakuta watu wamekopa fedha nyingi, lakini fedha hizi hazitumiki kuendeleza mashamba haya na hatimaye tunakosa ajira kwa vijana wetu, lakini pia tunakosa fedha ambazo zingetokana na kuuzwa yale mazao na kupata fedha za kigeni. Kwa hiyo, kimsingi uchumi wa nchi unaharibiwa na hawa wakopaji ambao wanakopa lakini wanaenda kufanyia mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sheria hii ni nzuri, itasaidia kuhakikisha kwamba fedha zinazokopwa, hasa kwa

mashamba yale ambayo hayajaendelezwa ili yaweze kuendelezwa na yale ambayo yameendelezwa kidogo basi yaweze kupanuliwa zaidi. Kwa hiyo nimeona hii sheria ni nzuri na itasaidia kuhakikisha kwamba fedha zinawekezwa nchini na hatimaye uchumi wa nchi unakuwa tofauti na ilivyokuwa hapo mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nichangie na Sheria hii ya Utumishi wa Umma ambayo inahusu kuongeza muda wa kustaafu, kwa maana ya maprofesa, wahadhiri waandamizi, lakini pia na madaktari bingwa. Ni kweli, wanasema wataalam kwa uzoefu kwamba daktari bingwa au mhadhiri mwandamizi au profesa jinsi umri unavyozidi kusogea basi uzoefu unaongezeka. Kwa hiyo kwa kufanya hivi itatusaidia maprofesa, wahadhiri waandamizi na madaktari bingwa kuweza kuwawezesha wale wengine ambao hawana uzoefu wa kutosha waweze kuwapa uzoefu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia sheria hii imefuata nchi nyingine jinsi wanavyofanya, kwa mfano Nchi ya Kenya, wao madaktari bingwa hasa waliopo kwenye hii fani ya tiba wanastaafu kwa hiari katika umri wa miaka 70 na kwa lazima miaka 75. Pia ukiangalia Nchi ya Nigeria, madaktari na maprofesa wanastaafu kwenye umri wa miaka 70; Botswana nao wanastaafu kwenye umri wa miaka 65 na nchi nyingine kama Zimbabwe wanastaafu miaka 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa na sisi pia tutakuwa sawasawa na nchi nyingine kwa maana ya hawa maprofesa, wahadhiri waandamizi na madaktari bingwa, kwa hiyo tutaendana sambamba na nchi nyingine. Maana yake wataalam wetu wengi wamekuwa wakistaafu katika umri wa miaka 55 wanaondoka kwenda kusaidia nchi nyingine ambako wanaendelea kustaafu mpaka miaka 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona madaktari bingwa nao wamekuwa wakiamua kustaafu mapema ili waweze kuingia kwenye mkataba na hatimaye waweze kulipwa pensheni lakini pia wanaanza kulipwa ule mkataba, kwa hiyo

imekuwa ni gharama kubwa sana kwa Serikali. Kwa hiyo kwa kuongeza muda maana yake tunatatua tatizo la kulipa gharama kubwa kwa ajili ya mikataba ambayo tungewapa hawa madaktari ambao wamefikia miaka 55 au wamefikia miaka 60, wameshastaafu tayari; kwa hiyo kwa mtindo huu tunaokoa gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sasa Serikali katika mipango yake ni vizuri ijipange vizuri kuhakikisha kwamba inaweka mpango wa muda mrefu wa kuhakikisha kwamba wanaanza kuwaandaa hawa madaktari bingwa mapema au wanaanza kuwaandaa hawa wahadhiri waandamizi mapema ili kusijitokeze tena haya matatizo ambayo yamejitokeza katikati kuwa na... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ruth Mollel atafuatiwa na Mheshimiwa Joyce Sokombi na Mheshimiwa Ally Saleh ajiandae.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Muswada uliopo hapo Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia inaonesha kwamba ajira kwa watumishi wa umma zimekuwa hazitoki kwa muda mrefu na vile vile zoezi lile la kuondoa watumishi wengi katika utumishi wa umma limesababisha upungufu mkubwa wa vijana ambao wangeweza kukua katika utumishi wa umma waweze kuendeleza utumishi wa umma. Kwa hiyo, matokeo yake sasa tuliyokuwa nayo si katika fani tu ya madaktari na maprofesa lakini ni katika fani zote, kwamba tuna watu wengi

wanastaafu lakini hatuna maafisa waandamizi hapo katikati ambao wanaweza kuchukua hizo nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *gap* ambayo pia iliyowakumba madaktari na maprofesa inaongezewa pia na kwamba sasa hivi ajira hazitoki kwa muda muafaka, kuna madaktari wengi ambao wamemaliza shule MUHAS na kila mahali wako bado mtaani hawajapata kazi. Sasa ikiwa, sawa, kuongeza umri, hawa madaktari ambao wako mtaani ambao ndiyo baadaye tutakuwa na maprofesa na madaktari bingwa, Serikali inafanya jambo gani kwa ajili ya kuhakikisha hawa walioko sasa hivi mitaani wanaajiriwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, wote tumekuwa mashahidi katika kupitisha bajeti. Bajeti ya mafunzo ni kidogo sana, kwa hiyo matokeo yake tunakuwa hatuna wataalam (*specialists*) kwenye maeneo mbalimbali kwa sababu Serikali haitengi fedha za kutosha kwa ajili fedha ya mafunzo ya kujenga rasilimali watu. Kwa hiyo ni muhimu sasa Serikali kwanza ikatoa ajira kwa hao madaktari na wanachuo ambao wanafanya *internship* ili waweze kuongeza nguvu katika utumishi wa umma na vile vile pesa itengwe kwa ajili ya ajira ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamezungumzia Ghana, Uganda, Kenya, Nigeria, Botswana wanakwenda mpaka miaka 70. Wanakwenda mpaka miaka 70 kwa sababu *package* wanayopata ni nzuri, ndiyo maana watu wako tayari kwenda mpaka miaka 70. Pia tumeona kwamba madaktari wetu wengi wako Botswana, mimi nina shemeji yangu yuko Botswana na *he was one of the best neurosurgeons*, yuko Botswana kwa sababu kule maslahi ni mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali, pamoja na kuongeza hiyo miaka 60 mpaka 65, ambayo sidhani kama ni suluhu, Serikali iangalie ni kwa jinsi gani itaboresha maslahi ya madaktari, hao maprofesa ili wawe na moyo wa kubaki nchini. Maana kama unalipwa vizuri huwezi ukaondoka



kwenda kwenye nchi nyingine, utabaki kwenye nchi yako kuweza kutoa *contribution* katika kuendeleza nchi yako. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni muhimu kwa Serikali sasa kuangalia *package* ya madaktari, *package* ya *professionals* kwa sababu wengi wasingependa kuendelea mpaka miaka 65, wengi wangependa kuchukua pesa zao waondoke kwa sababu ya maslahi duni. Kwa hiyo ni muhimu basi hii *package* yao ikaweza kuangaliwa upya ili iwape motisha ya kufanya kazi katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile *studies* zimeonesha kwamba baada ya kustaafu *life expectancy* ni miaka 12 tu. Kwa hiyo kama wewe umeongezewa miaka ya kustaafu mpaka 65, *package* unayopewa mshahara wenyewe ni duni, *life expectancy* baada ya kustaafu miaka 65 miaka 12, hiyo hela siji utaitumia kwa muda gani. Kwa hiyo ni vizuri miaka 60, 65 sawa lakini si suluhu, tuangalie kuongeza mishahara ya watumishi ili iwape motisha wabaki nchini na kuendelea kufanya kazi na kuchangia katika uchumi wa Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mollel kwa mchango wako. Mheshimiwa Joyce Sokombi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh na mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi hii. Nitachangia upande wa Sheria ya Ardhi, kipengele cha tisa kifungu cha 120A(3)(a)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona ni jinsi gani hii Sheria ya Ardhi ilivyowekwa, kwamba mtu anapokopa ni ndani ya miezi sita ripoti inatakiwa ipelekwe, kwa kweli muda ni mdogo sana. Tupo hapa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi, kuwainua kiuchumi na kuwalinda, kuhakikisha wanapata haki zao sawa sawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba yawekwe mazingira mazuri kwa namna ya kuweza kumsaidia huyu mwananchi anayekopa kwa njia hii ya ardhi. Tukiangalia muda uliowekwa wa miezi sita ni muda mdogo sana, *at least* ungewekwa hata mwaka mmoja, tena hapo ni *at least*, hata huo mwaka mmoja bado tunaona kwamba pengine muda utakuwa bado hautoshi. Ukiangalia jinsi changamoto zilizvyo nyingi, miezi sita haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia mtu hata kama ni mfanyabiashara amechukua mkopo, ndani ya mwaka mmoja ndiyo anaanza kuona faida. Kwa hiyo, hiyo miezi sita bado itakuwa ni midogo sana kwa kumwezesha mtu huyu kuweza kulipa ndani ya hii miezi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sheria hii inamkandamiza mtu ambaye anakaa kijijini; watu wengi wanaokaa vijijini wana hatimiliki za kimila. Tayari hapa kwenye hiki kitabu cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kinaeleza kabisa kwamba mtu akiwa na hatimiliki ya kimila haruhusiwi kupata mkopo huu. Sasa hapa tunaona kabisa namna gani hii sheria inavyomkandamiza mwananchi au inabagua, yaani kuna watu wa vijijini ambao hawataruhusiwa kuchukua mkopo na watu wa mjini ambao wanaruhusiwa kuchukua huu mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuiangalie kwa umakini kwenye hiki kipengele cha 9 (3) Tutakaporekebisha vizuri kipengele hiki tutaweza kumsaidia mwananchi, maana lengo letu ni kumsadia mwananchi na sio kumkandamiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango. Tunaendelea, Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Juzi hapa tulisikia kwamba wanasayansi wa Kenya wamegundua *satellite*, sasa hivi Kenya wametengeneza

*satellite* yao wenyewe ambayo ita-serve madhumuni yao na si kutegemea *satellite* za nchi za magharibi ambazo zimetawala anga zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hatufanyi haki ya kuweka pesa katika *research*, nazungumza hapa haja ya kuweka pesa kwa ajili ya maprofesa kuwaweka kwa muda mrefu, maprofesa hawa ambao haki yao ya kwenda *sabbatical* ni ndogo, mazingira ya kuweza kufanya kazi madogo, mazingira ya kuongeza sayansi ya kisasa mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hata kama tutaunga mkono kwamba tuongezee muda wataalam hawa, lakini kama alivyosema Mheshimiwa Mollel, kama *package* ni ndogo basi hali kadhalika wataondoka, au watabaki katika madaraka kwa kuwa tu wanajua kuna kitita kinawasubiri na kwa hiyo matokeo yake watabaki ilimradi wabaki. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma *Wage Bill* tuliyoletewa na Serikali ambayo inaelezea kwamba *2.9 billion* wanalipwa maprofesa wakubwa, *1.8* wanalipwa maprofesa wadogo na *1.3* kwa jumla *5.5 billion* kwa miaka miwili ni mkataba mzima wa wataalam hao. Unaweza ukaziona ni nyingi lakini *after reflection* ukizigawa unaweza ukaona zile *package* ni milioni tatu tu kwa kila mtaalam, wakati akienda Botswana anaulizwa *how much does he or she want*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ingawa tunaunga mkono kwa maslahi mapana ya Taifa, kwa maana kwamba kuna ukosefu wa wataalam kwa asilimia 50 sasa hivi Tanzania; lakini pia viko vyuo kama *UDOM* hata profesa mmoja hawana. Kuna ukweli kwamba machapisho yameshuka Tanzania; labda pengine tungeweza kuchapisha machapisho 500, 600 kwa ujumla kwa maana ya nchi nzima, hatuwezi na huwezi *sustain academic institutions* bila machapisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tayari udororaji wa taaluma yetu unashuka, lakini je, tuna-*address* vitu hivyo?

Wengine tulihoji katika Kamati hii isiwe njia ya mkato tu ya kupata wataalam; kuna *program* gani endelevu ya kupata wataalam? Ni kweli tulikuwa na *gap* ya miaka 10 ya kutoajiri, lakini tulisomesha? Kwa sababu kama tulisomesha na kama watu walisoma *gradually* wangeweza kupanda, kwa hiyo hata hii *agreement you can't buy from it* kwamba kwa kuwa kulikuwa na *gap* ndiyo maana sasa hivi kuna uhaba wa wataalam, lakini pia hatukusomesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pengine tulifanya uchoyo wa *promotion*; kwa sababu hiyo inafanyika katika *system* ya Serikali. Inawezekana mtu ana *qualify* lakini anacheleweshwa kwa sababu nyingine nyingine tu, mbali ya watu ambao wamekatizwa kwa sababu ya maoni yao pengine kwa sababu ya fikra zao. Hasa katika kuja katika vyama vingi sasa hivi watu wengi *academicians* wameingia kwenye *loggerhead* na Serikali, pengine hawakubaliki katika vyuo na kwa sababu hiyo wameona kwamba kuna mgongano wameamua kuacha na kwa hivyo ile *gradually* ya watu kupanda pengine imesaidia katika kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo nakubaliana na Serikali katika hili, kwa maana kwamba kuja na wataalam kuwaongeza kutoka 60, mpaka 65; lakini isiwe kwamba ni mwisho wa mambo. Ukweli ni kwamba tunahitajika kutengeneza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu nchi nyingine wanatengeneza mazingira wala vijana wao waende wakasomeshe nchi nyingine kama kuna *excess*. Mwaka jana sisi tuliambiwa kuna *excess* ya madaktari hapa tukataka kuwapeleka Kenya. Kwa hiyo wakati mwingine ni *contradiction* ya Serikali, wengine tukataka waenda kule, tuwasaidie Kenya, wakati kumbe sisi wenyewe tuna upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukweli ni kwamba kuna taka tuwe *very pragmatic*, tuwe wa uhalisia kwamba tatizo hili haliwezi kukamilishwa tu kwa kuzidisha umri, lazima tuwe na *program* ya kutosha kuweza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri sana. Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kunipa nafasi niweze kuchangia kidogo kwenye Muswada ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sheria ya ardhi inayosema kwamba ardhi zinaweza kutolewa kama dhamana kwa ajili ya kupata mkopo kwa ajili ya kuendeleza imekuwa inatumika sana kwenye mashamba makubwa. Kwa Tanzania ardhi ambayo zina hati kabisa benki hazikubali kutoa mikopo kama hakujaendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sheria ipo na 120A; kwa nini mabanki yanakataa kutoa fedha mikopo kwa kutumia viwanja (*plots*) ambazo tayari zina hati na mpaka viendelezwe, lakini kwa mashamba ambayo hayajaendelezwa wanatoa tena fedha ambazo ni nyingi. Kwa hiyo ningependa kwanza sheria hii ambayo ipo 120A iweze kutekeleza benki zikubali hati na kutoa fedha ili wananchi waweze kuendeleza yale maeneo kwa ajili ya maisha ya watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, tumekuwa na mapori mengi sana Tanzania ambapo ukiyafuatilia mengi unakuta ni mapori kwa sababu fedha ilichukuliwa kweli ilienda kuendeleza maeneo mengine. Nakubaliana na Serikari kwamba mashamba ambayo yalichukuliwa hati, ilichukuliwa mikopo, mikopo itumike kwa ajili ya kuendeleza maeneo ya pale pale kwa sababu sasa hivi mapori ni makubwa kwa sababu fedha ilichukuliwa na watu wengine pengine hata wako nje ya nchi lakini mapori yako pale fedha inafanya kazi maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali ya kujiuliza, kuna baadhi ya mapori ambayo yameshindwa hata kufuta zile

hati kwa sababu benki zinadai. Sasa atakapokuja ku-*wind up* Mheshimiwa Waziri hapa atuambie; yale mashamba ambapo tayari benki zinadai na wameshindwa kufuta hati kwa sababu zinadaiwa hatima yake ni nini. Yataendelea kuwa ni mapori au Serikali inafanyaje, au italipa sasa mikopo kwa benki zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la kuongeza mmekuja na Muswada hapa wa utumishi kuongeza miaka kwa ajili ya wahadhiri, madakatari, *proffesors* na watu wengine. Tunafanya hivi kwa sababu hatuna watu wa kutosha ku-*fit* nafasi hizo kwa wakati huo. Nina imani aliyeweka miaka 60 *compulsory* kuweza kustaafu alifanya utafiti wa kutosha. Kwa mtu unayefanya kazi kwa kujituma kwa miaka 60 kwa mazingira ya Tanzania unakuwa umechoka, kiukweli kabisa; unahitaji upate muda wa kufanya yale mambo yako mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapongeza muda mpaka miaka 65 *are we sure* kwamba hawa watu wako tayari kufika huko? Tunahitaji ufanisi kwenye utendaji. Kwa hiyo, nadhani tungekuja na mpango ambao utakuwa na ufanisi zaidi kuliko kuongeza miaka, anaweza akawepo tu kwa sababu kuna mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maprofesa wengine wakifika miaka 55 wameshachoka. Wana elimu yao ya kutosha, wameshawekeza wangenda watoke nje ya utumishi, lakini kwa kuwa tunawahitaji kama Serikali wanalazimika kukaa kwenye utumishi. Kwa hiyo, naomba Serikali tuwe na *succession plan* katika kuhakikisha kwamba tuna watu kwenye nafasi hizo. Tuhakikishe kwamba kila mwaka tunajua wanaostaafu ni kiasi kadhaa ili tuweze kuwa na mpango wa ku-*cover* zile nafasi zao. Kwa hiyo hata tulicholetewa leo ni mpango wa muda mfupi, ni miaka 65 baada ya hapo je? Bado shida iko pale pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwenye hili la watumishi lazima Serikali ije na *succession plan* ya namna wahadhiri wanapostaafu nafasi zao zinakuwa *covered* na

wale madaktari bingwa. Leo ukianza ku-*compare* daktari bingwa wa Tanzania na wa Zimbabwe au Zambia ni tofauti kabisa. Daktari wa Ulaya anahudumia watu 15 mpaka 25 kwa siku, daktari bingwa wa Tanzania watu 40 mpaka 100, *definetely* atakuwa amechoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ni tofauti, utumishi ni tofauti, posho ni tofauti. Lazima mazingira yetu tuyaangalie na tuwaangalie watu wetu, tuweze kuhakikisha kwamba tunawapa *package* ya kutosha wafanye kazi vizuri kwa ajili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Profesa Ndalichako, dakika tano, atafuata na Mheshimiwa Lukuvi dakika tano.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja iliyoko mezani. Kwanza nianze kwa kusema naunga mkono hoja hii ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na naunga mkono mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma ambayo inapendekeza kuongeza umri wa kustaafu kwa maprofesa na wahadhiri waandamizi pamoja na madaktari bingwa kutoka umri wa miaka 60 hadi miaka 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kama walivyozungumza Waheshimiwa Wabunge ambao nashukuru sana wachangiaji karibu wote wameunga mkono hoja hii. Uhitaji wa maprofesa na madaktari ni mkubwa sana na ndiyo maana kati ya mwaka 2012 mpaka 2016 maprofesa na wahadhiri waandamizi ambao walistaafu walikuwa ni 395; lakini kati yao walioajiriwa kwa mkataba walikuwa ni 324. Kwa hiyo inaonesha ni jinsi gani bado wanakuwa wanahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumwambia Mheshimiwa dada yangu Magdalena Sakaya kwamba

ukiangalia hizi takwimu hawa maprofesa wanaoendelea; ni kwamba hii mikataba inakuwa ni ya hiari. Kwa hiyo ukiangalia idadi ya wanaomaliza lakini bado wanaendelea ni kubwa. Niseme kwamba Serikali inayo mikakati ya kuhakikisha kwamba suala hili la uhaba wa maprofesa linafanyiwa kazi. Niseme tu kwamba maprofesa hawapatikani kwa kusomeshwa, kuna Mbunge mmoja alikuwa anasema kwamba kuna kipindi tumekaa bila kusomesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa profesa ni juhudi binafsi na inatokana na kuandika, kufanya machapisho. Serikali inapoajiri ngazi ya chini katika vyuo vikuu ni mkufunzi msaidizi (*tutorial assistant*) ambaye anakuwa na *degree* ya kwanza; baada ya hapo sasa anapanda kulingana na mchapisho. Ngazi inayofuata ni Mhadhiri Msaidizi ambaye ni *Assistant Lecture* anatakiwa awe na shahada ya uzamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo anaweza akapanda kuwa Mhadhiri kwa kuandika machapisho matatu. Kutoka Mhadhiri kwenda Mhadhiri mwandamizi yaani *Senior Lecture* lazima awe na shahada ya uzamivu. Kwa hiyo unaweza ukaona kwamba kuna vigezo vingine ambavyo ni juhudi binafsi ya mkufunzi au mwalimu kuweza kufika hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunatambua kwamba baadhi ya wahadhiri wameshindwa kupata shahada za uzamivu kutokana na ufadhili. Mkakati wa Serikali katika mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi bilioni nane kwa ajili ya kutoa ufadhili katika fani ambazo zina uhaba mkubwa wa wahadhiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutatua tatizo la madaktari ambalo lipo nchini tayari Serikali kupitia chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi *MUHAS*; tunayo hospitali ya Mloganzila ambayo ni hususan kwa ajili ya kufundishia madaktari pamoja na watoa huduma mbalimbali wa afya. Tayari Serikali imekwishatenga fedha shilingi bilioni 13.1 kwa ajili ya kukabiliana na tatizo hili ambapo tumewapa kazi



Wakala wa Majengo Tanzania kuweza kujenga baadhi ya majengo ambayo yatawezesha kuongeza udahili wa wanafunzi 1,500 katika mwaka wa masomo 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali imekwishatoa fedha za awali kwa TBA bilioni 3.9. Pia Wizara ya Fedha katika bajeti yake kuna fedha ambazo zimetengwa na kuna madaktari 290 ambao wanasoma kwa ajili ya ufadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda Serikali pamoja na kuomba Muswada wa kuongeza umri wa madaktari na maprofesa lakini tuna mikakati. Niseme tu kwamba uhaba wa madaktari pia umechangiwa na kuongezeka kwa vyo vikiu, jambo ambalo lina afya kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningepomba Waheshimiwa Wabunge wote waunge mkono hoja hii kwa sababu ina maslahi mapana kwa Taifa letu, ina maslahi kwa maprofesa wetu ambao kadri wanavyokuwa wanaendelea na umri wao pia uzoefu katika fani zao unakuwa ni mkubwa na ndiyo maana katika nchi nyingine maprofesa hawawekewi umri wa kustaafu. Naamini kwa kufanya hivyo tutaendelea kuongeza pia vyo vikiu na tutaendelea kuwahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Profesa Ndalichako. Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Ardhi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni mfupi; nataka niwapongeze Kamati na Waheshimiwa Wabunge kwa kuchangia hoja hii ya marekebisho ya sheria ya ardhi, lakini pia naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwa ufupi waliochangia, Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Mbogo na Mheshimiwa Makamba; nataka niwakumbushe kwamba

marekebsho ya sheria ya mwaka 1999 yalitambua kwamba ardhi inathamani hata isiyoendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka kuwaambia wengi ambao mna mashaka kwamba ardhi peke yake mtu hawezi kukopea, inakopesheka kwa sababu ina thamani yenyewe. *Valuers* wanatathimini na wanaandika *business plan* zinakwenda benk wanapata mkopo. Inawezekana huwezi kupata kama thamani ya ardhi yako ni bilioni 1,000,000, *bank* hutoa 50 *per cent* 20, lakini unapewa. Hata kwenye viwanja vya majengo tunakopa kutokana na viwanja vile. Isipokuwa hati zile zinakuwa mali yao mpaka utakapomaliza mkopo wa benki, wanakuja kuzisajili. Kwa hiyo hiyo inakopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hati za kimila tumesema wenye hati za kimila, wale wananchi masikini hawatahusika katika mpango huu kwa sababu kwanza hawakopesheki nje ya nchi kwa kutumia hati za kimila. Pili wale wanaokopa kwa kutumia hati za kimila tayari hati za kimila kwa sheria ina masharti yake. Benki wanakopesha kupitia hati ya kimila, lakini wanapokuja kuuza yale mashamba hawauzi sawasawa kwa sheria kama hati hizi za miaka 99.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanatakiwa kwanza wawauzie *family members*. Hati ya kimila ukichukua kama dhamana uki-*default* yule anayekuja kuuza ile adhi lazima auzie *family members*; kwa hiyo hati za kimila zipo *protected*. Kama ikishindikana wanatakiwa wanunue *within the village*. Kwa hiyo hati za kimila ziko *protected* ndiyo maana tukasema tusiwaingize kwenye mgogoro huu kwa sababu ya *protection* ile ile ardhi ile hai potei iko bado mikononi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Makamba, hivi sasa tumefanya ukaguzi zaidi ya ekari laki moja ambazo hazijaendelezwa, zimewekwa rehani pamoja na *business plan*. Kwenye *business plan* wanasema watatoa ajira, vile vile watajenga viwanda na mali ghafi itatumika hiyo ya mashamba na mazao yatakayozalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yote haya yanayeyuka, watu wanachukua pesa kwa mashamba yasiyoendelezwa, wanachukua zile pesa wanakwenda kufanya biashara za haraka haraka na fedha zile zinalipwa benki. Benki *interest* yao ni kwamba mikopo yao imelipwa, lakini ukiangalia miamala yao kupitia ile *business plan* Serikali inakosa. Kwa sababu kama mtu hakulima maana yake hajafanya biashara, maana angefanya biashara *according to business plan* tungepata kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama angetekeleza ile *business plan* lazima angeajiri watu, kama angetekeleza *business plan* angetengeneza kiwanda cha kutengeneza zile bidhaa au cha kuchakata zile bidhaa. Kwa hiyo Serikali inakosa vingi sana na hayo mambo yanafanyika. Wizara yangu imeshafanya ukaguzi sasa hivi tumeshapata zaidi ya ekari laki moja ambazo zimeshakopewa kwa utaratibu huu. Tumeshuhudia madalali kutoka nje ya nchi wakija kunadi ardhi za watu ambao wame-*default* lakini wamekopa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo marekebisho haya Waheshimiwa Wabunge hayakuletwa kimchezo mchezo. Naamini kwa sababu sisi Wabunge ni wazalendo namba moja ndiyo maana tumeunga mkono hoja hii. Nataka kuwaondoa mashaka kwamba hoja hii haina mgongano wowote wa kimaslahi na benki. Kamishna baada ya wewe kukopa, kabla hujakopa, Kamishna hana habari. Tuna kwambia ukishakopa baada ya miezi sita umeshakopa mpe tu taarifa kamishna kwamba nimekopa kiasi hiki na niko katika *process*, hii basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kwamba miezi sita kwamba umeshamaliza, lakini ujue mpaka unapopeleka *business plan* benki. Unapokopa Kamishna hana habari, ukishakopa basi mjulishe Kamishna na sisi kama Serikali tuna vitengo vyetu vya kufuatilia. Kwa sababu kule benki na kwenyewe nao ni binadamu *Loan Officers* wamekuwa wanadanganya watu wengine. Wanaweza ku-*collude* na mkopaji lakini benki sipate faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka kusema kwamba mikopo ambayo watu wamekopa kwa kutumia dhamana ya ardhi ambayo haijaendelezwa hati zile zinafutika, sisi tunawashauri benki...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuunga mkono.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, mtoa hoja Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa dakika, dakika 15.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuungana kwenye suala la msingi sana kwa maslahi ya nchi; kama hili suala la Muswada huu ambao tunaona hoja zote ambazo zimeletwa kwenye muswada huu; mabadiliko ya Sheria ya Ardhi, mabadiliko ya Sheria ya Utumishi wa Umma, mabadiliko ya Sheria ya Ufilisi, Sheria ya Bajeti na sheria zote ambazo zimeletwa mbele yako. Kwa kweli kwangu nimepata faraja sana ninapoona Waheshimiwa Wabunge wanaungana na kuwa kitu kimoja. Kwa sababu Wabunge wote wameunga mkono hoja hii na Waheshimiwa Wabunge wamechangia vizuri; kwanza naanza kwa kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua mchango mzuri wa Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria. Mchango mzuri wa Kambi ya Upinzani, mchango mzuri wa Waheshimiwa Wabunge wote na naomba niwataje Wabunge hawa kwa heshima yao kabisa. Kwanza Mheshimiwa Mhagama, Mbunge wa Madaba; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Tasika Mbogo, Mbunge

wa Viti Maalum, Mheshimiwa Salome Makamba, Mbunge Viti Maalum; Mheshimiwa Joram Hongoli, Mbunge wa Lupembe; Mheshimiwa Ally Salehe, Mbunge wa Malindi; Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Kaliua; Mheshimiwa Joyce Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum; na mwisho Mawaziri wawili, Profesa Ndalichako Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Mheshimiwa William Lukuvi Waziri wa Ardhi na Makazi. Samahani nimemsahau Mheshimiwa Lucy Mollel, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa ujumla, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na michango yao kwa kweli ilikuwa mizuri, sijui hata kama nitakuwa na ya kuongeza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tu moja, suala la kuoanisha umri huu wa kustaafu; Waheshimiwa Wabunge pamoja na kuunga mkono wamesema kwamba labda tungeenda kama miaka 70 hivi. Ni suala ambalo pia hata ukiangalia bado kuna kubishana kama twende miaka 65 na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachoweza kusema tu ni kwamba mpaka sasa umri wa kustaafu katika makundi mbalimbali ya watumishi wa Umma tulionayo yana miaka 60. Miaka 65 ni Majaji wa Mahakama ya Rufaa akiwemo na Jaji Mkuu. Miaka 65 wengine ni *Controller and Auditor General* (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) ambaye naye anastaafu kwa miaka 65. Watumishi wengine tunaobaki tunastaafu kwa miaka 60 kwa lazima, japokuwa kwa hiari ni miaka 55. Kwa hiyo naomba tuendelee na *standard* hii ya kiwango hiki; nashukuru lakini kwamba mmeunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya maelezo mazuri aliyoyotoa Mheshimiwa Waziri kuhusu hili la watu wa hati za Kimila kuachwa, ukweli ni kwamba tumeweka kile kifungu pale makusudi ili kutokuleta mkanganyiko; kwamba je, Sheria hii pia itatumika na kwa hati za kimila? Hati za kimila zina sheria yake mahususi, Sheria ya Ardhi ya Vijiji. Ukisoma ile Sheria

ya Ardhi ya Vijiji ya Mwaka 1999 inaweka utaratibu wote wa matumizi ya hati hizo za kimila; na Sheria ile inatambua kwamba hati ile ina hadhi sawa na hati ya Kiserikali ya kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la watakaowajibishwa namna gani ya kuwawajibisha hawa waliochukua mikopo kwa kutumia hati hizi lakini ardhi haikuendelezwa. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ameshasema, kuna kitu kimoja hiki nadhani hakikueleweka vizuri. Kipindi cha ndani ya miezi sita, huyu anayechukua mkopo anatakiwa tu kuwasilisha kwa Kamishna utaratibu na namna gani atakavyoutumia huo mkopo wake, si kwamba sasa ndiyo anatakiwa aeleze jinsi ambavyo ameendeleza hiyo ardhi. Miezi sita haiwezekani, ni muda mdogo sana na utaratibu wa namna gani na kusimamia utawekwa kwenye kanuni na Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo hilo nalo niliona nilitolee ufafanuzi kwa sababu lingeweza kuleta mkanganyiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kama kuna kitu nimekisahau hapa madam Waheshimiwa Wabunge wote wameunga mkono, kwa mara nyingine namshukuru Mwenyezi Mungu, niwashukuru sana Wabunge Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki na wewe mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Katibu!

**NDG. RAMADHANI ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**  
Kamati ya Bunge Zima.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Waheshimiwa tunaanza kazi yetu, kazi muhimu sana hii ya kutunga Sheria. Katibu!

### **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2017 yaani *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.5) Bill, 2017]***

*Ibara ya 1*

*Ibara ya 2*

*Ibara ya 3*

*Ibara ya 4*

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*Ibara Mpya ya 5*

*Ibara Mpya ya 6*

*(Ibara Mpya zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*Ibara Mpya ya 7*

*Ibara Mpya ya 8*

*(Ibara Mpya zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

*Ibara Mpya ya 9*

*(Ibara Mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*Ibara Mpya ya 10*

*(Ibara Mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 11  
Ibara Mpya ya 12

(Ibara Mpya zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara Mpya ya 13

**MWENYEKITI:** Haya tunaanza, tumsikilize mwenye marekebisho, Dokta Immaculate.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Napendekeza hiyo *clause* 12 tuitoe kabisa iwe *section 25A* ambayo inatoa mwongozo wa umri mpya wa kustaafu kwa wahadhiri wa vyuo vikuu, maprofesa na *medical specialist* au madaktari miaka hiyo 55 na 65, naomba tukitoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na-*propose deletion* ya *section 25B* naishukuru Serikali imezingatia na imeshatolewa

**MWENYEKITI:** Hoja yako ni nini? Unapewa nafasi katika Muswada unauchezea chezea tu hivi, eleza.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasubiri akubaliane na kuitoa au kutokuitoa...

**MWENYEKITI:** Hapana.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zangu ni tatu; ni kwamba nina *propose* tuitoe kwa sasa kwa sababu imewahi kabla ya kurekebisha maslahi ya hawa maprofesa, *senior lecturers* na madaktari. Kwa hiyo unam-*force* huyu mtalaam kuendelea kufanyakazi miaka mitano au 10 zaidi na unajua kabisa *life span* yetu ikoje na maisha ya hawa watalaam wetu ni tatanishi. Kwa hiyo unazidi kumbana kwa nini usimpe mafao yake *then* ana-*choice* ya kuendelea kama anataka? Sasa hivi tuna *system* ya kufanya *consultancies* na pia tunawapa mikataba ya



miaka miwili miwili sasa kwa nini uendeleze umaskini na maisha duni ya hawa watalaam wetu ambao tunawahitaji kwa kuwakandamizia sheria hii? Kwa hiyo nasema kwamba kwa sasa hivi turekebishe kwanza maslahi yao *then u-propose*, u-*extend* miaka yake ya kuzidi kuwa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo hoja yangu mahususi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Profesa Ndalichako.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niseme kwamba anachoki-*propose* Mheshimiwa Dkt. Semesi kuhusiana na hii hakuna uhusiano, kwa sababu ukiangalia takwimu ambazo tumezitoa kati ya maprofesa na wahadhiri waandamizi waliostaafu 395 ni 324 waliomba mikataba. Kwa hiyo suala la kusema kwamba wanakuwa na maslahi duni ni suala ambalo halipo kwa sababu wao wenyewe baada ya kustaafu miaka 60 wamekuwa wakiomba mikataba na hata kuna wengine walikuwa wanaendelea kuomba mikataba mpaka miaka 70 mpaka Serikali ikafikia kukataza kwamba mwisho wa kuomba mikataba ni miaka mitatu; yaani kwamba huwezi ukapata mikataba zaidi ya mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge waliunga mkono hoja hii, mimi naomba kwa maslahi mapana ya nchi yetu, kwa maslahi mapana ya elimu ya juu nchini na katika hali halisi ya kuongeza madaktari naomba Waheshimiwa Wabunge waunge mkono hoja hii, madaktari na maprofesa wastaafu kwa miaka 60 kwa hiari na miaka 65 kama ambavyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali amependekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dokta Semesi baada ya maelezo hayo bado una...

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kabisa nitaomba kutoa hoja Waheshimiwa Wabunge wenzangu wanisaidie kwenye hili kama Waziri hataridhia bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anachokisema Profesa Ndalichako kwamba wengi wa hawa maprofesa wanakwenda kimkataba miaka miwili, miwili lakini tukumbuke wanakuwa wameshapatiwa mafao yao, kwa hiyo wanakuwa wanajjendekeza ni kweli na sidhani kama Kamati za Bunge iliwaita wadau wahusika.

Mheshimiwa mwenyekiti, mimi nimetokea Chuo Kikuu cha Dar es salaam na nilipoona hii hoja niliwautiliza *seniors* wenzangu kule Ofisini, wote hapa tuko kwenye *group* la kikazi, wote wamekataa, *text* ninazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sidhani kama kuna wadau wahusika waliitwa wakaambiwa, hawajaitwa. Kwa sababu kama waliitwa hili *group* la *University of Dar es Salaam* wana-*stick to 60 years* kwa sababu baada ya hapo unapewa mafao yako *then* unaendeleza mkataba, unakuwa kimkataba miaka miwili miwili. Sasa huyu Profesa mnambana *for so long* kwenye mazingira ya kimaslahi hafifu halafu bado mna-*extend* ndiyo tunawahitaji lakini tuangalie *options* mbalimbali za ku-*recruit* ili kusiwe na hizi *gaps* na kutengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya hawa *scientist* wetu tunaowahitaji, madaktari na maprofesa

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mazingira yalivyo sasa hivi ni kubana, nafikiri ni *strategy* ya kubana matumizi *or something else* lakini si kimaslahi ya hawa maprofesa na madaktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Makamba, Mheshimiwa Masoud. Mheshimiwa Mtolea inatosha na Yosepha na Profesa Mwenyewe. Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Semesi Sware. Napata tabu kuona kwa nini Serikali wanashindwa kuelewa; kwa sababu dhamira ya kutaka kuongeza umri hallengi kumlazimisha mtu kutumikia hiyo kada ambayo anaifanyia kazi kwa muda mrefu. Bado lazima tuheshimu ile *willingness* ya mtu mwenyewe kufanya kazi. Sasa mtu akishafikia ukomo wake wa kustaafu ni vizuri akastaafu apate fursa ya ku-*enjoy* na yale mafao yake na Serikali kama itakuwa bado inamhitaji ndiyo kuna huo mlango mwingine wa mtu kum-*approach* kwa mkataba ama miaka miwili au miaka kadhaa kwa namna ambavyo mtaona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri hapa badala ya kuwalazimisha watu waende muda mrefu sana katika huu utumishi tuwaachie wapate nafasi ya wao kuamua kwamba sasa nipumzike au niendeleo kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua pale ambapo unastaafu kwa kufikia ukomo wa umri wa kufanya kazi ina heshima yake sana tofauti na ile ya kuomba kwamba ukomo ukifika na ndiyo ukaacha unapokuja kuomba tena inaonekana kwamba hukuwa na tamaa ya kuacha, umri ulifika lakini sasa tunavyoupandisha maana yake mtu akitaka kupumzika ili achukue hayo mafao yake ni lazima aombe kuacha jambo ambalo si zuri. Mtu anaweza kuonekana kwamba siyo mzalendo, ametaka kuacha kazi wakati kumbe tungeiacha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Masoud atafuatiwa na Mheshimiwa Makamba.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na mtoa hoja kwamba Serikali kwa hili waliangalie kwa umakini mkubwa. Kwanza suala zima la maslahi mapana juu ya hawa ambao tunawazungumza; na muda ukifika, pale ambapo hawa tunaowazungumza baada ya kuwapatia maslahi yao vizuri, ile *package* ambayo inatajikana baadae kutakuwa na uhuru unaohitajika nini cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni kwamba kwenye *contact* basi kutakuwa na jambo lingine ambalo wao wenyewe kwa kipindi hicho ndiyo kitakachoweza kuwapa motisha ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa mtoa hoja mambo haya tuyaangalie iliyo nzuri ili waweze...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Sware na nataka niseme ukweli, Mheshimiwa Waziri hawa watu hawajakuwa-*consulted*. Hawa watu maoni yao hayajazingatiwa, kwanza hawajaitishwa maoni yao na hayajazingatiwa; na kama yamefanyika siyo kwa kiwango ambacho kinatakiwa kifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ya maslahi ya maisha ya watu. Unayemuongezea ni Profesa, mtaalam, kuna mdau mmoja kwenye kitabu cha Kambi amesema Daktari mwenye miaka 60, uwezo wake wa kufanya upasuaji hauwezi kuwa sawa na Daktari mwenye miaka 40 na 50. Mnalazimisha hili jambo lakini hatujalifanyia utafiti wa kina. Nadhani hapa *ajenda* ya siri ni mafao ya kuwalipa hawa Madaktari kwa sababu naona tumeshaelekeza mifuko yote sasa tupeleke hela kwenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tunakosa pesa kwa ajili ya kuwalipa mafao. Walipeni mafao yao kwanza halafu mkae nao mkubaliane nao. Tusiwalazimishe hawa watu mtu aende mpaka miaka 65 wengine wanasema mpaka miaka 70...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naona nisiunge mkono hoja iliyoweka mbele yetu kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sasa hivi umri wa kustaafu kwa lazima ni miaka 60 na hiari ndiyo ilikuwa 55, lakini uzoefu hata baada ya kufika 60 ya lazima bado kwa asilimia 82 watu wanaomba mikataba kwa mujibu wa takwimu za Profesa Ndalichako. Kama asilimia 82 wanaomba mikataba *that means* kuna haja, kuna tatizo la kuiweka kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona hapa ni kwamba ukiwekwa kwa mkataba unachokuja kulipwa baadaye ni kikubwa zaidi ambacho ni gharama kwa Serikali kwa hiyo Mheshimiwa kama wana uwezo wa kuingia kwa mikataba kwa asilimia 82 tuweke kisheria ili wao waweze kutumia ule ujuzi lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Maghembe.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa nafasi hii. Ningependa nisiunge mkono hoja iliyowekwa mezani kwa sababu mapendekezo ni kustaafu katika umri wa miaka 65, lakini

ukifika miaka 60 kama nia yako ni kupokea mafao yako basi unaweza ku-*opt* ukapokea mafao yako, kwa hiyo hakuna mtu anayelazimishwa kwenda mpak 65 kwa sababu ile fursa ya kupata mafao yako ukiwa miaka 60 iko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa maelezo fasaha. Mheshimiwa Waziri Ndalichako.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami siungi mkono hoja hii. Kwanza suala la kusema kwamba wadau hawakushirikishwa kazi ya kuita wadau wa kutoa maoni huwa ni kazi ya Bunge na siyo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili; takwimu zimejiweka wazi na mimi natamani hawa ambao wanasema kwamba wahadhiri hawahitaji kuongezewa muda wangetoa takwimu. Hii ni kwa sababu kwa takwimu nilizonazo mimi ni Waziri mwenye dhamana sijawahi kuona Profesa akiwa na miaka 55 akaomba kustaafu kwa hiari na wamekuwa baada ya miaka 60 wanaomba kuendelea. Kwa hiyo tunachokifanya ni kurasimisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Makamu Wakuu wa Vyuho, walifanya utafiti na wakaona kuna umuhimu. Kwa hiyo, naomba kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge waliunga mkono niombe Bunge lako lipitisha huu Muswada kwa maslahi mapana ya elimu yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenye hoja, Mheshimiwa Dokta Semesi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi.

**MWENYEKITI:** Umeshaelimishwa vizuri?

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Ni hivi; nilipoanza mwanzoni ulivyosema ni-*justify* nilisema hiki kifungu kimewahishwa. Ni bora kurekebisha kwanza maslahi ya hawa walengwa *then* hiki kifungu ndipo labda kije. Kwa sababu hata wanapo-*retire* kama ni *voluntary* miaka 55 au hii ya *proposal* sasa hivi miaka 60, sawa ana-*retire* halafu anapewa *package* yake si ndiyo? Halafu anafanya anachokitaka baada ya hapo ana-*option* ya kupata mkataba na malipo ya mkataba yako juu kuliko *the normal salary* ambayo alikuwa anaipata, kwa hiyo *obviously* nitaomba mkataba, nitaomba *extension* mikataba ndiyo hiyo asilimia 80 unayoiongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tusitumie hicho kigezo kwamba ni asilimia 80 wanaomba kwa sababu eti hawana kazi, no! Ni maslahi. Kwa hiyo turekebishe kwanza maslahi then hiki kifungu kije.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante, sasa nitawahoji, kuhusu hoja ya Mheshimiwa Dkt. Semesi kuhusiana na kufutwa kwa kifungu cha 25A cha Muswada.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Ibara Mpya iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imemaliza kazi yake.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja taarifa

## T A A R I F A

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 89(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa mwaka 2017 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No.5, Bill of 2017*) ibara kwa ibara na kuukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho Mbalimbali Na.5 wa mwaka 2017 (*The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 5, Bill of 2017*) kama ulivyorekebisha katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono. Katika hatua hii lazima hoja hii muamue. Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Walioafiki wameshindwa. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ABDALLAH-KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria Mbalimbali kwa Lengo la Kuondoa Mapungufu



ambayo yamejitokeza katika Sheria hizo Wakati wa Utekelezaji wa Baadhi ya Masharti katika Sheria hizo (*A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws*)

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulipitishwa na Bunge*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge Muswada huu sasa umepitishwa rasmi na Bunge hili na utafuata hatua za kikatiba na kikanuni ili ukapate pia idhini ya upande wa pili wa Bunge kwa maana ya Mheshimiwa Rais.

Niwashukuruni kwa kazi nzuri tuliyoifanya pamoja; na kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, ukiona maudhui yake ni kidogo, machache lakini *very loaded* lakini yana maslahi mapana sana kwa nchi hii. Tunatofautiana kidogo lakini mtaona faida ya marekebisho hayo.

Waheshimiwa Wabunge, sina la ziada kwa maana ya taarifa, kwa hiyo, baada ya kusema hayo sasa naahirisha Bunge hadi kesho siku ya Jumatano, tarehe 31 mwezi huu saa 3.00 asubuhi .

(*Saa 7.49 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 31 Januari, 2018, Saa Tatu Asubuhi*)